# Nipashe

Jumanne Julai 9, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579965

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Wabunge watoro majimboni CCM kutoswa uchaguzi 2020

UKURASA 3


Nipashe
TESA
JE, WAJUA?
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Mzazi mtie moyo mwanao anapofanya vibaya masomoni
Matumizi yaliyokithiri ya simu chanzo wanafunzi kuwa na wapenzi wengi?
IMANI HIZI KUHUSU DHAMANA ZIPUUZWE

UKURASA 13

# Mpango afichua wizi hatari ndani ya benki

**AWEKA** wazi mtandao unavyofanya kazi ndani na nje, aipa neno zito NMB ikitoa gawio kwa serikali... *Endelea ukurasa wa 2*

## AJALI ILIVYOFUPISHA UHAI WATUMISHI WATANO AZAM





**FLORANCE** BITALIHO NDIBALEMA



**CHARLES** WANDWI



**SAID** HAJI HASSAN



**SALIM** JUMA MHANDO



**SILVANUS** WAZIRI KASSONGO



UKURASA 2

# Msako msaidizi Membe waanza

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA, YANGA DIMBANI JAN. 4 UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Mpango aanika wizi hatari benki

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amefichua wizi unaofanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu wa benki na mitandao ya kimataifa ya wizi.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati akipokea gawio la serikali kutoka Benki ya NMB la Sh. bilioni 10.48.

Alisema suala la uaminifu wa watumishi wa benki ni muhimu kwa taasisi zote za fedha na kwamba kuna taasisi wananchi wanazilalamikia.

"Wanalalamika ukifuatilia kwa karibu ni kwa sababu ya watumishi wa benki si waadilifu. Mimi ninazo kesi za watu ambao anaweka fedha zao benki, yuko mmoja kesi yake ya ovyo sana tumetuma vyombo vya dola vifanye kazi yake," alisema.

"Siku hiyo walimteka kwa makusudi na siku ile ile waliyomkamata ndiyo siku mtumishi wa benki akahamisha fedha yake na kupeleka benki nyingine, zimefuatiliwa huko nako zimeondolewa na kupelekwa kwingine, hii ni kwa sababu ya watendaji wa benki si waaminifu," aliongeza.

Hata hivyo, Dk. Mpango alisema benki hiyo si NMB na kusisitiza kuwa suala hilo halikubaliki.

"Wapo Watanzania wanaibiwa fedha kwenye ATM. Kwa mfano Makamba (Katibu wake) huyu ni mmoja ambaye tulikuwa tunasafiri kutoka Dar es Salaam kuja hapa (Dodoma) tukiwa njiani akaunti yake ilikuwa inatoa (deducted) fedha mara tatu NMB akawa anahangaika bahati nzuri meneja mmoja akamsaidia 'kublock' (kuzuia)," alisema.

Waziri alisema Makamba alipoangalia alikuta fedha zimetolewa mara tatu na akawa anapata ujumbe kwenye simu na wizi huo ulikuwa unafanywa na mtandao wa kimataifa.

"Tulifuatilia tukagundua zile fedha zilikuwa zinakatwa Vietnam, maana yake ni kwamba muwe makini na mitandao ya kihalifu ya kimataifa, ipo ya ndani na kimataifa," alisema.

"Kuna mama naye namfahamu, zilikuwa zinaondoka hivyo hivyo. Tulikuja kufuatilia tukakuta zinatolewa Zimbabwe, muwe macho wale wataalamu wenu wa IT (teknolojia ya habari), lazima kulinda amana za wananchi wetu hawa maskini."

Aliwataka kuhakikisha wanalinda wizi huo na pale wanapoajiri wahakikishe wanawafanyia uchunguzi wa kina watumishi wa benki.

**KUPANUA HUDUMA**

Dk. Mpango alisema Rais alipokutana na wafanyabiashara walisema wanatamani kufanya biashara nchi jirani lakini huduma za benki hazipo na kuwataka kuangalia

INAENDELEA UK 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Waziri Mkuu wa Misri, Dk. Moustafa Madbuoly, alipowasili jijini Cairo, jana, kwa ziara ya kikazi ya siku tatu. **PICHA: OWM**

# Ajali ilivyofupisha uhai watumishi Azam

**Na Mary Geoffrey**

WATU saba wakiwamo wafanyakazi watano wa kampuni ya Azam Media, wamefariki dunia papo hapo katika ajali iliyohusisha basi dogo aina ya Toyota Coaster lililokuwa likitoka Dar es Salaam kwenda Chato mkoani Geita, kugongana uso kwa uso na lori la mizigo.

Mbali na vifo hivyo wafanyakazi wengine watatu wamejeruhiwa vibaya na walipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora kwa matibabu.

Ajali hiyo, kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Peter Kakamba, ilitokea jana saa 2:30 asubuhi katika eneo la Kizonzo, katikati ya Igunga mkoani Tabora na Shelui mkoani Singida.

Wafanyakazi hao wa Azam Media walikuwa safarini kikazi kwenda kwenye hafla ya uzinduzi ya hifadhi mpya ya Burigi, ambayo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais John Magufuli. Walikuwa wakitarajia kurusha matangazo ya moja kwa moja ya hafla hiyo inayofanyika leo.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu ajali hiyo, Kamanda Kakamba alisema: "Nipo eneo la tukio ni kweli watu saba wamefariki dunia, wakiwamo wafanyakazi wa Azam TV. Bado tunaendelea na uchunguzi wa kutambua majina yao na majeruhi watatu wamekimbizwa (wamepelekwa) hospitalini kwa sababu hali zao ni mbaya sana."

Kuhusu chanzo cha ajali hiyo, alisema bado wanaendelea na uchunguzi kabla ya kutoa taarifa kamili.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Tido Mhando, alithibitisha kupoteza taarifa za wafanyakazi wake watano pamoja na madereva wawili wa gari hilo la kukodi.

Aliwataja wafanyakazi hao waliopoteza maisha kuwa ni wapigapicha wawili, Said Haji na Charles Wandwi na mafundi mitambo Salim Mhando, Florence Ndibalema na Sylvanus Kasongo.

Mhando pia aliwataja waliojeruhiwa ni mpigapicha Mohamed Mwinshehe na Mhandisi Artus Massawe.

Alisema Shirika la Hifadhi ya Taifa (Tanapa) linaandaa helikopta maalum ya kuchukua maiti na majeruhi ambao wako katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga kwa ajili ya kuwapeleka Hospitali ya Taifa Muhimbili. Hata hivyo, hadi gazeti hili linaenda mitamboni walikuwa hawajafikishwa Muhimbili.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya

INAENDELEA UK 8

# Coaster yaua 4, Polisi yaua mtuhumiwa wa ujambazi

**Na Alphonce Kabilondo, GEITA**

WATU wanne wamefariki dunia katika ajali ya barabarani mkoani Geita.

Tukio lilitokea jana asubuhi wakati gari aina ya Coaster mali ya kampuni ya Kabaya l namba T550 DED ikitokea Kijiji cha Kakubilo Senta kwenda Mjini Geita kuacha njia kisha kupinduka na kusababisha vifo vya watu wanne na wengine 40 kujeruhiwa na kulazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Mosses Simeo, alithibitisha kupokea miili minne na majeruhi 40, na kwamba majeruhi wawili wana hali mbaya na walitarajiwa kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Bugando jijini Mwanza.

Dk. Simeo alisema majeruhi wengine wanaendelea na matibabu, na baadhi wanaweza kuruhusiwa wakati wowote.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Lotson Mponjoli, alisema waliofariki dunia ni watoto wawili na wanaume wawili na ambao hata hivyo, majina yao hayajafahamika.

Aidha, katika tukio la pili mtu mmoja anayedaiwa kuwa jambazi, ameuawa na polisi katika majibizano ya risasi.

Kamanda huyo alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku katika Mtaa wa Katundu Mjini Geita, ambapo mwanaume mmoja anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 35 anadaiwa kuwa jambazi ambaye hakufahamika jina wala makazi yake, aliuawa katika majibizano ya risasi na askari polisi.

Kamanda huyo alisema katika majibizano hayo, watuhumiwa watatu wa ujambazi walifanikiwa kutoroka katika eneo hilo na kutokomea kusikojulikana.

Aidha, Kamanda Mponjoli alisema askari walifika eneo hilo baada ya kupata taarifa kutoka kwa raia wema kuwa kuna kundi la majambazi watano wanataka kuvamia kwenye maduka ya M-PESA, na kuwakuta wanne.

Alieleza kuwa mmoja aliyekuwa na bastola aina ya Browing namba 558484 ikiwa na risasi tatu ndani ya magazine pamoja na maganda mawili, aliuawa katika majibizano hayo.

Amesema kuwa uchunguzi wa awali umebaini kuwa silaha hiyo ni kutoka jijini Mwanza na inadaiwa kutumiwa katika matukio mbalimbali ya uhalifu katika maeneo ya Mji wa Geita na jijini Mwanza.

## HABARI KITAIFA

# Wabunge watoro CCM kutoswa 2020

Na Mary Geofrey

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetishia kukata majina ya wabunge na madiwani ambao wanashindwa kufika kwenye majimbo na kata zao kusikiliza kero zinazowakabili wananchi.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally (pichani), alitoa tahadhari hiyo juzi wakati akizungumza na wanachama wa chama hicho katika mkutano wa hadhara uliofanyika wilayani Siha, Kilimanjaro.

Alisema viongozi wa chama hicho wenye tabia hizo, wasahau kuteuliwa na chama kuwania nafasi hizo kwa sababu CCM ndicho chama chenye jukumu la kusimamia shughuli zinazofanywa na viongozi hao.

"Bungeni wamekuwa wakienda bila kukosa kwa sababu Mheshimiwa Spika anafuata kanuni na sheria kwa wasioenda bungeni na mimi naanza sasa kufuata kanuni za chama wasioenda majimboni, kwenye kata. Wabunge na madiwani wa CCM wasahau uteuzi wa chama kugombea nafasi hizo tena," alisema Dk. Bashiru.

Alisema haiwezekani wabunge na madiwani wanaochaguliwa na wananchi kushindwa kwenda kusikiliza kero zao na kufananisha kitendo hicho na usaliti usiokubalika.

"Huo ubunge wao ni wa CCM na CCM imepata ubunge huo kwa wananchi, hivyo



tuna wajibu wa kurudi kwao. Wabunge wamekuwa wakienda bungeni kwa sababu wasipoenda bungeni wananyimwa posho huku kwa wananchi hawaji," alisema.

Alisema ili kuondokana na changamoto hiyo, wabunge na madiwani wawasilishe ratiba za ziara katika majimbo na kata zao kwenye chama na watakapofanya ziara wawasilishe kwa viongozi na kuainisha maeneo waliyotembelea.

"Wote waandae ratiba ya ziara kwenye majimbo yao na wafanye ziara na walete taarifa kwenye chama kuwa wametembelea maeneo gani kwa sababu walipata ubunge au udiwani kupitia CCM, hivyo aliyechaguliwa hana hiari ya kutofanya ziara katika jimbo lake," alisema.

# Msako wa msaidizi wa Membe waanza

Na Romana Mallya

SIKU moja baada ya kuzagaa mtandaoni taarifa za kutekwa kwa Allan Kiluvya, msaidizi wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, Jeshi la Polisi limesema linaendelea na uchunguzi, huku likiomba mwananchi mwenye taarifa mahali alipo, wawasiliane nao.

Juzi, kulizagaa taarifa mitandaoni ikidai Allan alitekwa na watu wasiojulikana maeneo ya Mbezi Jogoo, jijini Dar es Salaam nje ya nyumba ya rafiki wake.

Taarifa hiyo ilitolewa na mwanamke aliyejitambulisha kwa jina moja la Magreth, mkazi wa Jogoo, ambaye ndiye rafiki yake alijirekodi akielezea namna alivyotekwa kisha kusambaza taarifa hiyo mtandaoni.

Akizungumza na Nipashe jana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Musa Taibu, alisema wamepokea taarifa hizo na kueleza kuwa wanaendelea kuzifanyia kazi.

"Taarifa tumezipata na tunaendelea kuzifanyia kazi, lakini tunaomba hata wewe mwandishi kama una taarifa au fununu wapi alipo utusaidie, kama kuna mwananchi ana taarifa alipo wawasiliane nasi. Lengo ni apatikane," alisema.

Juzi, Kamanda Taibu alipoulizwa alisema tukio hilo ni jipya kwake.

"Ninashangaa sijui kuna wimbi gani, huyu shetani sijui anatoka wapi? Nitafuatilia kama kuna ukweli wowote ila kwangu bado halijanifikia," Kamanda Taibu alisema.

Katika maelezo yake Magreth aliyojirekodi kuhusiana na tukio hilo alidai alikuwa yeye dada yake Agnes pamoja na Allan, katika hoteli ya Juliana iliyopo Mbezi Africana.

"Nilikuwa mimi, Allan na dada yangu mwingine anaitwa Agnes, tulikuwa hoteli ya Juliana kule Africana, baada ya kunywa ulifika muda wa kwenda nyumbani, Allan akasema atatupeleka, siyo mbali na hapo Juliana, ni Jogoo kituo kinachofuata. Alitupeleka hadi nyumbani, nikashuka na kufungua geti akaingiza gari akashuka Allan na dada yangu."

Magreth aliendelea kusimulia: "Allan alitaka kumsalimia mama yake ambaye wakati huo alikuwa hajalala, alimsalimia wakaongea muda wa kuondoka aliniambia nimfungulie geti ili atoke, nilifungua na kulifunga, nilikuwa nimemuomba fedha, si unajua ile kikaka kaka aniachie pocket money 'fedha za matumizi' kidogo, akaniambia niende nje tuongee. Akarudi kinyume nyume, nikafunga geti, nikatoka nje. Nilipotoka nikasogelea gari lake kwa mbele

INAENDELEA UK 8




# Wafugaji wa vipepeo waomba kuuza nje

**Na Mwandishi Wetu, SAME**

WAFUGAJI na wauzaji wa vipepeo kutoka Kijiji cha Bwambo, wilayani Same, wameiomba serikali kufungua soko la vipepeo lililoanza kuwaingizia kipato na kuwafanya waache kuvamia Msitu wa Hifadhi ya Mazingira ya Asili Chome.

Mradi wa ufugaji wa vipepeo ambao umeonyesha kuwa na soko nzuri nje ya nchi, ulianza kijijini Bwambo mwaka 2012 chini ya ufadhili wa Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) na tangu wakati huo, umeonyesha kuungwa mkono na wanakijiji wengi.

Katibu wa Kikundi cha Wafugaji wa Vipepeo Bwambo, Msese Mbwambo, alisema jana kuwa tatizo kubwa linalowakabili kwa sasa katika shughuli hiyo ni ukosefu wa soko la uhakika.

Alisema soko kubwa la vipepeo liko nje ya nchi lakini kwa muda sasa serikali imezuia uuzaji wa viumbe hai nje ya nchi.

"Soko ndilo linatupa shida. Awali tulikuwa tunauza lakini sasa soko limekuwa shida, tunaomba serikali itufikirie kuhusu huu mradi kwa maana tulishaanza kuona faida yake," alisema na kuongeza karibu tangu Januari, mwaka huu hadi sasa, hawana soko la uhakika la vipepeo wanavyofuga.

Naye mkazi wa kijiji hicho, Emmanuel Mbwambo, alisema walianza kupata matunda ya mradi huo mwaka 2016 baada ya kuanza kuuza mabuu (pupae). Buu ni hatua ya tatu baada ya yai na lava kabla ya kuwa kipepeo kamili.

Alisema awali walikuwa wakipeleka mabuu Amani, Muheza mkoani Tanga ambako kulikuwa na mnunuzi aliyekuwa akiuza nje ya nchi lakini kwa sasa imekuwa ngumu.

Mwaka 2018, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Profesa Jumanne Maghembe, alipiga marufuku uuzaji na usafirishaji wa viumbe hai nje ya nchi, marufuku ambayo ilipigiliwa msumari na waziri wa sasa wa wizara hiyo, Dk. Hamis Kigwangala, mjini Dodoma Machi, mwaka huu.

Mratibu wa EAMCEF Kanda ya Mashariki, Magreth Victor, alisema mradi wa ufugaji wa vipepeo ni mmoja kati ya mradi ambayo imelenga kuwapatia kipato wananchi ili wasivamie na kuharibu misitu ya hifadhi asili. Alisema hayo wakati yeye na timu yake walipotembelea na kujionea miradi wanayoifadhili katika maeneo hayo, mwishoni mwa wiki.

Alisema mfuko umeamua kuwezesha miradi ya wakazi wa vijiji jirani na Misitu ya Hifadhi Asili ya Tao la Mashariki baada ya awali kubaini kuwepo kwa uharibifu wa mazingira yake.

Alisema Milima ya Tao la Mashariki inatambulika kitaifa na kimataifa kwa sababu ya kuwa tajiri wa bionuai, hivyo waliamua kuwawezesha wakazi wanaoishi vijiji jirani na misitu hiyo miradi ya kuwapatia kipato ili kuendesha maisha yao hatua ambayo imesaidia kupunguza uvamizi katika misitu hiyo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, John Nnko, ambaye ni Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili, alisema halmashauri hiyo ikishirikiana vizuri na EAMCEF kusaidiana na wakazi wa vijiji vinavyozunguka misitu hiyo kwa kuanzisha miradi ya kuwaingizia kipato.

# Tanesco kuweka umeme kwenye mashamba miwa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limeahidi kuweka umeme katika mashamba ya miwa ya Mkulazi yanayomilikiwa kwa ubia kati ya Jeshi la Magereza nchini na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kupitia Kampuni Hodhi ya Mkulazi, ili kurahisisha shughuli za umwagiliaji.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Dk. Tito Mwinuka, alipotembelea mashamba hayo mwishoni mwa wiki iliyopita.

Alisema Tanesco itapeleka umeme ili kufanikisha kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha kwa vipindi vyote vya msimu wa mwaka.

"Sisi tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba tunaleta umeme kwa wakati mwafaka, ili shughuli zao za kukuza miwa na hatimaye kuja kuanzisha kiwanda zisije kukwama kwa hiyo nawaahidi kwamba hatutawaangusha katika kuleta umeme katika eneo hili," alisema Dk. Mwinuka.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alimshukuru Mkurugenzi wa Tanesco kwa kuahidi kupeleka umeme katika mashamba ya Mkulazi kwa kuwa itarahisisha kilimo cha umwagiliaji.

"Tunashukuru kwamba wametuhakikishia kabla ya mwisho wa mwezi wa nane umeme utakuwa umefika katika maeneo yote haya mawili na tutaweza kuendelea na hatua zinazofata za uwekezaji huu," alisema Erio.

Aidha, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, Phaustine Kasike, alibainisha namna Jeshi la Magereza lilivyojipanga kuhakikisha zao la miwa linalimwa kwa wakati na kwa wingi zaidi.

"Shamba hili linahudumiwa na wafungwa, shughuli zote ambazo zinaendeshwa katika shamba hili zinafanywa na wafungwa kwa hivyo tunauwezo mkubwa wa kuendelea kutekeleza majukumu haya na tunahakikisha kwamba tutafanikisha kulingana na malengo ambayo yamepangwa," alisema Kamishna Kasike.

Dk. Mwinuka alitumia fursa hiyo kukagua maandalizi ya eneo ambalo kiwanda chasukari kitajengwa na shamba la Mbigiri ambalo tayari limeshapandwa miwa.




Ofisa Uhusiano Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF), Fatma Elhady na Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa Mfuko huo, Abdul Njaidi, wakiwasikiliza wananchi waliotembelea banda la mfuko huo, kwenye Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa kwenye viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magunia 200 mkaa yanaswa kwenye majahazi

**Na Robert Temaliiwa, BAGAMOYO**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Bagamoyo, wamekamata majahazi mawili yaliyokuwa yamebeba mkaa zaidi ya magunia 200 katika bandari bubu ya Mto Shanga, kitongoji cha Razaba Kata ya Makulunge.

Meneja wa TFS Wilaya ya Bagamoyo, Ally Khalfani, alisema mkaa huo ulivunwa bila kufuata utaratibu na ni kinyume cha Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002 na Mwongozo wa Uvunaji wa Mazao ya Misitu wa mwaka 2017.

Khalfan alisema kukamatwa kwa majahazi hayo ni mwendelezo wa doria zinazofanywa na kikosi cha TFS kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ili kubaini watoroshaji wa mazao ya misitu.

Hivi karibuni, TFS ilikamata basi la abiria lenye namba za usajili T 612 DFU likiwa limebeba magunia 18 ya mkaa kinyume cha sheria.

Akizungumza baada ya kufika eneo la tukio hilo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Bagamoyo, Kasilda Mgeni, aliwataka wananchi wilayani hapa kufuata sheria za uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu ili kuepuka usumbufu ambao wanaweza kuupata.

Mgeni alisema watakaokiuka sheria za uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu serikali itawachukulia hatua za kisheria.

Alisema kutofuata sheria katika uvunaji wa misitu kunasababisha uvunaji holela jambo ambalo ni hatari kwa ustawi wa mazingira.

Katibu Tawala alisema misitu inahifadhiwa kwa ajili ya utunzaji wa mazingira, hivyo shughuli zote za uvunaji wa mazao ya misitu ni lazima zifuate sheria na kupata maelekezo kutoka kwa wataalamu wa misitu.

Aliongeza kuwa uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uvunaji holela utasababisha kuwa na maeneo yenye majangwa na kukosa mvua kwa wakati jambo ambalo pia litasababisha ukame wa mazao ya binadamu na wanyama.

Mgeni pia alibainisha kuwa utoroshaji wa mazao ya misitu unasababisha pia kuikosesha serikali mapato ambayo kimsingi ndiyo yanategemewa kuleta maendeleo katika jamii.

Kwa mujibu wa Mgeni, serikali haikatazi wananchi kufanya shughuli zao lakini kinachotakiwa ni kufuata sheria na taratibu zilizowekwa ili mwananchi ajiongezee kipato, mazingira yatunzwe huku serikali ikiwa inaingiza mapato kwa ajili utekelezaji wa huduma za jamii.

# TCCIA INVESTMENT PLC

P. O. Box 72678 Dar es Salaam, Tanzania Tel: 255 – 22 – 2138048/2138049 Fax: 255 – 22 – 2119437
Email: info@tcciainvest.co.tz, Web site: http://www.tcciainvest.co.tz

## YAH: TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 10 AUGUSTI 2019, KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KARIMJEE, DAR-ES- SALAAM, SAA TATU ASUBUHI

Tanapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 10 Augusti, 2019 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Karimjee, Dar-es-Salaam. Mkutano utaanza saa tatu (3.00) asubuhi. .

**Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne ni:**

14.1 Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne.

14.2 Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne.

14.3 Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2018.

14.4 Kupokea, kujadili na kuridhia Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu uliofanyika tarehe **30 Novemba, 2018.**

14.5 Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018.

14.6 Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018.

14.7 Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu Uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Desemba, 2019 pamoja na Malipo yake.

14.8 Kupokea na kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu Gawio kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2018.

14.9 Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi (Directors Fees).

14.10 Kupokea, kujadili na kuamua kuhusu Dondoo mbalimbali zitakazokuwa zimewasilishwa na wanahisa kabla ya tarehe 22 Julai, 2019.

14.11 Kufunga Mkutano wa Kumi na Nne.
Mwisho tunapenda kuchukua fursa hii kuwahimiza wanahisa kuhudhuria Mkutano huu muhimu.

**Angalizo:**

1. Mwanahisa atakayehudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne atatakiwa kujigharamia mwenyewe. Hii ni pamoja na usafiri, malazi na chakula.
2. Mwanahisa anatakiwa aje na Cheti chake cha Hisa pamoja na kitambulisho chake, ambacho ni aidha Kitambulisho cha Uraia, Kitambulisho cha Mpiga Kura,Hati ya Kusafiria, Leseni ya Udereva au barua ya Utambulisho iliyotolewa na Afisa Mtendaji au Mwenyekiti wa Mtaa anakoishi.
3. Mwanahisa anayestahili kuhudhuria Mkutano Mkuu na kupiga kura lakini akashindwa kuhudhuria kutokana na sababu mbalimbali anaweza kuwasilisha jina la Mbadala wake yaani **"Proxy"** kabla ya tarehe 27 Julai,2019. Fomu ya Proxy imeambatanishwa kwenye Taarifa hii.
4. Tunarudia na kusisitiza kuwa Dondoo za Wanahisa zitakazojadiliwa ni zile ambazo zitawasilishwa kabla ya tarehe 27 Julai, 2019 tu.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi

**Donald J. Kamori**
**Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi**

215213302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Makamanda wa polisi sasa wasimamie agizo la Lugola*

**Juzi** Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, aligusia kero kubwa na ya miaka mingi kwa wasafiri wa mabasi ya kwenda katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Waziri huyo alitangaza kuwapiga marufuku makamanda wa polisi wa mikoa nchini kuyazuia mabasi yanayotoka mikoa ya Kanda ya Ziwa kwenda Dar es a Salaam au kurudi Kanda ya Ziwa kusafiri wakati wa usiku kwa kisingizio cha kuhofia yatavamiwa na majambazi.

Hatua hii ya Waziri Lugola ni ya ujasiri wa aina yake, ambao unapaswa kuonyeshwa na Jeshi la Polisi hasa katika kipindi hiki kilichotawaliwa kwa sayansi na teknolojia.

Lugola alieleza bayana kuwa Jeshi la Polisi lipo imara na kamwe haliwezi kucheka na majambazi wala kuwaonea huruma na kuwapa nafasi ya kuwapangia muda gani mabasi yasafiri na yasisafiri, mabasi hayo yanapaswa kusafiri saa 24.

Kauli hiyo ya ujasiri Lugola aliitoa katika mkutano wa hadhara Kijiji cha Namibu Kata ya Neruma, Jimbo la Mwibara, wilayani Bunda.

Tunapongeza kwa hatua hiyo kwa kuwa ameonyesha ukomavu akiwa kiongozi mwenye dhamana, na anayesikiliza na kuchukua hatia za kutafutia ufumbuzi wa kero mbalimbali zinazowakwaza wananchi.

Kimsingi, kuzuia mabasi kulikuwa kunawaongezea tabu wasafiri, ikiwamo kuwachelewesha kufika wanakopwenda.

Hatua ya kuzuia Morogoro mabasi yanayosafiri kutoka Kanda ya Ziwa kwenda Dar es Salaam wakati yale yanayotoka Dar es Salaam kwenda Kanda ya Ziwa yalikuwa yakizuiliwa Shinyanga kabla ya saa sita usiku ikidaiwa kuwa ni sababu za kiusalama.

Lugola alijinasibu kuwa akiwa ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hawezi kupangiwa ratiba ya kusafiri na majambazi.

Alibainisha kuwa Serikali ya Rais Magufuli ipo imara, na polisi ipo imara, hivyo agizo hili ambalo pia aliwahi kulitoa lizingatiwe ipasavyo.

Alikumbusha kuwa alitoa maagizo kuwa majambazi wote wasambaratishwe, wasakwe mpaka jambazi wa mwisho, akamatwe kama kuku.

Lugola amelitaka Jeshi la Polisi lihakikishe linawashughulikia majambazi mmoja baada ya mwingine ili kuwafanya wananchi katika nchi yao waendelee kushughulika na masuala ya kujijengea uchumi.

Katika karne hii ya sayansi na teknolojia Jeshi la Polisi linaweza kuwa na mbinu nyingi za kujipanga vyema kuhakikisha kuwa hatua hiyo inatekelezwa vizuri.

Pia Polisi wana uwezo wa kutosha kuwapa elimu madereva, makondakta na abiria jinsi gani wanaweza kutumia simu zao za mikononi za kisasa kutoa taarifa haraka mara wanapovamiwa.

Tunaamini kwamba jeshi letu ni la kisasa, hivyo lina vifaa vya kisasa ambavyo vinawapa uwezo mzuri wa kutumia simu za mkononi katika kuwatega na kuwabaini majambazi iwapo wataibuka kwa namna yoyote.


Pia hamasa iliyopo kwenye jamii katika maeneo mengi nchini kuna polisi jamii au sungusungu nao ni vyema vikiimarishwa na kupewa elimu zaidi ili wajipange vyema kwenye malindo yao yaliyopo jirani na barabara kuu.

Hatua hii ya Waziri Lugola inapaswa kuungwa mkono kwa utekelezaji unaoshirikisha pembe tatu ambazo ni askari polisi, madereva na wamiliki wa vyombo hizo pia na abiria wenyewe kuwa makini miongoni mwao wanapokuwa safarini.

Lakini wawajibikaji wakuu wawe ni makamanda wa polisi wa mikoa ambao wanapaswa kutekeleza agizo la waziri kuhakikisha hawayazuii mabasi kusafiri usiku, lakini pia kuhakikisha maeneo yao ni salama kwa abiria kusafiri usiku.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wawakilishi wawasemee wakulima ili pamba yao inunuliwe 'keshi'

Na Raphael Kibiriti

KIMSINGI kuna uhalali kwa maoni ya Muungwana kuzungumzia ustawi wa wakulima nchini.

Zipo sababu zinazohalalisha kuwasemea wakulima na hasa pale maslahi yao yanapoonekana kuwekwa pembeni.

Sababu ya kwanza ni kwamba kilimo ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi inayochukua kundi kubwa la Watanzania.

Asilimia takribani 70 ya raia wa taifa hili wanategemea kilimo kama chanzo cha mapato ya kujiendeleza kimaisha.

Vilevile katika dhima nzima ya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025, adui umaskini anahitajika kupigwa vita kwa nguvu zote.

Na hili litafanikiwa kama ilivyopangwa iwapo nguvu kubwa itaelekezwa kuwanyanyua wakulima kimaisha.

Kwamba ni kwa kutoa kipaumbele kwao kupitia programu na mipango mbalimbali ya maendeleo, ndipo lengo la kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025 litafanikiwa mapema zaidi.

Lakini tangu awamu ya tano iingie madarakani chini ya Rais John Magufuli, imeazimia kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, na wakulima ni wadau sahihi wa kutoa malighafi zinazohitajika kupeperusha uchumi huo.

Lingine la msingi analoliona Muungwana kwamba kupigania maslahi ya wakulima ni jambo la msingi, ni la nguvu yao linapokuja suala la kuchagua wawakilishi wa wananchi wenye fursa ya kuzungumza kwa niaba yao.

Hapa ninawazungumzia madiwani na wabunge ambao huchaguliwa kwa ajili ya kuwasilisha changamoto za wananchi katika majukwaa ya kutunga sheria kwa maana ya Mabaraza ya Madiwani na bungeni.

Kwa takribani wiki tatu sasa, Muungwana amekuwa akizungumzia changamoto inayowakumba wakulima wa zao la pamba nchini.

Nayo ni ya kutonunuliwa kwa pamba yao hadi sasa pamoja na msimu wa ununuzi kuzinduliwa mwezi Mei.

Ni jambo jema kwamba msimu huu zao hilo limezalishwa kwa wingi na wakulima wa mikoa takribani 10 inayolima pamba nchini, mingi ikiwa Kanda ya Ziwa.

Na tija katika uzalishaji wa zao hili imetokana pamoja na mambo mengine hamasa ya wadau na hasa serikali, ambayo imeliingiza zao hili kuwa moja ya mazao ya kimkakati.

Hadi sasa kampuni zilizosajiliwa na Bodi ya Pamba Nchini (TCB) kwa ajili ya kununua zao hili zinaendelea kusuasua.

Muungwana anasema kusuasua kwa sababu taarifa kutoka maeneo mbalimbali zinaonyesha kwamba ni kampuni chache ambazo zimeanza kununua katika baadhi ya maeneo.

Hata hivyo, ununuzi wao si wa fedha taslimu kwa pamba yote, kwani pamba iliyo nyingi inakopwa kwa maana kwamba fedha inayopelekwa katika maeneo machache yaliyoanza kununua zao hilo inakuwa kidogo.

Kwamba inakuwa kidogo wakati wakulima wanaopeleka pamba kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) ni wengi na hivyo baadhi wanajikuta wakikopwa.

Na hilo linafanyika pamoja na kuwapo maagizo kutoka kwa viongozi wa kiserikali ya kutokopwa kwa pamba ya wakulima.

Ndiyo maana Muungwana anasema bado changamoto hii ni kubwa, na kitendo hiki kinakwamisha maendeleo ya wakulima wa zao hili katika dhima nzima ya kujiletea maendeleo yao.

Ikumbukwe shule nyingi zimefunguliwa jana nchini kwa ajili ya muhula wa pili wa masomo, na kwa hali hiyo wakulima kama walivyo Watanzania wengine wanahitaji fedha pamoja na mengine kugharimia mahitaji ya shule ya watoto wao.

Ni bahati mbaya kwamba pamoja na umuhimu wa kundi hili kwenye suala la kupata wawakilishi wa wananchi kama madiwani na wabunge, bado ni wawakilishi wachache ambao wamejitokeza kupaza sauti dhidi ya changamoto hii inayowakumba wakulima wa pamba.

Changamoto ambayo ni kikwazo kwa Tanzania ya uchumi wa Kati ifikapo 2025 na kufikia Tanzania ya uchumi wa viwanda.

Ni rai ya Muungwana kwa wawakilishi wa wananchi kuwasemea wakulima hawa ili pamba yao yote inunuliwe, tena kwa fedha taslimu tofauti na ilivyo sasa ambapo kuna wakulima ambao pamba nayo inakopwa.

## BARUA/MJADALA

# Hii kero Mikese hadi lini?

***Ndugu Mhariri***

*SISI wananchi tunaoishi Kitongoji cha Ukomanga, Kijiji cha Fulwe, Kata ya Mikese, mkoani Morogoro tunaleta masikitiko yetu makubwa kwako ili wahusika wapate kulielewa hili tukitegemea kupatiwa ufumbuzi kabla ya hali ya sintofahamu haijatokea.*

*Masikitiko yetu makubwa/kero yetu kubwa ni juu ya uwepo wa baadhi ya makanisa katika kitongoji chetu na utaratibu wake wa uendeshwaji kwa kutofuata sheria, ambapo imefikia kuwa kero, mateso, adhabu na hata kukosa amani.*

*Baadhi ya kero hizo ni pamoja na upigaji kelele kwa kutumia spika kubwa ambazo hutoa muziki mkubwa usiku kucha na kila siku, mbaya zaidi, makanisa haya yapo katikati ya makazi ya watu.*

*Hali hiyo husababisha wagonjwa, watoto, wazee na wanafunzi kuteswa na kelele na hata kupelekea kutofanya vizuri kimasomo.*

*Aidha, miradi yao ya ufugaji wao wa nguruwe pasipo kufuata utaratibu, kwani hufuga katikati ya jamii na kuwaacha wakizurura ovyo, usafi mdogo na mabanda yanayopelekea kutoa harufu kali na isiyovumilika, hali ambayo inahatarisha afya zetu.*

*Sisi kama wanakitongoji tulishawahi kuwaita hawa wamiliki wa makanisa na kuwaeleza tena kiungwana tu juu ya haya tukitegemea kupata suluhu, na badala yake wakawa na majibu yasiyotarajiwa.*

*Wakatoa majibu kuwa wao wana kibali cha serikali na wataendelea bila mtu yeyote kuwasumbua. Ninauliza hivi kweli huu ndio utaratibu wa uendeshaji wa makanisa? Je, kwa majibu haya kuna amani hapa?*

*Haya malalamiko ya kero hizi tumezifikisha katika uongozi wa serikali ya kijiji, Ofisi ya Diwani, Kata ya Mikese lakini utekelezaji haupo.*

*Hivyo basi, kwa matumaini makubwa tuliyonayo kupitia gazeti lako pendwa, barua yetu wahusika wataiona na kulitatua hili kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.*

***Ahsante ni sisi wanakitongoji, Ukomanga-Fulwe, Mikese***

### WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Hatua hii ya wazazi Musoma Vijijini nuru sekta ya elimu

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI ilianzisha sekondari za kata ili kusaidia watoto wengi kuingia sekondari na pia wasitembee umbali mrefu kufuata masomo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kabla ya kuwapo kwa shule hizo.

Kimsingi watoto wanapotembea umbali mrefu hufika shuleni wakiwa wamechoka, kuhisi njaa na kukosa usikivu katika kufuatilia vipindi vya masomo, hali ambayo inaweza kusababisha wasifanye vizuri darasani.

Serikali imefanikiwa katika kuondoa kero hiyo kwenye baadhi ya maeneo, lakini kule ambako bado zipo, baadhi ya wazazi wamechukua hatua ya kupambana nazo ili kuhakikisha wanazimaliza.

Mfano mmojawapo wa wazazi, ambao wameshiriki kikamilifu katika ujenzi wa shule za sekondari za kata na sasa wameanza za vijiji ili kusogeza zaidi huduma ya elimu kwenye maeneo yao ni Wilaya ya Musoma Vijijini.

Wilaya hiyo ina kata 21 na imefanikiwa kuwa na sekondari 17 zinazofanya kazi ikiwa imebakiza kata nne za Bugoji, Busambara, Ifulifu na Nyegina, ambazo wananchi wanaendelea na ujenzi.

Kata zenye sekondari kwa sasa ni za Suguti, Nyambono, Bugwema, Nyamurandilila, Mugango, Nyakatende, Bukima, Rusoli, Bulinga, Murangi, Kiriba, Bwasi, Makojo, Bukumi, Etaro, Masanja na Tegeruka.

Ofisa Elimu wa Wilaya ya Musoma, Majid Kalugendo, anasema, wakati ukamilishaji wa sekondari kwenye kata nne ukiendelea, baadhi ya vijiji vimeanza ujenzi wa sekondari zao.

"Lengo la wazazi kufanya hivyo ni kutaka kusogeza karibu zaidi huduma ya elimu na kuwapunguzia watoto kutembea umbali mrefu kufuata elimu katika sekondari za kata," anasema Kalugendo.

Anavitaja vijiji hivyo kuwa ni Nyasaungu, Kata ya Ifulifu na Kigera Etima, Kata ya Nyakatende, ambapo Kalugendo anasema hatua hiyo ni ya kuungwa mkono, kwa vile wahusika wanatambua kuwa ni wadau muhimu wa elimu.

Kalugendo anasema vijiji hivyo vipo mbali na maeneo ambayo sekondari za kata zimejengwa, hivyo wazazi wanaona ni bora wajenge sekondari nyingine ili kuwapunguzia watoto kero ya kutembea umbali mrefu.

Hatua ya wazazi hao kujenga sekondari za vijiji ni wazi kwamba ni ya msingi pamoja na kuwa serikali ilianzisha sekondari za kata ili kusogeza huduma ya elimu lakini imeonekana bado wapo wanafunzi wanaotembea umbali mrefu.

Hivyo wazazi kwa kutambua kuwa wao ni wadau wakubwa wa maendeleo ya elimu, wameshiriki ujenzi wa sekondari za kata na sasa wanajenga za vijiji ikiwa ni juhudi za kuboresha elimu.

Kwa hiyo linapokuja suala la umuhimu wa mzazi kushiriki kwenye maendeleo ya elimu, maana yake linagusa mustakabali wa maisha ya mtoto wake, na ndiyo maana anatakiwa kuhakikisha anashiriki kikamilifu kwa hali na mali.

Ninajua wapo baadhi ya wazazi, ambao wamekuwa ni wagumu kushiriki katika maendeleo ya shule wakidai kwamba hiyo ni kazi ya serikali, wakidhani wao hawahusiki kwa lolote.

Lakini ukweli ni kwamba shule ni za wazazi, na pale zinapokumbwa na changamoto hawana budi kufanya juu chini ili kuzitatua badala ya kusubiri serikali wakati wapo.

Kimsingi mzazi kama kiungo muhimu cha maendeleo ya elimu kwa mtoto wake, ndio maana kwa kutambua hilo, wazazi wa vijiji nilivyotaja wameona kuna haja ya kupiga hatua zaidi na kuanza ujenzi wa sekondari za vijiji.

Mjadala unaunga mkono juhudi hizo za wazazi hao za kujenga sekondari za vijiji, kwani elimu ndio kila kitu katika maisha ndio maana kuna kaulimbiu mbalimbali zinazohamasisha jamii kuipenda.

Baadhi ya kaulimbiu hizo ni kama vile 'Elimu ni msingi wa maisha, elimu ni ufunguo wa maisha, elimu ni mali, elimu ni uhai' na nyingine nyingi ambazo zinalenga kuifanya jamii kupenda elimu.

Ninaamini kwamba wazazi wote wakitoa kipaumbele katika suala la elimu ikiwamo kuboresha miundombinu ya shule au kujenga shule mpya pale inahitajika, watakuwa wametimiza wajibu wao kikamilifu.

Ni vyema wadau wote wa elimu wakaunga mkono juhudi zinazofanywa na wazazi ambao wameamua kujenga shule za sekondari za vijiji kwa vile wanachofanya ni kuikomboa nchi, katika sekta ya elimu.

Kwa kauli ya Kalugendo ni kwamba wanafunzi kufanya vibaya darasani kunachangiwa na mambo mengi ikiwamo kutembea umbali mrefu, hivyo anapoona wazazi wanachukua hatua za kuboresha elimu anafarijika.

Kalugendo anaweka wazi kuwa wazazi ni wadau wakubwa wa maendeleo ya elimu, hivyo kile ambacho kinafanywa na wakazi wa vijiji vya Nyasaungu na Kigera na Etima kinaonyesha wanajua wajibu wao katika maendeleo ya elimu.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



## HABARI KITAIFA

# Mpango aanika wizi hatari benki

INATOKA UK 2

uwezekano wa kuzifikisha.

"Hebu mzitazame nchi zinazotuzunguka ili kuona NMB kama inaweza kujitanua huko. Kwa mfano (Jamhuri ya Kidemokrasia ya) Congo ni soko kubwa, shida yake kwa sasa ni hali ya usalama. Lakini siku bunduki zikinyamaza ni soko kubwa sana ambao tunafanya nao biashara," alisema.

Pamoja na msisitizo huo na mafanikio waliyoyapata kuna changamoto ambazo bodi na menejimenti inatakiwa kuzifanyia kazi ikiwamo suala la riba.

"Rais na mimi kwa nyakati tofauti huwa tunasema ni changamoto kwa wananchi wetu wa kipato cha chini wanashindwa kukopa ili kuwekeza kuboresha na kukuza biashara zao, sababu kubwa ni riba, riba za benki zetu bado zipo juu," alisema.

Dk. Mpango (pichani) alisema pamoja na hatua zinazochukuliwa Benki Kuu (BoT), benki zina wajibu mkubwa wa kufanya ili riba hizo kushuka.

"Menejimenti niwaombe mwangalie kwa jicho kali gharama zenu za uendeshaji. Lakini mwangalie sana kusimamia taratibu za ukopaji ndani ya benki, nikisikia mimi huwa si mpole, kuna benki hazifuati taratibu za ukopeshaji. Wanakopesha watu au taasisi ambao hawastahili kukopa," alisema.

Alitaka utumike mfumo uliowekwa na BoT na sasa utalazimishwa na sheria kuhakikisha kwamba wanatumia taarifa za benki ambazo zina historia ya wakopaji.

"Siyo unakopa ovyo ovyo tu, hapana. Mwenyekiti hujaniambia mikopo chechefu kiasi



gani, asilimia sita nataka zishuke, mikopo hii chechefu kwenye benki zetu bado ni kubwa," alisema.

**HUDUMA ZA KIBENKI**

Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na benki mbalimbali na sekta ya fedha kwa ujumla, Waziri Mpango alisema bado kuna wananchi wengi hawafikiwi na huduma za kibenki.

"Nilienda sehemu kwenye tawi langu hapa, nina kaakaunti kangu na siku hiyo nilitoka mtaani, tutumie huduma zinazotembea. Nilienda mnadani kijiji kinaitwa Kigwe, nilimkuta kijana anahesabu fedha mbele ya macho yangu Sh. milioni 30 akaweka kwenye mfuko wa rambo akaanza kunywa bia. Niliogopa kwa sababu hakukuwa na polisi pale," alisema.

"Sikuona tawi la benki karibu, watu wanahitaji kusogezewa huduma. Watu wanafanya biashara kubwa kwenye minada kwa ukanda huu wa kati kuna minanda mingi," aliongeza.

**SERIKALI NA NMB**

Katika hatua nyingine,

Waziri Mpango aliihakikishia benki hiyo kuwa serikali itaendelea kufanya kazi nayo na kuwataka maofisa wake wasio na akaunti ya NMB kwenda kufungua ili kuhifadhi fedha zao.

"Naibu Katibu Mkuu Nduguru una akaunti NMB? Leo (jana) mkafungue ili muwe wa mfano. Tunavyozidi kuwa wa mfano kutumia ndiyo wananchi wanaipenda. Sasa mtawaambiaje wananchi wafungue akaunti NMB wakati nyie hamna? Kwa hiyo muanze leo," alisema.

Awali, Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema serikali ni mmoja wa wanahisa wakubwa na kwamba kwa mwaka 2018 benki ilitengeneza faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 142 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia tatu kutoka Sh. bilioni 138 faida ya mwaka 2017.

"Faida baada ya kodi ilikuwa Sh. bilioni 98 ikiwa ni ongezeko la asilimia nne kutoka Sh. bilioni 93 faida ya mwaka 2017," alisema.

Alisema Sh. bilioni 33 zimetolewa gawio kwa mwaka 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia tatu kutoka Sh. bilioni 32 zilizolipwa mwaka 2017.

Alibainisha kuwa serikali ambayo inamiliki hisa kwa asilimia 31.8 imepata gawio la Sh. bilioni 10.48 ikiwa ni ongezeko la asilimia tatu kulinganisha na Sh. bilioni 10.17 za mwaka 2017.

# Msako wa msaidizi wa Membe waanza

INATOKA UK 3

ambako Allan alikuwa anaelekea kulikuwa na gari iliyokuwa ikipandisha kwa sababu kuna kibonde, ilikuwa inaelekea upande wa kulia alikokuwa Allan."

Magreth anaendelea kusimulia kuwa, baada ya gari hiyo kupita, ilikuja nyingine aina ya Land Cruiser ikitokea nyuma ya gari la Allan.

"Hiyo Land Cruiser ilikuwa na rangi kama ya khaki, brown au gold hivi, nikamwambia Allan kuwa kuna gari nyingine nyuma ili asogee mbele aipishe, Allan aliniambia mbona njia ni kubwa sana, nikamwambia asogee ili kuepusha ugomvi, akasogea, aliposogea kama anarudi geiti ile gari nayo ikasogea, nikamwambia asogee tena ili kuepusha ugomvi, aliposogeza gari alishuka na yule mtu kwenye Land Crusier naye akashuka," anasimulia.

Magreth alieleza kuwa, baada ya dereva wa Land Cruiser kushuka aliangalia mbele na nyuma na akawauliza kwani vipi.

"Allan naye alimuuliza kwani vipi, na mimi nilimuuliza mbona tumekupisha hujapita, wakati namalizia kujibu nilipomgeukia Allan, nikaona watu wamezunguka gari, wawili pembeni yetu, wawili nyuma yangu na wengine walikuwa kama saba na yule kaka wa kwanza. Wakamvamia Allan na kumpiga, Allan alikuwa anasema Mage nisaidie, yule kaka wa kwanza akaninyooshea bastola, nikasikia mmoja anasema mchukue na huyo (yaani mimi), huyu hakutii alichoambiwa na mwenzake, akaniambia nifanye haraka niingie ndani, nikanyata kurudi ndani sikufunga geti na komeo, nilipofika mlango wa kuingia ndani ya nyumba nikapiga kelele Allan ametekwa."

Magreth anadai walipotoka walikuta wameshaondoka ingawa kuna watu wa bodaboda walijitokeza na kueleza kuwa gari hilo lilipita mtaani hapo kama mara tatu.

"Tukio hili lilichukua kama dakika tatu hivi. Ila wakati tunatoka baa kuna bodaboda niliiona kama vile ilikuwa inatufuatilia, lakini sikuitilia maanani, hawajachukua kitu waliacha gari, fungu, simu yake smart phone, simu yake ndogo ambayo alikuwa nayo ambayo ni ya laini yake ya Tigo, hata polisi tumejaribu kuipiga haipatikani," Magreth alidai.

**"Hiyo Land Cruiser ilikuwa na rangi kama ya khaki, brown au gold hivi, nikamwambia Allan kuwa kuna gari nyingine nyuma ili asogee mbele aipishe, Allan aliniambia mbona njia ni kubwa sana, nikamwambia asogee ili kuepusha ugomvi, akasogea, aliposogea kama anarudi geiti ile gari nayo ikasogea, nikamwambia asogee tena ili kuepusha ugomvi, aliposogeza gari alishuka na yule mtu kwenye Land Crusier naye akashuka," anasimulia.**

# Ajali ilivyofupisha uhai watumishi

INATOKA UK 2

Wilaya ya Igunga, Merichad Magongo, alithibitisha kupokea majeruhi hao watatu huku wawili wakiwa na hali mbaya.

**JPM ATUMA RAMBIRAMBI**

Kutokana na ajali hiyo, Rais John Magufuli amemtumia salamu za rambirambi Mwenyekiti wa Kampuni za Azam, Said Salim Bakhresa.

Taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema Rais ameshtushwa na ajali hiyo iliyopoteza maisha ya watu saba wakiwamo wafanyakazi watano wa Azam Media na madereva wawili.

"Nimeshtushwa sana na vifo hivi. Nampa pole Mwenyekiti Said Salim Bakhresa, ndugu wa marehemu wote, Mtendaji Mkuu wa Azam, Tido Mhando, na wafanyakazi wote wa Azam Media Ltd, waandishi wa habari wote na watu wote walioguswa na vifo hivyo.

Rais Magufuli pia aliwaombea majeruhi wa ajali hiyo wapone haraka ili kuendelea na majukumu yao ya kila siku.

Aidha, Rais Magufuli alirejea wito wake wa kuwataka watumiaji wa barabara, husussani madereva, kuwa makini na kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zinazoweza kuzuilika.

**VIONGOZI WAWALILIA**

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alituma salama za rambirambi kutokana na msiba huo na kusema: "Natoa pole kwa familia, ndugu jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao. Mwenyezi Mungu awape nguvu na faraja katika kipindi hiki kigumu. Vile vile nawaombea majeruhi wengine wapone haraka."

INAENDELEA UK 26




# Kibaha yaanzisha kampeni ya elimu

**Na Yasmine Protace,** KIBAHA

HALMASHAURI ya Kibaha Mjini mkoani Pwani, imezindua kampeni ya Elimisha Kibaha.

Lengo la kampeni hiyo ni kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za serikali za sekondari.

Kampeni hiyo imeanzishwa kutokana na kuwapo upungufu wa vyumba vya madarasa 31 katika shule za sekondari Kibaha Mjini, na hali hiyo imesababisha wanafunzi kusoma kwa awamu mbili.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Asumpta Mshama, baada ya kukutana na mdau wa maendeleo, Jamal Mohammed, ambaye ameahidi kujenga vyumba viwili vya madarasa.

"Tumeona tuzindue kampeni hii ambayo tumeiita jina la changia elimu Kibaha na kibali tumeomba ili kuifanya kampeni hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa katika kampeni hiyo, wadau mbalimbali wa maendeleo wamejitokeza kuiunga mkono kampeni hiyo.

Alisema kutokana na kupata ahadi kwa wadau wa maendeleo na michango ya michanga na misumari, mpaka mwishoni mwa mwaka huu vyumba 31 vya madarasa vitakuwa vimekamilika.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa ujenzi huo, kutaokoa kiasi cha Sh. milioni 600 ambacho kingetolewa na halmashauri kutumika kwa ajili ya ujenzi huo.

"Halmashauri pekee isingeweza kujenga vyumba hivyo mpaka mwishoni mwa mwaka viwe vimekamilika," alisema na aliongeza kuwa anawashukuru wadau wote wa maendeleo waliojitolea kuwasaidia kujenga vyumba hivyo.

Mshama alisema zaidi kuwa katika kampeni hiyo walikubaliana katika mikutano na wananchi kuwa kila kaya itachangia shilingi 1,000 kwa ajili ya kuongeza nguvu katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ambapo shule 13 za sekondari zina uhaba wa madarasa 31.

# Wananchi wajitolea nguvu ujenzi hospitali ya wilaya

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WANANCHI wa Kata ya Mbuyuni Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wamesema kuwa wataendelea kuchangia nguvu zao kwa kushiriki kwa vitendo ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Masasi inayojengwa kwenye kata hiyo.

Wamesema watafanya hivyo, licha ya baadhi ya viongozi kutaka kukwamisha ujenzi huo kwa lengo la kujitangaza kisiasa. Kauli hiyo waliitoa jana katika gazeti hili wakiwa katika ujenzi wa hospitali hiyo ambao utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.5, ambazo zimetolewa na serikali kwa lengo la kuboresha huduma ya afya wilayani hapa.

Walisema licha ya baadhi ya viongozi lengo lao ni kutaka kuona serikali inakwama katika jitihada zake za kuleta maendeleo, hivyo wamekuwa wakiwaambia wananchi wasijitolee kushiriki ujenzi huo kwa madai kuwa hospitali hiyo haikuwa imepangwa kujengwa kwenye kata hiyo.

**Hawa baadhi ya viongozi ambao nia yao ni kuona hospitali hii inakwama ili wapate jukwaa la kujitangaza kisiasa, basi watafute mtaji mwingine wa kujitangaza kisiasa na sio kupitia hospitali hii...**

Uamuzi wa kujengwa eneo hilo ulipingwa na Baraza la Madiwani, baadhi wakidai eneo hilo sio rafiki kwa ujenzi kwa vile lina majimaji, hivyo inaweza kuathiri majengo yanayojengwa.

Bakari Selemali, mkazi wa kijiji cha Mbuyuni, aliipongeza serikali na hasa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, kwa kuingilia kati mvutano wa madiwani na watendaji wa Halmashauri,ambapo baadhi ya madiwani hawakufurahishwa na maamuzi ya serikali ya kujenga hospitali hiyo katika kata ya Mbuyuni.

Alisema wataendelea kushiriki kikamilifu katika ujenzi huo kwa vile serikali dhumuni lake ni kupeleka huduma ya afya kwa wananchi.

Naye Sophia Swalehe alisema itakapokamilika kutasaidia wanawake wengi ambao awali walikuwa wakitembea umbali mrefu kwenda hospitali ya mji wa Masasi Mkomaindo kufuata huduma za matibabu.

Fatuma Issa, mkazi wa Mbuyuni, alisema viongozi wanaotaka kukwamisha ujenzi huo hawana nafasi kwa vile nia yao ni kutaka kurudisha nyuma maendeleo.

"Hawa baadhi ya viongozi ambao nia yao ni kuona hospitali hii inakwama ili wapate jukwaa la kujitangaza kisiasa, basi watafute mtaji mwingine wa kujitangaza kisiasa na sio kupitia hospitali hii... sisi tutashiriki katika kila hatua ya ujenzi hadi pale itakapokamilika na tunaipongeza serikali kwa hili," alisema Issa.

Mkuu wa wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, alisema ujenzi unaendelea vizuri na tangu kuanza wananchi wameonyesha ari katika kushiriki kwa vitendo.

Alisema tayari baadhi ya majengo yameshapauliwa na kwamba amekuwa akifuatilia mara kwa mara ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati.

Alisema suala la mvutano juu ya wapi hospitali hiyo ijengwe serikali ilishaamua na kuagiza ujenzi kufanyika katika kata ya Mbuyuni.




Mkazi wa la Dar es Salaam akiwa amejitwisha mzigo wa chupa tupu za plastiki, akizipeleka kuziuza ili ajipatie riziki, kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Bil. 2.8/- kuletea maji wananchi vijiji vitano

**Na Sabato Kasika**

VIJIJI vitano vya Bujaga, Bulinga, Busungu, Bukima na Kwikerege wilayani Musoma Vijijini mkoani Mara, vinatarajia kunufaika na mradi wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria, utakaogharimu Sh. bilioni 2.83.

Maji yatatolewa Ziwa Victoria na kujazwa katika tangi lenye uwezo wa kuchukua lita 225,000 lililopo kijiji cha Bujaga na kisha yatasambazwa kwenye vijiji hivyo.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, aliliambia gazeti hili jana kuwa usambazaji wa maji kwenye vijiji hivyo umegawanywa katika makundi mawili ili kuharakisha utekelezaji wake.

"Katika kundi la kwanza ni kwamba maji yatachukuliwa na kutoka tangi lililopo kijijini Bujaga na kusambazwa kwenye kijiji cha Bulinga na Bujaga yenyewe," alisema Dk. Anney.

Dk. Anney alifafanua kuwa mradi huo unatekelezwa na mkandarasi Medes Company Ltd na gharama yake ni Sh. bilioni 1.81, na kwamba mradi huo ulizinduliwa na mbio za Mwenge wa Uhuru, Mei 31 mwaka huu.

"Kundi la pili ni mradi wa vijiji vya Busungu, Bukima hadi Kwikerege, maji yatachukuliwa kutoka tangi la Bujaga na kusambazwa kwenye vijiji hivyo, utekelezaji wa mradi unaendelea kwa kasi ya kuridhisha," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema, mradi wa Busungu, Bukima hadi Kwikerege unagharimu Sh. bilioni 1.02, na kwamba unatekelezwa na mkandarasi Edm Network, Ltd & JV Fau Construction Ltd.

"Mradi huu unakwenda sambamba na ujenzi wa tangi lenye uwezo wa kuchukua lita 225,000, ofisi ya mradi, vituo 18 vya kuchotea maji, vioski viwili vya kuuzia maji, birika za kunyweshea mifugo na utandazaji wa mabomba ya kusambazia maji," alisema.

Alisema, ujenzi wa vituo hivyo vya maji, ofisi, vioski na birika la kunyweshea mifugo, ambao ulianza mwaka jana, unatekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja na kufikia Septemba mwaka huu utakuwa umekamilika.

"Serikali imedhamiria kuhakikisha vijiji vyote 68 vya Musoma Vijijini vinaondokana na kero ya ukosefu wa maji, hivyo wananchi waendelee kuiunga mkono serikali inapotekeleza miradi kama hii," alisema.

Alifafanua kuwa kwa sasa taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya mradi wa vijiji vya Bugunda, Bwasi, Chimati na Kome zimeanza ili navyo viweze kupata maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria.

Naye Mtendaji wa kijiji cha Busungu, Charles Ndagile, alisema wakazi wa kijiji hicho wamekubali kutoa maeneo yao ili kupitisha mabomba ya maji bila kuhitaji fidia.

Kwa niaba ya wananchi wa Musoma Vijijini, Mbunge wao Profesa Sospeter Muhongo ameishukuru serikali kwa kuanzisha na kutekeleza mradi ya usambazaji maji kwenye vijiji vya jimbo hilo.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaondoa kero ya ukosefu wa maji na kwamba wananchi watakuwa wanapata majisafi na salama na pia kinamama hawatatembea tena umbali mrefu kwenda kuchota maji.

SABASABA

# TET yapiga jeki vitabu shule za Kinondoni

TAASISI ya Elimu Tanzania (TET), katika kuadhimisha Siku maalum ya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba (DITF), imetoa zawadi ya vitabu vya kiada na ziada kwa wanafunzi wa shule nne za Wilaya ya Kinondoni waolifanya vizuri katika shindano la kujibu maswali ya ufahamu kuhusu maktaba ya mtandaoni.

**Shule nne za Kinondoni zilionyesha ufahamu mkubwa katika kujibu maswali hayo...**

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam katika maonyesho hayo, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Utafiti, Habari na Machapisho kutoka TEC, Kwangu Zabron, alisema, maswali yalihojiwa ili kupima uelewa wa wanafunzi juu ya matumizi ya mfumo huo. Alisema katika shindano hilo lililohusisha shule zote za Halmashauri ya Kinondoni ni nne tu ndizo zilizoibuka kidedea.

"Shule nne za Kinondoni zilionyesha ufahamu mkubwa katika kujibu maswali hayo ambapo tumeona ni vyema kuwapa zawadi kwa wanafunzi na shule pia," alisema Zabron.

Alisema mfumo huo unatumika katika mikoa mbalimbali nchini ambapo hadi sasa tisa imeanza kusajili.

Alitaja mikoa iliyosajiliwa ni pamoja Sar es Salaam, Pwani, Simiyu, Dodoma, Geita, Ruvuma, Lindi, Unguja Mashariki, Kagera na Rukwa.

Alisema lengo la mfumo huo ni kurahisishia kupatikana kwa vitabu vya kiada na ziada pale vinapochelewa kufika katika shule husika.

Aliongeza kuwa usajili huo unaendelea na kwamba hata shule binafsi zinatakiwa kujiunga na mfumo huo..



Wananchi wakijaza fomu za kuomba vyeti vya kuzaliwa kwa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kampuni 150 zajisajili Brela kidigitali

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), umesema kampuni 150 zimejisajili kwa njia ya kimtandao na kuwasilisha majina ya biashara zao katika kipindi hiki cha Maonyesho ya 43 ya Biashara (Sabasaba).

Akizungumza Dar es Salaam jana, katika maonyesho hayo, Ofisa Habari wa Brela, Robetha Makinda, alisema watu wamejitokeza kwa mwingi katika banda lao na kusajili kampuni na biashara zao ili ziweze kutambulika.

"Mwitikio wa wananchi umekuwa mkubwa katika maonyesho haya tofauti na kipindi cha nyuma, watu wamekuja kwa wingi kututembelea katika banda letu na kupata elimu ya kina ya namna ya kuandikisha kampuni, alisema Makinda.

Makinda alisema kuanzia Januari 2018 hadi 2019 kampuni 8150 zimejisajili kwa njia ya mtandao kwa wakala huo.

Alisema kampuni zilizohuisha kuanzia kipindi cha Januari 2018 hadi Juni 2019 ni 4,565, huku majina ya biashara yaliyosajiliwa kipindi hicho ni 16,683.

"Kupitia maonyesho haya tumekuwa tukitoa elimu kwa wananchi wanaokuja kutembelea banda letu tunawapatia elimu sahihi ya masuala ya kujiandikisha kwa njia ya kimtandao," alisema Makinda.

Alisema usajili wa kampuni kwa njia ya mtandao ulianza mwaka 2018 na wamekuwa wakisajili kampuni, majina ya biashara, huduma zake pamoja na leseni za kibiashara.

Kwa upande wake Ofisa wa Brela, Nimzanael Mchome, alisema miongoni mwa changamoto wanazokumbana nazo ni uelewa mdogo wa matumizi ya Tehama na sheria katika baadhi ya watu wanaojisajili.

# Mwisho magogo kukatia nyama ni Septemba 15

BODI ya Nyama Tanzania, imesema mwisho wa kutumia magogo ya kukatia nyama ni Septemba 30, mwaka huu, na kwamba atakayekaidi atachukuliwa hatua za kisheria.

Ofisa Usajili kutoka katika bodi hiyo, Geofrey Sosthens, akizungumza katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Kibiashara yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, aliwataka wafanyabiashara wa bidhaa hiyo kutii agizo hilo.

Alisema watakao kaidi agizo hilo watachukuliwa hatua na msajili wa bodi hiyo, kwa sababu tayari amekwisha ziandikia mamlaka za Serikali za Mitaa tangu Februari, kuhakikisha wanaboresha maeneo yote yanayozalisha nyama ikiwa ni pamoja na machinjio, makalo na mabucha.

Alisema wamepiga marufuku matumizi ya magogo hayo kwa sababu yanamdhara kwa sababu hayasafishiki.

"Tutahakikisha tunawashauri wamiliki wa mabucha kuhakikisha yanakuwa ya viwango ikiwa ni pamoja na kuacha kutumia magogo," alisema. Ofisa huyo pia alitoa ombi kwa wadau wote wanaojishughulisha na mnyororo wa nyama kuhakikisha anajaliwa na kumiliki cheti kutoka katika bodi hiyo.

# Nishati jadidifu yaleta fursa ya ajira

SERIKALI imesema ugunduzi na ubunifu katika nishati jadidifu ihusishayo nishati endelevu, ni miongoni mwa fursa inayoleta ajira, kuongeza uzalishaji, ubunifu na kupunguza umaskini nchini.

Pia, imesema jamii inapaswa kubadili mtazamo na kufungua upeo kuyaona masuala ya nishati jadidifu kwa jicho chanya kwa kuwa yanatoa fursa mbalimbali za kibiashara na uzalishaji.

Akizungumza Dar es Salaam jana wakati wa Jukwaa la Mabadiliko ya Tabianchi katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam yaliyoandaliwa na Shirika la FORUMCC, Kaimu Mkurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Amos Maganga, alisema serikali inatambua changamoto zitokanazo na uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi katika kufikia maendeleo ya uchumi wa kati, hivyo utumiaji wa nishati jadidifu utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza athari hizo za mabadiliko ya tabia nchi.

"Changamoto hizo zimeathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo ambayo ndio inachangia kwa kiasi kikubwa malighafi za viwanda, uhaba wa maji ambayo hutumika viwandani na uzalishaji wa nishati na uharibifu wa miundombinu ambayo hutumika kukutanisha malighafi, viwanda na masoko, tunaamini utumiaji wa nishati jadidifu utasaidia kuondokana na janga hili la mabadiliko ya tabianchi," alisema.



Habari na Elizabeth Zaya

Alisema Tanzania inahitaji mpango wenye taarifa sahihi za sekta ya nishati jadidifu ili kuainisha njia za maendeleo za baadaye na kuhakikisha watunga sera na wafanya maamuzi wanapata taarifa sahihi kuhusu nishati hiyo.

"REA kuna programu ambazo zinaendelea na tumekuwa tunawasaidia wabunifu mbalimbali kutoka vyuoni au wale wabunifu binafsi kwani tuna fedha kupitia kwa wahisani dola milioni 19 sawa na zaidi ya Sh. bilioni 40 ambazo zipo kwa ajili ya wabunifu na wanaoweka miradi ya nishati bora vijijini," alisema Maganga.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Forum CC, Rebecca Muna, alisema ili tuwe na Tanzania ya viwanda lazima tuwe na nishati ya uhakika hivyo tuangalie tuna fursa ili kujenga viwanda ambavyo havitaharibu mazingira.

Muna alitoa wito kwa wabunifu kuona fursa iliyopo katika nishati jadidifu na pia kutoa wito kwa serikali kuanza kutengeneza mazingira mazuri pamoja na kulea na kukuza vipaji vya wabunifu katika sekta hiyo ya nishati jadidifu.

# Watanzania wafundwa kulinda amani

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WATANZANIA watakiwa kutambua kuwa kazi ya kulinda uhuru wa nchi ya Tanzania na amani, ni wa kila mwananchi na sio jukumu la serikali peke yake.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, wakati akifungua na kuweka jiwe la msingi katika sherehe za uzinduzi wa boma la "Eunoto" Ooltwati zilizofanyika Kijiji cha Mti Mmoja kilichopo ndani ya Kata ya Sepeko wilayani Monduli mkoani hapa.

Dk. Bashiru aliwapongeza vijana wa jamii ya kifugaji ambao wameingia katika hatua ya makuzi na kupewa heshima ya kupewa rika na kuitwa Nyangulo.

Alisema uhuru na amani ambao upo, umetokana na mapambano ya wenyeji dhidi ya wageni ambao walitawala kwa muda mrefu na kupata ushindi mkubwa na ndio maana nchi ina uhuru na amani na kuheshimika duniani kote.

"Ndungu zangu nchi yetu ilitawaliwa na wageni na tabia ya mtawala wa kigeni hutumia mkakati wa kuwagawa nao watawala ili wasiweze kumpinga na kumwondoa katika nafasi aliopo, mkakati mkubwa wa mtawala wa kigeni ni kuwagawa watu wenyeji, hivyo tuwe makini na tusikubali kutawaliwa tena na wageni na uhuru wetu na pia tuendelee kulinda amani yetu kuendelea kuenza nidhamu na utulivu, " alisema.

Dk. Bashiru alisema mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga imepakana na Kenya na inategemeana katika shughuli mbalimbali za kibiashara, kijamii na hata za kiutamaduni.

"Mikoa hii pamoja na nchi jirani ya Kenya haina mipaka, kwani inategemeana katika shughuli hizi mbalimbali hivyo tuendelee kudumisha umoja huu wa nchi zetu, pamoja na jumuiya yetu na lengo la sisi Waafrika ni kufanya nchi zetu za Afrika kuwa moja," alisema na kuongeza:

"Naomba niwaambie nyie vijana wa rika la Eunoto (Nyangulo ) mwendelee kudumisha umoja huu na mwendelee na ujumbe kuwa kazi ya kudumisha umoja wetu haijakamilika na itakamilika pale Afrika itakapokuwa moja na mahali pa kuanzia ni kudumisha umoja wa Afrika Mashariki."

# TBS yateketeza bidhaa zilizopigwa marufuku

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeteketeza bidhaa zilizopigwa marufuku zikiwamo nguo za ndani za mitumba na vilainishi vya magari visivyo na ubora vilivyokamatwa katika masoko mbalimbali mkoani hapa.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa uteketezaji wa bidhaa hizo, Fundi Sanifu kutoka shirika hilo Kanda ya Kaskazini, Godfrey Nguka, alisema wamefikia hatua ya kufanya ukaguzi huo ili kupunguza madhara kwa watumiaji wa nguo za ndani za mitumba.

Alisema wameteketeza jumla ya tani mbili za nguo za ndani na vilainishi na uteketezaji huo ulifanyika katika dampo kuu la Mkoa wa Arusha lililoko Kata ya Muriet.

Nguka alisema, wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi mbalimbali mkoani Arusha juu ya madhara ya nguo hizo ikiwamo kusababisha magonjwa sugu kwa watumiaji, hivyo zoezi la uteketezaji linalenga kulinda afya za wananchi.

**Tumekuwa tukipita katika masoko na kutoa elimu kwa wananchi na wafanyabiashara hawa kuwa nguo hizi zina madhara makubwa sana, lakini bado wanaendelea kuuza sisi tutaendelea na msako.**

"Tumekuwa tukipita katika masoko na kutoa elimu kwa wananchi na wafanyabiashara hawa kuwa nguo hizi zina madhara makubwa sana, lakini bado wanaendelea kuuza sisi tutaendelea na msako wa kushtukiza mara kwa mara kwa lengo la kulinda afya za wananchi wetu," alisema Nguka.

Ofisa Mdhibiti wa TBS, Stanford Matei, alisema zoezi hilo limefanyika kwa mujibu wa sheria ili kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinaondolewa kwenye masoko kwa lengo la kuokoa afya za wananchi ambao ndio wateja wakubwa.

Aliongeza kitendo hicho cha uteketezaji wa bidhaa hizo ni mojawapo ya juhudi za kudhibiti uingizwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango zinazoingizwa kwa njia za panya.

Matei aliwataka wananchi kuhakikisha wanafanya biashara halali na kuepuka biashara zilizopigwa marufuku na serikali kwani ni hatari kwa afya za wananchi.

Wakizungumza kwa niaba ya wananchi walioshuhudia tukio hilo, Amir Hemed na Mwanaisha Juma wote ni wakazi wa Kata ya Muriet, walisema operesheni hiyo ya kuteketeza bidhaa hizo, inapaswa kuwa endelevu ili kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinaondolewa sokoni ili kunusuru maisha ya wananchi.

Walisema, licha ya mamlaka hiyo, kupiga marufuku matumizi ya nguo hizo, bado kuna changamoto kubwa katika utekelezaji kwa baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiendelea kufanya biashara hiyo kwa siri.

Hata hivyo, waliomba shirika hilo kuendelea kufanya operesheni hiyo mara kwa mara katika masoko mbalimbali ili kukomesha kabisa biashara hiyo.



Wachimbaji wa madini ya green katika machimbo ya Lemshuku, Kata ya Komolo, wakimsikiliza Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima (hayupo pichani), alipozungumza nao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waziri aiagiza KADCO kufuta hati ya Oryx

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, (KADCO), kuanza utaratibu wa kufanya mazungumzo na kampuni ya mafuta na gesi ya Oryx na kufuta hati miliki ya eneo ndani ya uwanja wa ndege.

Akizungumza katika ziara ya kikazi ya kutembelea mipaka ya uwanja wa ndege wa KIA, Nditiye, alisema ameshangazwa na kitendo cha Oryx kuwa na hati miliki ndani ya eneo la uwanja huo.

Alisema baada ya kubaini kasoro hiyo, ameiagiza KADCO, kuanza utaratibu wa kufanya mazungumzo na kampuni hiyo, ili kufuta hati miliki ya eneo la kituo cha mafuta na wabaki kama wapangaji kama watu wengine na siyo wamiliki wa eneo.

Nditiye alisema kampuni hiyo ya gesi na mafuta wanamiliki eneo ndani ya uwanja wa ndege lenye ukubwa wa mita za ujazo 1998.

"Siyo kitu cha kawaida mtu kuwa na hati juu ya hati naona kama kuna ujanja ulifanyika mwanzo na nimewaelekeza mamlaka husika kufanya utaratibu wa mazungumzo kwa ajili ya kufuta hati ya umiliki wa eneo la kampuni hii," alisema Nditiye.

Alisema kuwa uwanja huo upo kwa mujibu wa tangazo la Rais wa kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Nyerere la mwaka 1969.

Hata hivyo, alisema uwanja huo mwaka 1971, ulitangazwa kuwa uwanja mkubwa wenye urefu wa mita 800, na baada ya ujenzi kukamilika ndege zilianza kutua.

Alisema mwaka 1975, mmiliki wa Oryx alitumia mbinu za kijanja kupata hati miliki ya eneo ndani ya uwanja wa ndege akitambua kuwa eneo hilo, lilishatangazwa na serikali kuwa ni mali ya uwanja.

Akizungumzia kiwanja hicho kuchelewa kupata hati miliki ya eneo hilo, Nditiye alisema mwaka 1965, uongozi wa uwanja kipindi hicho walianza utaratibu wa kuomba hati miliki na mwaka 2005 walipatiwa.

Alisema ni utaratibu wa kawaida kwa taasisi za serikali kuchelewa kupatiwa hati miliki kwa kufuata utaratibu maalumu wa kisheria, ukilinganisha na watu binafsi ndio maana mmiliki wa kampuni hiyo aliwahi kupewa kabla ya uwanja wa ndege.

"Awali kampuni ya Oryx walikuwa na hati miliki ya eneo hili kwa muda wa miaka 33, lakini mwaka 2005, waliongezewa tena muda wa miaka mingine 33, nakufikisha miaka 66, ya umiliki wa eneo hili ndani ya uwanja.

"Hawa watu wa Oryx tunawapenda sana na tunawahitaji, lakini sisi kama serikali tunataka wawe wapangaji na siyo wamiliki," alisema Nditiye.

Aidha, alisema changamoto inayozikabili viwanja vya ndege hapa nchini, ni wananchi kuingilia na kuvamia maeneo hayo kutokana na kuwa na uwelewa mdogo.

# Uhifadhi waongeza utalii misitu

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

KUIMARISHWA kwa uhifadhi wa misitu ya asili kunakofanywa kwa ushirikiano na Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF), kumechagiza ongezeko la utalii wa misitu nchini.

Ofisa Mhifadhi Mwandamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Msitu wa Asili wa Chome, ulioko wilayani Same, Sosthenes Rwamugira, amesema idadi ya watalii waliotembelea msitu huo imeongezeka hadi 426 kwa mwaka huu kutoka watalii sita, mwaka 2002.

Rwamugira alikuwa akizungumza jana na wadau wa uhifadhi wa maliasili kuhusu mafanikio hayo.

Alisema ongezeko hilo linatokana na mchango mkubwa wa fedha unaotolewa na EAMCEF kwa ajili ya kufanya doria, kukarabati njia za kupita watalii ndani ya msitu, kutangaza msitu huo katika mitandao mbalimbali na kuwajengea uwezo wanavijiji waishio jirani na msitu na kuanzisha miradi ya kuwaingizia kipato.

**Tangu kuanzishwa kwa miradi hiyo na wananchi kujipatia kipato kutokana nayo, wananchi wameacha kuingia ndani ya msitu na kuleta uharibifu wa mazingira.**

Alisema Msitu wa Chome umezungukwa na vijiji 27 na kazi kubwa inayofanywa na mfuko ni kuwajengea uwezo wanavijiji ili kuingia ndani ya msitu na kufanya uharibifu wa mazingira.

Msitu wa Chome wenye hekta 14,283 unatambulika kitaifa na kimataifa kutokana na utajiri mkubwa ulio nao katika bionuai na chanzo kikubwa cha maji katika maeneo ya Same na kwingineko.

Mratibu wa EAMCEF mwenye makazi yake wilayani Muheza, Magreth Victor, alisema wamekuwa wakitoa Sh. milioni 28 kila mwaka kwa ajili ya uhifadhi wa msitu huo.

Rwamugira alikiri kuwa fedha hizo zimekuwa msaada mkubwa wa kuhifadhi msitu huo.

Kwa upande wa Msitu wa Hifadhi wa Asili wa Magamba, Mhifadhi Mkuu wa Msitu huo, Getrude Nganyagwa, alikiri kuanza kuongezeka kwa idadi ya watalii katika hifadhi hiyo.

Alisema kwa sasa wanaweza kupokea watalii sita kwa mwaka ambao wanatoka mataifa mbalimbali lakini hasa Ujerumani.

Nganyagwa alisema kutokana na kuimarika kwa njia ya kuingia ndani ya msitu huo zinazokarabatiwa na EAMCEF na watalii wameanza kupenda kutembea kwa miguu kutoka Lushoto mjini hadi ndani ya msitu huo.

Alisema ndani ya msitu huo kuna vivutio vingine kama vile maeneo ya mapumziko na uwepo wa pango la kihistoria la Wajerumani linalosaidikiwa lilikuwa likitumika kama sehemu ya ulinzi wakati wa Vita vya Kwanza ya Dunia mwaka 1914-1918 au walikuwa wakichimba madini bati (bauxite).

Mhifadhi Victor alisema mafanikio ya kuhifadhi msitu huo yamechangiwa pia na EAMCEF ambayo imekuwa ikitoa misaada ya kifedha ya Sh. milioni 26 kuanzia mwaka 2012 hadi sasa.

Akizungumzia uwezeshaji wa jamii, Mratibu Nganyagwa alisema wamekuwa wakishirikiana na wanavijiji hao kuanzisha miradi ya upandaji miti, bustani za mboga, viungo na ufugaji wa kuku na utengenezaji wa majiko banifu.

Pia alisema wanachangia kuimarisha doria, miundombinu ya njia na kuwajengea uwezo wanavijiji wa jirani kuanzisha miradi ya kujipatia kipato.

Alisema tangu kuanzishwa kwa miradi hiyo na wananchi kujipatia kipato kutokana nayo, wananchi wameacha kuingia ndani ya msitu na kuleta uharibifu wa mazingira.

Wizara ya Maliasili na Utalii, ilishatamka mwaka 2017 kuwa itaimarisha utalii wa misitu ya asili nchini iweze kutoa mchango mkubwa kwenye pato la taifa tofauti na hali ilivyo sasa ambapo utalii hutegemea zaidi wanyamapori.



Waendesha guta wakiwa wamejipumzisha kwenye vyombo vyao, wakisubiri wateja nje ya Soko la Boma Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# CCM yakiri tena uonevu wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amesema kuna unyanyasaji mkubwa wa wakulima unaoendelea katika eneo la West Kilimanjaro na maeneo mengine nchini.

Kutokana na hali hiyo, amesema CCM haiwezi kukubali wafanyabiashara wachache wakaharibu taswira ya serikali katika kushughulikia kero za wanyonge na maskini nchini.

Dk. Bashiru alifichua uonevu huo jana, alipokuwa akizungumza na viongozi wa CCM, jumuiya zake na matawi yaliyoko katika Wilaya ya Siha.

"Yako maeneo ambayo yamekuwa sugu na tuhahitaji kujipanga, eneo la kwanza ardhi, sheria zetu zinasema ardhi ni mali ya umma, sisi tuna haki ya kupangiwa namna ya kutumia na ardhi hiyo ikatunzika, ikatumika na ardhi siyo pesa na watakapojitokeza watu wenye uchu wa madaraka watatusumbua.

"Kwenye eneo la kilimo kuna unyanyasaji mkubwa hasa katika masoko ya mazao, lumbesa bado ni tatizo, hatuwezi kuvumilia unyanyasanyaji huo ukaendelea, kwa sababu matukio hayo yanapingana na dhamira ya Rais John Magufuli katika kusimamia uendelezaji wa mazao ya kimkakati," alisema.

Akiwa Siha, Katibu Mkuu huyo aliagiza viongozi wote ngazi ya wilaya kuacha kukaa ofisini na kwenda vijijini kutatua migogoro ya ardhi inayoonekana kuwa tatizo kubwa.

"Wekeni utaratibu wa kuitisha mikutano na kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua, na si kila kero imsubiri Rais wetu (Magufuli)," alisema Dk. Bashiru.

Kauli ya Dk. Bashiru inatokana na malalamiko ya wananchi wa Kijiji cha Ngarenairobi, ambao wamekuwa wakiwalalamikia baadhi ya viongozi wa maeneo hayo kuruhusu ujazo huo na kushindwa kuchukua hatua.

# Kilimanjaro kutengeneza matela ya trekta

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KIWANDA cha kutengeneza vipuri cha Kilimanjaro Machine Tools Manufacturing Ltd (KMTC) kilichoko chini ya Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), kimetangaza kuanza utekelezaji wa mradi mpya wa uzalishaji wa matela ya matrekta kwa ajili ya kuchochea uwekezaji katika sekta ya viwanda.

Taarifa ya menejimenti ya kiwanda hicho iliyoandikwa kwenda kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, inaeleza kuwa katika kuelekea kwenye uchumi wa kati, kiwanda hicho kitaanza kuzalisha matela hayo wakati wowote kuanzia sasa.

Meneja Mkuu wa KMTC, Andriano Nyaluke, alisema tayari serikali imeshatoa baraka zote kutekelezwa kwa mradi huo mkubwa.

Alipoulizwa Waziri Bashungwa kueleza kuhusu mradi huo alisema: "Ni kweli na nitoe wito kwa wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na mikoa mingine nchini hususani wakulima kujitokeza kununua matrekta kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo.

"Kama unavyojua wakulima wanayo nafasi kubwa kuipeleka nchi katika ujenzi wa viwanda, kwa sababu idadi kubwa ya Watanzania ni wakulima na malighafi nyingi za viwanda zinatokana na kilimo. Nimeshazindua tela la treka na michoro yake ambayo itazalishwa na kiwanda hicho."

Wakati KMTC ikijipanga kuanza kazi hiyo, NDC kupitia mradi wake wa kuunganisha matrekta kutoka Poland, nao umeanza kuuza matreka kwa bei nafuu kwa lengo la kuwainua wakulima na kukuza uzalishaji wa mazao.

Matrekta hayo yako ya uwezo tofauti, kuanzia ya Horse Power 50 hadi 85, 2WD na 4WD ambayo serikali imetangaza kuuzwa kwa bei ndogo kwa Sh. milioni 38.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 9, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## JE, WAJUA?

Ukurasa 15



## Mzazi mtie moyo mwanao anapofanya vibaya masomoni



Ukurasa 18

## Matumizi yaliyokithiri ya simu chanzo wanafunzi kuwa na wapenzi wengi?




# IMANI HIZI KUHUSU DHAMANA ZIPUUZWE

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI

## HATI YA TABIA NJEMA INAYOTOLEWA NA JESHI LA POLISI (POLICE CLEARANCE CERTIFICATE)

NI cheti/hati ya uthibitisho ambayo hutolewa na Jeshi la Polisi, ikithibitisha kuwa mtu aliyepewa hati hiyo hajawahi kutiwa hatiani na Mahakama kwa makosa ya jinai.

**MATUMIZI YA HATI YA TABIA NJEMA**

Hati ya tabia njema hutumika kwa shughuli mbalimbali za uthibitisho kama ifuatavyo:-

Kuomba Visa katika balozi mbalimbali za nchi za nje zilizopo hapa nchini kwa ajili ya mtu kusafiri kwenda katika nchi hizo kikazi, kimasomo, kibiashara au vinginevyo.

Kuomba ajira ndani ya nchi au nje ya nchi, kusajili kampuni na kumiliki bunduki.

Vilevile kuomba uraia wa Tanzania, pia taasisi au mwajiri kumchunguza mtumishi wake.

Pia kuomba kibali cha ukaazi katika nchi ya kigeni (Residence permit) pamoja na kuomba kibali cha kufanya kazi nchi ya kigeni (work permit).

Aidha, kuomba kibali cha kusoma nchi ya kigeni (study permit).

**KIGEZO MUHIMU CHA MTU KUPEWA HATI YA TABIA NJEMA**

Ili mtu aweze kupewa hati ya tabia njema inampasa kufika Forensic Bureau Makao Makuu Dar es Salaam, kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole ambazo zitachunguzwa kitaalamu ili kutambua kama alishawahi kutiwa hatiani au hapana.

Pia mbali na makao makuu, kwa watu walioko mikoani wanaweza kufika katika ofisi za wakuu wa Upelelezi wa Mikoa au Ofisi za Polisi za Wilaya waliko kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole.

Alama hizi zitatumwa Forensic Bureau Makao Makuu kwa ajili ya uchunguzi na utolewaji wa hati ya tabia njema ambayo itatumwa kwa mhusika aliyeomba hati hiyo.

**UMUHIMU WA HATI YA TABIA NJEMA**

Katika dunia ya leo yenye shughuli nyingi na mwingiliano mpana na uliowazi kwa kiasi kikubwa kati ya watu wa mataifa mbalimbali, hakuna nchi ambayo ingependa kupokea mtu ambaye haeleweki au mtu mwenye historia mbaya ya uhalifu.

Halikadhalika, hakuna kampuni au taasisi yeyote ambayo ingependa kumwajiri au kumpa jukumu lolote mtu ambaye ana historia chafu ya kiuhalifu.

Nchi na kampuni au taasisi mbalimbali zinahitaji watu wenye tabia na mwenendo mwema katika maisha ambao hawawezi kuwa chanzo cha matatizo katika nchi au taasisi zao.



Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) Robert Boaz. **PICHA: MTANDAO**

Hivyo, ni jukumu la kila mtu kujitunza na kutojihusisha na uhalifu wa aina yoyote ili asije akakosa huduma hii muhimu kwa sasa ambayo ukiikosa ni dhahiri unaweza kushindwa kufikia malengo hayo.

Yaweza kuwa ni ya malengo ya kielimu, ajira, biashara, safari za kikazi, kibiashara, kiutalii, kusajili kampuni.

**MAMLAKA YA KUTOA HATI YA TABIA NJEMA**

Hati ya tabia njema hutolewa na Jeshi la Polisi kupitia kurugenzi ya Forensic Bureau ambayo ni taasisi ya uchunguzi wa kisayansi ndani ya Jeshi la Polisi.

Mojawapo ya huduma muhimu zinazotolewa na taasisi hii ni hati ya tabia njema (Police Clearance Certificate) ambayo kwa kiasi kikubwa ni kwa matumizi ya kiraia.

**VIAMBATANISHO MUHIMU KATIKA MAOMBI YA HATI YA TABIA NJEMA**

Pamoja na alama za vidole, viambatanisho muhimu katika maombi ya hati ya tabia njema baadhi vinatofautiana kulingana na sababu ambayo mtu au taasisi inaombea hati ya tabia njema kama ifuatavyo:-

**VISA YA MASOMO NJE YA NCHI**

Panahitajika nakala ya hati ya kusafiria, vilevile nakala ya barua ya kukubaliwa chuo (ADMISION LETTER).

Aidha, picha 'passport size' moja na barua ya maombi.

VISA YA MAKAZI/KUFANYA KAZI NJE.

Panahitajika nakala ya hati ya kusafiria na picha 'passport size' moja.

Vilevile barua ya maombi na nakala ya mkataba wa kazi.

URAIA WA TANZANIA

Hapa panahitajika barua kutoka ofisi ya Uhamiaji, nakala ya hati ya kusafiria na picha 'passport size' moja.

**MAOMBI YA KAZI/AJIRA NDANI YA NCHI**

Panahitajika barua ya ofisi anayotarajia kuajiriwa kama benki, kampuni za ulinzi.

Pia nakala ya kitambulisho cha mhusika na picha 'passport size' moja. Vilevile barua ya maombi kama mhusika hatoki kwenye taasisi.

**MAOMBI YA HATI YA TABIA NJEMA KWA WAGENI WALIO NJE YA NCHI**

Panahitajika nakala ya hati ya kusafiria na picha 'passport size' moja.

Vilevile alama za vidole zilizochukuliwa kutoka kituo chochote cha polisi katika nchi ambapo mhusika anaishi, pia barua ya maombi.

***Imetolewa na:***
***Ofisi ya Uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi***
***Dar es Salaam.***
***habariphq@gmail.com***



# TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Maneno yawapayo watu shida

KWA mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha (Zanzibar), lugha ya Kiswahili imepanuka sana na matumizi yake yameenea kwa kasi duniani kuliko watu wengi walivyotarajia. Imevuka kiwango cha kuwa lugha ya taifa na kuwa na hadhi ya kimataifa.

Sasa Kiswahili kimevuka mipaka ya Afrika Mashariki na kusambaa katika mabara yote ulimwenguni. Tayari kimekuwa miongoni mwa lugha zinazotumika katika mikutano ya kimataifa na mawasiliano ya intaneti (mtandao wa mawasiliano kimataifa wa kikompyuta).

Kutokana na mabadiliko na maendeleo hayo, pameibuka matumizi ambayo si fasaha, na mara nyingine si sahihi, katika mfumo wa sarufi, matamshi na hata maana ya maneno ya lugha hiyo.

Kwa mfano neno 'kwa' hutumiwa mno na wazungumzaji kama ilivyo kwenye vyombo vyetu vya habari. Neno hili lina maana nne: Linaunganisha sentensi mbili; neno linalotumika kuhusisha tendo na kifaa kinachotumika kutendea.

Neno linaloeleza namna tendo lilivyofanyika: "Amesoma kwa shida sana;" "anaishi kwa mashaka" (shida zinazompata mtu katika maisha); neno linaloeleza pahali tendo lilipofanyika: "Amepelekwa kwa daktari; ingawa ni mbali lakini amekwenda kwa miguu."

Neno linaloonesha kwenda, kutoka au kukaa mahali panapomilikiwa na mtu mwingine: "Atakwenda kwa baba yake." Namna, jinsi ya kutenda jambo: "Tembea kwa maringo." Neno linalobainisha uwiano baina ya mambo mbalimbali: "Wamefungana mabao mawili kwa mawili." Neno linaloonesha sehemu za hesabu kitarakimu, kwa mfano: "Nne kwa tano (4/5)."

Neno linalotumika kuunganisha vitu viwili katika kulinganisha: "Walishindana nyumba kwa gari;" neno linalounganisha kitu kimoja na kingine katika utendaji. Pamoja na ufafanuzi huu, bado neno 'kwa' hutumiwa tofauti na maudhui (mambo yanayoelezwa katika hadithi, riwaya, hotuba, tamthilia au masimulizi yoyote yale) yake. Hukereka (sumbuliwa na jambo; chukizwa) kila nisikiapo redioni, kwenye runinga au kusoma magazetini jinsi wanadamu wanavyolinganishwa na mtambo/mitambo! Mfano: "Bony atupia Ivory Coast ikitesti mitambo." Neno 'tupia' nilikwisha eleza jinsi linavyotumika kwa hiyo niwieni radhi kwa kutolitanzua tena.

'Testi' si Kiswahili ingawa hutumiwa sana na magazeti yetu ya michezo. Maana yake ni jaribu, tahini; pima. Aidha 'mtambo' ni kifaa chenye kutoa nguvu za kuendesha vitu vinavyofanya kazi mbalimbali; kamba inayotengenezwa kwa chane za miyaa na hutumiwa kuvutia mtego wa samaki.

Vilevile 'tupia' nililitolea maana yake kwenye matoleo yaliyopita. Neno hilo latokana na 'tupa' lenye maana ya peleka au vugumiza kitu kisichohitajika kwenye kikapu au shimo la taka; acha bila kutunza; rusha kitu kutoka ulipo kwenda mbali. Pia ni kifaa kigumu cha chuma cha kukerezea au kunolea vitu vingine, mfano kisu, panga, jembe n.k.

"Yanga mpya balaa" ni kichwa kilichofuatiwa na habari ifuatayo: "Licha ya maneno ya kejeli kutokana kwa watani zao, Yanga wametamba kujua wanachokifanya kuhusiana na usajili wanaoendelea nao, hasa wa wachezaji wa kigeni."

'Balaa' ni jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; kisirani, nuksi. Pia ni jambo lenye kuleta hali ya kutoelewana; kizaazaa, mtafaruku, beluwa. Je, ni kweli Yanga mpya ni 'hasara, kisirani au nuksi?'

Aidha sentensi ya mwandishi imeandikwa shaghalabaghala (shelabela; upogoupogo; bila mpango). Ingeandikwa: "Licha ya maneno ya watani wao, Yanga wanasema wanajua wanachofanya kuhusu usajili, hasa wachezaji wa kigeni."

"Okwi: Sina bifu na Simba." Wasiwasi wangu ni waandishi wa leo kushabikia sana maneno ya mitaani ambayo Waingereza huyaita 'slang.' Imenilazimu kutumia neno la Kiingereza ili kuwazindua waandishi wanaopenda sana matumizi ya kigeni ingawa yapo ya Kiswahili! Mwandishi angeandika: "Okwi hana kinyongo na Simba kwa kutoshirikishwa kwenye tuzo za MO Simba Award msimu huu.

Hata hivyo habari hiyo yenye aya (paragrafu) tano, mwandishi haelezi mtu aliyesema au wanaosema Okwi ana kinyongo kwa kutoshirikishwa kwenye tuzo za MO Simba Award. Malalamiko hufuatiwa na kinyongo. Mwandishi haelezi jinsi Okwi anavyolalamika hata kuwa na kinyongo alichokiita 'bifu.'

Maana ya 'beef' ni nyama ya ng'ombe lakini pia kwa maana nyingine (kwa Waingereza wenyewe), ni maneno ya mitaani yakimaanisha kuwa na dukuduku, lalamika. Kwa mfano maana ya 'beef up' ni imarisha.

Jambo lingine lililonishangaza ni mwandishi wa habari husika kuandika sentensi moja yenye maneno 66 bila kidoto (nukta)!

Nimeeleza mara nyingi kuwa kuna maneno ya kuandika na yanayozungumzwa lakini nafanywa 'punguani' (upungufu wa akili)!

"Straika mpya Yanga tema mate chini!" Hiki ni kichwa cha habari katika gazeti la michezo. 'Straika' si neno la Kiswahili ingawa latumiwa sana na waandishi wa habari za michezo. Neno hili kwa Kiingereza latokana na 'strike' na maana yake ni piga, gonga, bisha, chapa, mgomo. 'strike at the roof of something' yaani kata mzizi wa fitina; ondoa kiini cha tatizo. 'Strike while the iron is hot" (methali) maana yake chuma kikunje kingali na moto au samaki mkunje angali m-bichi.

***Methali: Maji ya pondo hayataki tanga.***

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

## NA MWALIMU REUBENI LUMBAGALA

# Mzazi mtie moyo mwanao anapofanya vibaya masomoni



Baadhi ya wanafunzi wakimpongeza mwenzao aliyefanya vizuri zaidi katika mtihani wa taifa. **PICHA: MTANDAO**

MAISHA ya kusoma yamejaa changamoto nyingi ambazo mwanafunzi anahitaji msaada kutoka kwa wazazi au walezi wake.

Wazazi na walezi ni washirika wakubwa wa mafanikio ya kielimu ya mtoto au watoto.

Inapotokea mtoto amefanya vibaya katika masomo, kama wazazi na walezi tuna wajibu mkubwa wa kumsaidia mtoto huyo ili atoke hapo alipo na apige hatua mbele ili azidi kusonga mbele.

Wapo wazazi wa aina tatu ambao mtoto anapofanya vibaya katika masomo huchukua hatua.

**WASIOJALI**

Aina ya kwanza ya wazazi ni ile ambayo haijali pale mtoto anapofeli masomo. Kwao huchukulia kama ni jambo la kawaida tu.

Mzazi aliye katika kundi hili hajisumbui kumuuliza mtoto kulikoni mpaka matokeo yake yamekuwa vibaya kiasi hicho.

Kwa mzazi au mlezi wa aina hii, kwake hajihesabu kama ana wajibu mkubwa wa kufuatilia masomo ya mwanawe. Ni wazazi wanaopuuzia mambo ya msingi maishani.

**WATUMIA VIBOKO**

Lakini liko kundi vilevile la wazazi ambao wanapopokea mitihani ya watoto wao au ripoti ya maendeleo ya watoto wao, wakaona kuwa wamefeli, wao huwa hawana cha kuuliza bali ni kuchukua kiboko na kuanza kuwachapa. Mzazi aina hii angalau kidogo anajali elimu ya mwanae na anataka afanye vizuri. Na ndiyo maana anaumia anapomuona mwanawe amefeli tofauti na matarajio yake.

Udhaifu wa mzazi au mlezi huyu ni mmoja tu, anatangulia kumwadhibu mtoto aliyefeli bila hata ya kuzungumza naye na kujua kulikoni hadi imetokea hajafanya vyema katika masomo yake.

**WANAOJADILI**

Aidha, kuna kundi la wazazi ambao wanapopokea ripoti au mitihani ya watoto wao na wakaona hawajafanya vizuri, huamua kukaa kitako na watoto wao na kuanza kujadili hali hiyo ya kufeli.

Kwangu mzazi au mlezi wa aina hii anafanya jambo la busara sana ambalo ningetamani wazazi wengi tufuate mkondo huu. Mtoto aliyefeli huhitaji sana msaada wa mzazi au mlezi wake katika kushughulikia tatizo hilo la kufeli.

Kama mzazi au mlezi ni wajibu wako kukaa na mwanao kujadili nini kimesababisha kufeli kwake.

Na mazungumzo haya yafanyike katika hali ya urafiki mkubwa baina ya mzazi na mtoto wake. Hii itamsaidia sana mtoto kuwa wazi kueleza tatizo la msingi lililosababisha kufanya kwake vibaya katika masomo.

Pamoja na maelezo ambayo mtoto ataamua kumweleza mzazi au mlezi wake kama sababu iliyosababisha kufeli kwake, bado mzazi ana jukumu kubwa la kumjenga mwanawe kisaikolojia ili asiendelee kufeli.

**UJASIRI**

Kwanza mzazi anapaswa kumjengea mwanawe ujasiri na kujiamini kuwa anaweza kufaulu na hilo la kufeli ni kama ajali tu, imetokea katika safari ya masomo.

Hili likifanyika litaamsha ari ya mwanafunzi huyu aliyefeli kuamini kuwa anaweza kufaulu.

> Na mazungumzo haya yafanyike katika hali ya urafiki mkubwa baina ya mzazi na mtoto wake. Hii itamsaidia sana mtoto kuwa wazi kueleza tatizo la msingi lililosababisha kufanya kwake vibaya katika masomo.

Kuanza kumpiga mtoto eti kisa tu amefeli haitasaidia, sanasana inaweza kuwa ndio mwendelezo wa mtoto huyo kufeli zaidi mbeleni.

Kwa sababu jambo lililosababisha kufeli kwake litakuwa bado halijewekwa bayana na mhusika mwenyewe.

Katika mazingira ambayo mzazi atamtia moyo mwanawe kuwa "Wewe mwanangu una akili sana, kinachotakiwa ongeza bidii zaidi katika kusoma." Kunaweza kukawa msaada mkubwa kwa sababu matatizo mengine yanatatuliwa kwa msaada wa kiushauri (moral supports).

**UZEMBE**

Lakini pia mzazi amsisitize mwanawe asizembee katika masomo. Maneno matupu peke yake ya kumshauri mtoto yanaweza yasilete matunda kama mtoto hataweka msisitizo wa kusoma.

Hakuna jambo jepesi chini ya jua. Ni wajibu wa mzazi kuliweka hili sawa. Pamoja na kumtia moyo mwanawe kuwa ana akili, lakini suala la kuongeza juhudi masomoni halikwepeki.

Kwa kufanya hivi naamini mtoto huyu ambaye alianza kufeli mitihani, hali yake itabadilika pale atakapopata msaada wa mzazi wake.

> Hakuna jambo jepesi chini ya jua. Ni wajibu wa mzazi kuliweka hili sawa. Pamoja na kumtia moyo mwanawe kuwa ana akili, lakini suala la kuongeza juhudi masomoni halikwepeki.

**USHIRIKIANO MZAZI, WALIMU**

Lakini pia mzazi anapaswa kushirikiana na walimu wanaomfundisha mtoto wake ili kuona njia nyingine bora ya kufanya kwa minajili ya kumnasua mtoto huyu katika hatari ya kufeli zaidi masomoni.

Wazazi na walezi wasione suala la kufeli kwa watoto wao kama ni jambo la kawaida ambalo halihitaji ufuatiliaji wa haraka.

Pale tu mzazi au mlezi unapogundua taaluma ya mwanao imeshuka, jitihada za makusudi zifanyike kuokoa jahazi.

Kuwahi kuchukua hatua ni sawa na mtu mwenye ndugu yake ambaye ni mgonjwa akawahi kumpeleka hospitali kupata matibabu. Mgonjwa huyo atapata tiba haraka na afya yake itaimarika.

Kuchelewa kumpeleka mgonjwa hospitali ni kumchelewesha mgonjwa kuanza kupata matibabu na mgonjwa atakuwa katika hatari ya kupoteza maisha.

Kwa nini mtoto afeli zaidi wakati mzazi au mlezi una uwezo wa kuwahi tiba kwa njia ya kufuatilia maendeleo ya masomo ya mwanao shuleni?

Vyovyote itakavyokuwa mzazi mtie moyo mwanao anapofanya vibaya masomoni ili umwokoe badala ya kumpoteza. Tafakari.

***Mwandishi wa Makala hii ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyopo Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma. Maoni 0764-666349.***

ELIMU

NA FRANSISKO MPANGALA

# Imani hizi kuhusu dhamana zipuuzwe

KUMEKUWA na maoni kutoka kwa baadhi ya watu katika majukwaa mbalimbali ikiwamo mitandao ya kijamii kwamba kwenye baadhi ya kesi, watuhumiwa hunyimwa dhamana kutokana na sababu mbalimbali.

Na kwamba baadhi ya sababu hizo sanasana huhusishwa na masuala ya kisiasa au uwapo wa mikono ya watu wengine nje ya mfumo wa Mahakama wanaozuia dhamana hizo kwa madhumuni mengineyo nje ya sababu za kisheria.

Kwa jinsi watu hao wanavyotoa maoni yao, unapata picha kuwa hawana imani kabisa na Mahakama kwenye baadhi ya kesi.

Binafsi ninapinga vikali mitazamo hii potofu na nadhani kuna haja ya kuelimisha watu kuwa Mahakama ni mhimili huru usioingiliwa na mhimili mwingine au sababu zozote zile zikiwamo za kisiasa wakati wa kufanya maamuzi yake.

Inawezekana watu hawa hawafahamu kuwa yapo baadhi ya mambo au sababu za kisheria ambazo zinaweza kumfanya mtu kukosa dhamana.

Msingi wa makala haya ni kutoa elimu ya sababu zipi zinazoweza kumfanya mtuhumiwa kukosa dhamana.

**DHAMANA NI NINI?**

Dhamana ni ruhusa ya kuwa huru anayoweza kupewa mtuhumiwa wakati uchunguzi wa kosa lake unaendelea au shauri lake likiendelea kusikilizwa mahakamani, au akisubiri uamuzi wa rufani yake.

> “Inawezekana watu hawa hawafahamu kuwa yapo baadhi ya mambo au sababu za kisheria ambazo zinaweza kumfanya mtu kukosa dhamana.



Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Kanda ya Mbeya, Robert Makaramba (wa tatu kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na baadhi ya watumishi wa Mahakama Kanda ya Mbeya.



Baadhi ya watuhumiwa (waliovaa kiraia), wakisindikizwa kuingia mahakamani. **PICHA: MTANDAO**

> “Kwa kuzingatia dhana hii ni muhimu kumruhusu mtuhumiwa kwa kumpa dhamana apate kuwa nje ya kizuizi mpaka hapo tuhuma zake...

Dhamana ni haki inayopata msingi wake katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ina dhana inayotamka kwamba mtu hatochukuliwa kuwa mwenye hatia mpaka tuhuma zithibitishwe dhidi yake.

Ibara ya 13 (6) (b) ya Katiba inatamka kuwa ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo.

Kwa kuzingatia dhana hii ni muhimu kumruhusu mtuhumiwa kwa kumpa dhamana apate kuwa nje ya kizuizi mpaka hapo tuhuma zake zitakapothibitishwa na Mahakama.

Kwa mantiki hii, dhamana ni haki ya mtuhumiwa na wala haitolewi kama upendeleo au zawadi.

> “Mtuhumiwa anaweza kupewa dhamana, lakini vitendo vya kutotekeleza masharti ya dhamana kunaweza kumsababishia kufutiwa au kunyimwa dhamana.

Kutokana na mitazamo hiyo ya baadhi ya watu nimeona kuna haja ya kutolea ufafanuzi wa kisheria.

Hivyo basi, zifuatazo ni sababu mbali mbali zinazoweza kumfanya mtu kukosa dhamana.

MAKOSA YASIYORUHUSU DHAMANA KISHERIA

Kuna makosa ambayo hayaruhusu dhamana kisheria.

Haya ni pamoja na makosa kama ya kuua kwa kukusudia, uhaini, unyang'anyi wa kutumia silaha, ugaidi na kunajisi ambayo ni kati ya makosa ambayo yanaweza kumfanya mtu akakosa dhamana.

Msingi wa kumnyima dhamana mtuhumiwa wa makosa haya ni kuwa, makosa haya yana adhabu kubwa pale mtuhumiwa akipatikana na hatia, hivyo basi kuna uwezekano mtuhumiwa huyo wa kutoroka.

Ili kujihakikishia uwepo wa mtuhumiwa kipindi chote cha kesi, mtu huyo inabidi aendelee kukaa kizuizini mpaka kesi yake itakapofikia tamati.

Kwa mfano mtu anayeshtakiwa kwa makosa ambayo adhabu yake ni kunyongwa ana uwezekano mkubwa sana wa kutoroka kuliko mtu ambaye anatuhumiwa kwa makosa ambayo adhabu yake inaweza kuwa ni faini.

**MTUHUMIWA KUKIUKA MASHARTI YA DHAMANA**

Kama mtuhumiwa amekiuka masharti ya dhamana au ana tabia ya kutokuheshimu masharti ya dhamana, inaweza kuwa ni sababu ya mtuhumiwa kunyimwa dhamana.

Mtuhumiwa anaweza kupewa dhamana, lakini vitendo vya kutotekeleza masharti ya dhamana kunaweza kumsababishia kufutiwa au kunyimwa dhamana.

Kwa mfano mtuhumiwa anapewa sharti la kurudi mahakamani kila kesi yake inapotajwa, akishindwa kufika bila sababu za msingi inaweza kumfanya mtuhumiwa huyo kufutiwa au kunyimwa dhamana.

Mtuhumiwa anapaswa kuheshimu sana masharti ya dhamana kuepuka kutotumiwa kwa hiyo hoja, ikitokea kesi nyingine kuonyesha mtuhumiwa huyo huwa haheshimu masharti ya dhamana.

**USALAMA WA MTUHUMIWA MWENYEWE**

Endapo usalama wa mtuhumiwa utakuwa hatarini, inaweza kuwa sababu ya mtu

**Inaendelea Uk. 18**

JIELIMISHE

## UTAFITI: KUBADILI MWENENDO WA KULALA NA KUAMKA NDIO SULUHISHO

KUBADILI mwenendo wa kulala kunaweza kubadilisha mfumo wa mwili wa mwanadamu hali ambayo inasaidia kuimarisha afya, wanasema wanasayansi wa Uingereza na Australia.

Utafiti wao uliangazia zaidi ndege aina ya bundi, ambao mfumo wa miili yao huwezesha kuwa macho usiku kucha.

Mfumo huo unaweza kutumiwa kwa kuhakikisha mtu analala wakati mmoja kila siku, kuepuka kunywa vinywaji vilivyo na caffeine kama vile chai na kupata mwanga wa jua, hasa saa za asubuhi.

Watafiti wanasema mpangilio huo unaonekana kuwa wa kawaida lakini ni muhimu kwa sababu unaweza kubadilisha maisha ya watu.

Kila mtu ana saa zake za kulala ambazo zinaambatana na kuchomoza na kuzama kwa jua. Ndio maana tunalala usiku.

Lakini mfumo wa miili ya watu inatofautiana na ya wengine.

Kuna wale wanaoamka mapema, lakini hawawezi kukaa macho kwa muda mrefu wakati wa usiku; na wengine wanaoweza kukaa macho kwa muda mrefu nyakati za usiku wakati kila mtu amelala.

Watu hao wanasemekana huenda wakapata matatizo ya kiafya.

Wanasayansi waliwafanyia uchunguzi watu 21 ambao ‘hukaa macho bila kulala hadi usiku wa manane na kulala hadi saa nne asubuhi.’

Walipewa maagizo yafuatayo:

Kwamba waamke saa 2-3 mapema kabla ya saa zao za kawaida na wapate mwangaza wa kutosha saa za asubuhi.

Kwamba wapate kifungua kinywa mapema kadri iwezekanavyo.

Vilevile wafanye mazoezi nyakati za asubuhi pekee.



Aidha, wale chakula cha mchana wakati mmoja kila siku na wasile chochote baada ya saa moja usiku.

Lakini waache kutumia vinywaji vilivyo na caffeine baada ya saa tisa mchana.

Kwamba wasilale baada ya saa kumi.

Walale saa 2-3 kabla ya saa zao za kawaida na kujiepusha na sehemu zilizo na mwangaza saa za jioni.

Vilevile wahakikishe wanalala wakati mmoja na kuamka wakati mmoja kila siku.

Baada ya wiki tatu, watu hao walibadili mfumo wa miili yao ya kulala, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo uliofanywa na vyuo vikuu vya Birmingham, Surrey na Monash.

Matokeo ya utafiti huo uliochapishwa katika jarida la matibabu, unaonyesha kuwa watu wanaweza kulala wakati mmoja kila siku.

Lakini pia iliripotiwa viwango vya chini vya usingizi na msongo wa mawazo huku uchunguzi zaidi ukionyesha kuwa hali yao ya afya pia iliimarika.

“Kufuata mwenendo rahisi wa kufanya mambo kunaweza kuwasaidia watu walio na tatizo la kulala kuimarisha afya zao za kiakili,” anasema Prof. Debra Skene kutoka Chuo Kikuu cha Surrey na anaongeza:

“Ukosefu wa usingizi unaweza kuathiri mfumo wa mwili wa mwanadamu, hali inayoweza kumweka mtu katika hatari ya kupata maradhi kama vile ya moyo, saratani na kisukari.”

Kuwa na tatizo la kutolala na kuamka wakati mmoja kunaweza kuvuruga mfumo wa mwili wa mtu, hali inayojulikana kama (circadian rhythm).

Mfumo wa kulala na kuamka kwa wakati mmoja kila siku kunaweza kutumiwa kuwasaidia watu kuimarisha afya zao.

Hata hivyo, watafiti hawakuweza kubaini ikiwa wale walio na tatizo sugu la kukesha usiku wakati wenzao wamelala wanaweza kunufaika na tiba hiyo rahisi.

“Bila shaka hoja kuu ni ikiwa mtu ana tatizo sugu la kulala, anaweza vipi kubadili hali hiyo?” Dk. Andrew Bagshaw wa Chuo Kikuu cha Birmingham anauliza.

“Hivi ni vitu vya kawaida ambavyo kila mtu anaweza kufanya na ambavyo vinaweza kuleta mabadiliko makubwa, na kwangu hivyo ni vitu vinavyo nishangaza,” anaongeza:

Anabainisha kwamba kuwa na uwezo wa kusaidia watu kwa kutumia mfumo huu rahisi wa tiba ni jambo la kutia moyo sana.

**BBC**

# Imani hizi kuhusu dhamana

Inatoka Uk. 17

kunyimwa dhamana.

Ikithibitika na Mahakama kwamba ni muhimu kwa mtuhumiwa kuwekwa chini ya ulinzi kwa ajili ya ulinzi au usalama wake, basi mtu huyo hatapewa dhamana. Kwa mfano mtuhumiwa anaweza kuwa amefanya jambo ambalo limeamsha hasira kali kwenye jamii, kuna uwezekano wa kunyimwa dhamana kwa hofu kwamba watu wanaweza kuchukua sheria mkononi dhidi yake.

**USALAMA WA JAMII**

Mtuhumiwa pia anaweza kunyimwa dhamana kwa ajili ya usalama wa jamii. Hii inatokea iwapo kama mtuhumiwa akiachiwa kuna uwezekano wa kwenda kuendelea kufanya makosa mengine. Kwa mfano kila mtuhumiwa akiachiwa amekuwa ni mtu mwenye fujo au ana tabia za kuwapiga wanawake.

Hili likithibitika mtuhumiwa anaweza kunyimwa dhamana kwa maslahi ya usalama ndani ya jamii kwa kumwepusha mtu huyo kuendelea kufanya makosa.

**MTUHUMIWA KUVURUGA UPELELEZI**

Ikithibitika kuwa mtuhumiwa akiachiwa kwa dhamana anaweza kuvuruga upelelezi nayo inaweza kuwa sababu ya mtu kunyimwa dhamana.

Endapo ikionekana kuwa mtuhumiwa akitoka anaweza kwenda kuvuruga upelelezi kwa njia ya kuondoa, kufuta au kurekebisha ushahidi ili umuweke kwenye nafasi ambayo itamsaidia kumpa ushindi au kuathiri mwenendo wa kesi, basi mtu huyo naye atanyimwa dhamana.

Hayo ndiyo mambo ya kisheria yanayoweza kumfanya mtu akakosa dhamana.

Hivyo basi maoni yanayotolewa na baadhi ya watu hayana ukweli wowote kwani mtu akinyimwa dhamana, sababu zitaangukia kwenye moja ya hizo hoja za kisheria zilizotajwa.

Nimeona kuna haja ya kutolea ufafanuzi hili ili kusaidia wasiofahamu kwa maslahi ya Mahakama, kwani madai au hisia hizi zisipojibiwa kwa wakati au zikapuuzwa zinaweza kujenga imani potofu dhidi ya mhimili wa Mahakama

Mahakama ndio mhimili wenye wajibu

## JE, WAJUA?



Vijana wakiwa makini na simu zao za mkononi. Utafiti unaonyesha matumizi yaliyopitiliza ya simu chanzo cha wanafunzi kuwa na wapenzi wengi. .**PICHA: MTANDAO**

# Matumizi yaliyokithiri ya simu chanzo wanafunzi kuwa na wapenzi wengi?

KATIKA utafiti wa zaidi ya watu 3,400 nchini Marekani wanaosoma shahada ya kwanza, wale waliosema wana matatizo na muda wanaotumia katika simu zao wanaripotiwa kuwa na wapenzi wengi pia.

Aidha, wanadhaniwa kuwa na msongo wa mawazo. Mmoja wa watafiti anasema kuwa matokeo ya utafiti huo yanashangaza.

Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Chicago, Cambridge na Chuo Kikuu cha Minnesota, wamefanya utafiti huu wa tabia za uraibu wa simu.

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kutaka kujua hali ya afya ya akili ya wanafunzi na jinsi gani simu zina matokeo katika utendaji wao.

Ili kujua matumizi yaliyopitiliza ya simu za mkononi, wanafunzi waliulizwa maswali mbalimbali yakiwamo yafuatayo;

- Rafiki zako na familia wanakulalamikia kuhusu matumizi makubwa ya simu?
- Una matatizo yoyote darasani kutokana na matumizi ya simu?
- Unadhani muda unaotumia katika simu umeongezeka?

Mwanafunzi mmoja kati ya watano miongoni mwa waliojibu maswali walikubali maswali yote, na kuwafanya kuwa watumiaji wa kupitiliza wa simu, miongoni mwao wengi ni wanawake.

**MAHUSIANO**

Kwa hao wenye matumizi yaliyozidi ya simu za mkononi, wameripotiwa pia kuwa na uhusiano wa kimapenzi na zaidi ya mwenza mmoja katika kipindi cha miezi 12, kuliko wale waliokutwa hawana matumizi makubwa ya simu.

Asilimia 37.7 ya wenye uraibu wa matumizi ya simu, wamekadiriwa kuwa na wapenzi hadi sita ndani ya miezi 12, ikilinganishwa na asilimia 27.2 ya walioripotiwa kutokuwa na tatizo la matumizi makubwa ya simu.

Dk. Sam Chamberlain, mmoja kati ya waandishi wa utafiti huu kutoka Chuo Kikuu cha Cambridge anasema sababu ya suala hili ni ngumu kuijua.

"Inawezekana kuwa watu wanatumia sana simu na kukutana na wapenzi mtandaoni na wanaweza pia kusahau mahusiano ya kila siku kwa sababu ya matumizi yaliyokithiri ya simu za mkononi," anasema na kuongeza:

"Kama hili suala lingekuwa na faida, basi ingekuwa kinyume na matokeo badala yake afya ya akili ingekuwa imeimarika."

Watafiti pia waligundua unywaji wa pombe kupita kiasi unawakumba wale wanaotumia simu kwa muda mrefu zaidi. Lakini hawakukutwa na uraibu mwingine wowote.

Baadhi ya wataalamu wanapendekeza kuwa uchezaji wa 'game', ambao umewekwa katika kundi la tatizo na Shirika la Afya Duniani (WHO), ujumuishwe pia kwenye tatizo la kukaa muda mrefu katika vioo vya simu.

Tafiti za nyuma zimeonyesha uhusiano wa kufeli kwa wanafunzi na matumizi ya simu, na ripoti hii pia ina uhusiano na suala hilo.

"Hata matokeo ya tatizo hili yana madhara yake katika taaluma ya mtu na baadaye katika kipindi chake cha kufanya kazi," anasema Profesa Jon Grant wa Chuo Kikuu cha Chicago.

Dk. Abigael San anasema kuwa anafurahia utafiti huu umefanyika: "Haya madhara yote ni ya kweli na tunatakiwa kuyazingatia... watu wengi wanaweka tatizo hili kama tatizo la afya ya akili ama kuvunjika kwa mahusiano, lakini hayo yote yanachangiwa na matumizi ya simu za mkononi."

***BBC***

# UTAFITI

## RIPOTI YA ILO:

## ONGEZEKO LA JOTO KUGHARIMU KAZI MILIONI 80 KUFIKIA MWAKA 2030

MAKADIRIO kwa kuzingatia ongezeko la joto la dunia la nyuzi joto 1.5 kufikia mwishoni mwa karne hii, yanaonyesha kuwa kufikia mwaka 2030, asilimia 2.2 ya jumla ya muda wa saa za kazi kote duniani utapotea kutokana na joto kali, na ni hasara sawa na nafasi za kazi milioni 80.

Hiyo ni sawa na hasara ya uchumi wa dola za Marekani bilioni 2,400, inasema ripoti mpya ya ILO iliyotolewa jijini Geneva nchini Uswisi na pia kwa mujibu wa maelezo ya ziada ya Patrick Newma.

Ripoti hiyo ya ILO iliyopewa jina 'Kufanya kazi katika sayari yenye joto: Athari ya msongo wa joto kwa uzalishaji na kazi rasmi,' imekusanya taarifa za tabianchi, saikolojia na ajira na inawasilisha makadirio ya hasara za sasa na makadirio ya hasara za uzalishaji kwa ngazi ya kitaifa, kikanda na kidunia.

Msongo wa joto ni joto la ziada zaidi ya lile ambalo mwili unaweza kuhimili bila kuathirika. Kiujumla hutokea juu ya nyuzi joto 35 katika fukuto la juu.

Joto kubwa la ziada wakati wa kazi ni hatari kwa afya, linaathiri utendaji kazi na uwezo wa watu na hivyo kuathiri uzalishaji.

Katika mazingira mengine hali hiyo inaweza kusababisha kiharusi kinachotokana na joto na kinaweza kuwa hatari, inafafanua ripoti hiyo ya ILO.

Sekta ambayo inategemewa kuathirika zaidi ni kilimo. Watu milioni 940, duniani kote wanafanya kazi katika sekta ya kilimo.

Inakadiriwa kuwa asilimia 60 ya muda wa kazi utapotea kufikia mwaka 2030 kutokana na msongo utokanao na joto.

Sekta ya ujenzi nayo inategemewa kuathirika pakubwa.

Sekta nyingine zinazotegemewa kuathirika iwapo hatua hazitachukuliwa ni usafiri, utalii, michezo na kazi kadhaa za viwandani.

Athari za hali hii hazitakuwa na mgawanyo sawa kwani nchi zinazotegemewa kuathirika zaidi ni Asia ya Kusini na Afrika Magharibi ambako takribani asilimia 5 ya saa za kazi zinategemewa kupotea kufikia mwaka 2030.

Zaidi nchi zilizoko katika maeneo maskini zitaathirika zaidi. Chatherine Saget, mkuu wa kitengo cha utafiti cha ILO amesisitiza kwamba athari za msongo utokanao na joto kwenye uzalishaji ni matokeo mabaya ya mabadiliko ya tabianchi.

"Tunaweza kutegemea kuona kukosekana kwa usawa zaidi katika nchi za kipato cha chini na cha juu na kuathiri zaidi hali ya ufanyaji kazi kwa walioko hatarini zaidi," anasema.



Wafanyakazi wa ujenzi katika kituo cha kuzalisha umeme wa maji cha Trung Son Vietnam.
**PICHA: MTANDAO**

***UN***

# zipuuzwe

na kauli ya mwisho kwenye kutoa haki kwa mujibu wa ibara ya 107A (1) ya Katiba ya nchi.

Pia katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, Mahakama zipo huru na zinalazimika kuzingatia masharti ya Katiba na Sheria za nchi kwa mujibu wa ibara ya 107B ya Katiba ya nchi, na si vinginevyo.

***Fransisko Mpangala ni mchambuzi wa masuala ya sheria na siasa. Kwa maoni anapatikana kwa barua pepe fransiscompangala08@gmail.com***

> Endapo ikionekana kuwa mtuhumiwa akitoka anaweza kwenda kuvuruga upelelezi kwa njia ya kuondoa...



## UCHAMBUZI WA KITABU;

# YOU CAN WIN by Shiv Khera (Unaweza Kushinda)

**K**ILA mmoja anapenda kushinda. Ushindi unampa mtu ujasiri na hata mafanikio makubwa.

Mwandishi Shiv Khera anatukaribisha sote kufahamu hatua nane za mambo muhimu kwa mwongozo wa maisha bora na ya ushindi.

Hizi hatua zinabebana na zitakupa matokeo bora pale ambapo hutazitenganisha. Kitabu hiki ni zawadi ambayo ukienda kuifungua na kuijali kwa hizi hatua nane hutabaki ulipo sasa.

**UMUHIMU WA MTIZAMO**

Mtizamo ni kila kitu katika maisha. Mtizamo ni namna uonavyo mambo katika maisha na kuyapa tafsiri yake.

Kuona huku na kutafsiri mambo kunaweza kuathiriwa na mazingira yanayomzunguka mtu, uzoefu wake, makuzi, elimu yake, matukio katika maisha.

Mtizamo mbaya unapelekea kushindwa katika maisha na ni mlango wa tabia mbaya kukua na kuharibu matokeo bora ya mafanikio.

Na kufanya mtizamo wako uwe bora, basi kila siku akili ilishwe mambo yanayojenga na kufanya kufikiri kuwe bora zaidi. Kwa namna hii unajiwekea mazingira mazuri ya kushinda na kufanikiwa.

**MAFANIKIO NA MIKAKATI YA USHINDI**

Mafanikio sio ajali, ila ni matokeo ya mtizamo unaootoa uchaguzi na hapa inakosoa kauli ya mafanikio ni kama bahati ijayo pasipo sababu nyuma yake. Earl Nightingale anasema mafanikio ni mwendelezo wa kutambua lengo fulani kubwa.


Wivu, hofu, kukosa malengo, kuahirisha mambo, kukosa 'fokasi' na vipaumbele: Haya mambo ni kikwazo katika kufanikisha malengo na jambo moja lenye usalama ni kuyaepuka na kuwa tayari katika safari ya kufikia mambo magumu kuwa rahisi.

Bila kuwa na mikakati huwezi kufanikiwa katika maisha.

**JIHAMASISHE, HAMASISHA WENGINE**

Watu wanasikia masomo mengi na hata mafundisho mengi sana ya kuchukua hatua lakini kwanini hakuna matokeo mazuri?

Jibu ni wengi kukosa hamasa ya mara kwa mara ili kusonga mbele na hatua. Na hamasa huja zaidi pale panapo kuwepo utoshelevu baada ya kufanya kitu au kupata kitu fulani.




Inawezekana kupongezwa, vyeti, zawadi na kupandishwa cheo. Jihamasishe mwenyewe kwa ushindi mdogo unaopata katika maisha na hii itakupa kushinda mambo makubwa.

**KUJITHAMINI**

Kujiona vizuri na kujithamini ni njia mojawapo ya kuwa mtu mshindi. Namna unavyojiona kuna athari kubwa sana katika maisha yako ya furaha, na yaliyo na utoshelevu.

Pia kujithamini ni pamoja na kuwa mwajibikaji na kuyaona maisha kwa sura nyingine nzuri zaidi. Jione wa thamani kila siku za maisha yako na hii itakupa ujasiri na hali ya kushinda mambo katika maisha.

**UJUZI WA KUHUSIANA NA WENGINE**

Maisha ni mwangwi. Na namna unavyotoa kile kwa watu ndivyo uwezekano mkubwa wa kupata kile kile unavyozidi kuwa.

Kadri unapotatua matatizo ya watu, ndivyo unapojenga mahusiano ya karibu nao. Ujuzi huu wa kuhusiana na watu unajenga hali ya ushindi na mafanikio makubwa ndani ya mtu.

Uaminifu ni msingi wa mahusiano yoyote yale, ukipotea tu basi na mahusiano huwa katika mpasuko.

Kuvunjika kwa uaminifu kunasababishwa na mambo mengi, machache kati ya hayo ni pamoja na kukosa uadilifu na ukweli, tabia mbaya, kutotimiza ahadi na umimi. Hivyo ni muhimu sana kuwepo na uaminifu katika kujenga mahusiano mazuri baina ya pande mbili.

**TABIA NA AKILI YA KUJITAMBUA**

Ni vitendo sahihi na bora vyenye kuleta ubora na kuzalisha tabia nzuri. Mafanikio yanaathiriwa na akili ya kufikiri na pia tabia za mtu za kila siku.

Na hizi tabia huja kwa njia ya kurudia rudia baadhi ya matendo kwa kipindi kirefu sana na ndipo tabia fulani huota mizizi.

Kanuni ya GIGO (Garbage in, garbage Out), ikiwa na maana kiingiacho ndicho kitokacho, na hii ndivyo akili hufanya kazi hii ya kuathiri matendo kwa kile kinachofikiriwa wakati huo au baada ya muda mrefu.

**KUPANGA MALENGO**

Malengo yanakupa kuwa na deni katika kujitahidi kuyatimiza. Katika kupanga malengo, sharti lengo liwe mahusisi, lijulikane, liweze kupimika, kufikika, halisi na lenye ukomo wa muda. Hizi sifa zinafanya lengo kuwa bora.

Na katika urefu wa malengo yawe katika malengo mafupi, ya kati na ya muda mrefu. Malengo mazuri huwa yanaleta usawa katika kugawanya maeneo sita muhimu katika maisha; Familia, uchumi, afya, akili, mahusiano ya kijamii na kiimani. Na haya malengo yaende na maadili na misingi, mtu aliojiwekea.

**MAONO NA MAADILI**

Maono ni picha uonayo mbele yako na kama dira inayokuongoza ikiwa na msingi wa maadili. Mambo saba yanayoua na kuichafua dunia ambayo Mahatma Gandhi aliyasema ni pamoja na haya machache; kupata mali pasipo kazi, starehe pasipo utashi, maarifa pasipo haiba, biashara pasipo maadili na siasa pasipo kanuni.

Na njia nzuri mojawapo ya kupima kiwango cha maadili cha mtu binafsi ni kupiga picha kama mama angelikuwapo angeridhika na kile mtu anachokifanya?

Ni vitu vilivyo vidogo vidogo ndivyo vyenye kuleta utofauti mkubwa katika maisha.

Haya ndio mambo nane muhimu ya kuyaishi kila siku katika maisha yenye kukujengea maisha ya ushindi.

Unaweza kushinda ukiwa na mtizamo chanya wa maisha, maadili, kufikiri vizuri na kuwa na picha ya maono.

***Dk. Raymond Nusura Mgeni ni Mchambuzi wa vitabu anayepatikana kupitia 2019+255 676 559 211 raymondpoet@yahoo.com***



Safari kama hii ya kupita milima inahitaji kupambana ili kuweza kuishinda. **PICHA: MTANDAO**



# WADAU SABATO KASIKA

## SUALA la mtoto kuwa na rafiki shuleni linaweza kuwa jambo la kawaida. Je, kuna umuhimu kwa mzazi kumfahamu rafiki wa mtoto wake shuleni? Wadau wanajadili.



**PANDAGOYA NEVELE**
**(MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

BAADHI ya watoto wana tabia ambazo hazipendezi mbele ya jamii hata bila kujua chanzo chake. Ni vyema wazazi na walezi wakawa na mazoea ya kuwajua au kuwafahamu watu, ambao huwa karibu na watoto wao shuleni na hasa marafiki zao ili ikiwezekana wachukue hatua mapema za kudhibiti tabia zisizokubalika kwa watoto kabla hawajashindikana. Tukiwaacha bila kujua marafiki zao wa karibu kwamba ni wema au wabaya, matokeo yake ni kujikuta wanatuletea nyumbani tabia ambazo hazifai katika jamii. Ikumbukwe kuwa chanzo cha tabia za ajabu kwa watoto kunatokana na baadhi yetu kutofuatilia watu ambao huwa karibu nao shuleni. Kwa mzazi au mlezi, ambaye anajali maendeleo ya mtoto wake shuleni hana budi kufuatilia na kujua watu gani ambao huwa karibu na mtoto wake shuleni ili kuhakikisha anazingatia masomo na siyo mambo mengine ambayo yanaweza kumwingiza kwenye matatizo. Kikubwa zaidi ni sisi wazazi kuwafanya walimu kuwa marafiki zetu kwani nao wana sehemu kwa maendeleo ya mtoto, hayo yakifanyika itakuwa rahisi kujua marafiki wa watoto wetu kama ni wema ama wabaya.



**SOMOE DANIEL**
**(MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA kawaida katika maisha, huwa kuna mambo ya msingi ya kuzingatia kwa ajili ya maendeleo ya mtoto shuleni, lakini mie niseme tu kwamba jambo moja kubwa ni mahusiano mazuri kati ya wazazi na walimu kwenye maendeleo ya elimu na hata tabia njema kwa ujumla. Wazazi wasiwaachie walimu kazi ya kufundisha na kulea na pia walimu wasione watoto shuleni wakijiingiza kwenye tabia chafu na kuwaacha. Kila upande ukitimiza wajibu wake, nina uhakika hakutakuwa na watoto watukutu shuleni, kwani wataogopa kujiunga na vikundi vya watoto wenye tabia hizo. Hapa ninahimiza ushirikiano kwa wazazi na walimu. Ni muhimu mzazi au wazazi kutenga muda na kwenda shuleni kuonana na walimu ili kujua maendeleo ya watoto wao ikiwamo kujua tabia, kwa sababu wakati mwingine mtoto anaweza kuwa na tabia fulani nyumbani, lakini akifika shuleni anakuwa na nyingine kwa sababu tu ya kuiga kwa wenzake. Siyo vibaya mtoto kuiga jambo au tabia, lakini inategemea ni jambo la aina gani au tabia ya namna gani. Watoto wanatakiwa kuiga mambo mema. Kifupi ni kwamba nafasi ya mzazi katika kuimarisha nidhamu ya mtoto ni kubwa, hasa akiwa na uhusiano mzuri na walimu. Mzazi amfundishe mtoto maadili mema na kufuatilia mwenendo shuleni kuliko kumwacha tu na kujikuta akiharibika tabia bila yeye (mzazi) kujua.



**AMINA MWASI**
**(MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MAISHA ya sasa wazazi wengi wanatumia muda mwingi kwenye kutafuta riziki, matokeo yake watoto wakirudi kutoka shuleni hukaa na watumishi wa ndani au kushinda wakiangalia televisheni. Hapa wazazi hawajui watoto wao wanajifunza nini na wakati mwingine huangalia mambo ambayo yako juu ya umri wao na kujikuta wakiharibikiwa bila wazazi kujua. Lakini kama ulivyouliza swali lako, naomba nikujibu kwamba mzazi kujua marafiki wa mtoto wake ni nani ni jambo la msingi. Lakini pia tunapozungumzia mtoto kujifunza tabia mbaya kutoka kwa marafiki alionao shuleni ni lazima pia tuangalie huku nyumbani, kwa sababu mtoto anaweza kuwa salama shuleni lakini akaharibikiwa nyumbani kutokana na kile anachokiangalia kwenye televisheni. Hii yote inaweza kusababishwa na uhuru wa kupitiliza aliopewa na wazazi wake, hasa kutokana na kukosa muda wa kukaa naye kwa sababu ya shughuli nyingi za kila siku. Lakini jinsi dunia inavyokwenda sasa, ni vyema wazazi wakatenga muda wa kuwa na watoto wao badala ya kuhangaikia maisha tu huku nyumbani watoto wakiharibika. Wazazi wawafanye watoto kuwa marafiki wa karibu ili wagundue tabia zao badala ya kuwaacha huru kupita kiasi. Wajue pia marafiki zao shuleni ni wa aina gani na wajue wanapokuwa nyumbani peke yao huwa wanafanya mambo gani, lakini kinyume na hapo itakuwa ni sawa na kuwapoteza. Walimu wana sehemu yao, lakini wazazi nao wana wajibu mkubwa wa malezi mema kwa watoto. Mzazi anayekwepa majukumu ya malezi kwa watoto hafai kabisa.



**MADINA MUSSA**
**(MHITIMU WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM)**

MZAZI hana budi kutekeleza jukumu la malezi kwa mtoto kwa kuzingatia kwamba ndiye aliyeamua kumleta duniani. Kwani kupitia mzazi/mlezi mtoto anapata nyenzo zitakazoongoza maisha yake yote kuanzia heshima, utii, unyenyekevu na nidhamu. Kwa sababu mara nyingi wema au ubaya wa mtu ni matokeo ya aliyojifunza nyumbani. Ninaamini kuwa nyumbani ndiko msingi hujengwa. Msingi huu usipokuwa imara mtoto anaweza kuharibika kwa kujiunga na makundi au marafiki wabaya. Wazazi au walezi ambao wako makini wanatakubaliana nami kuwa shule ya kwanza katika maisha ya mtoto ni malezi ya nyumbani kwao. Wapo baadhi ya wazazi wanaoona ni jambo la kawaida kuona mtoto akifanya vitendo visivyofaa mbele ya jamii. Hawa ndio wale ambao hawawafundishi tabia njema na hawa pia hawaoni umuhimu wowote wa kujua marafiki wa watoto wao shuleni. Lakini pia nitoe angalizo kwamba unaweza kumfundisha mtoto wako maadili mema lakini akakutana na marafiki wabaya shuleni akabadilika na kuiga tabia chafu. Kwa maana hiyo kujua marafiki wa mtoto wako shuleni ni jambo la muhimu, haijalishi umemfundisha tabia njema kiasi gani nyumbani. Watoto ni watu wa kupenda kuiga mambo yakiwamo mabaya. Kwa hiyo mzazi ukibweteka bila kumfuatilia na kuamini kwamba mtoto wako umemfundisha maadili mema hawezi kubadilika, basi utakuwa umekosea sana.



**ALLY SULEYMAN**
**(MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SUALA la mzazi kufuatilia na kujua marafiki wa mtoto wake shuleni ni msingi sana. Asipofanya hivyo anaweza kujikuta akilia mwenyewe hapo baadaye. Hii inatokana na ukweli kwamba anapomfuatilia shuleni atagundua kila kitu kutokana na jinsi anavyomjua tabia zake na hata uwezo wake katika masomo darasani. Kama atakuwa ana uwezo mzuri darasani, anaposhuka kimasomo ni lazima mzazi ajiulize ni kwa nini na atalazimika kufuatilia zaidi ili kujua chanzo cha kufanya vibaya ili kukibaini kama ni uzembe, vikundi au marafiki wabaya na kisha atachukua hatua zinazostahili ili kumrudisha kwenye mstari. Jukumu hili ni la kila mzazi anayetambua wajibu wake wa malezi. Mtoto yeyote ni taifa la kesho, hivyo anatakiwa kuandaliwa katika maadili mema kuanzia nyumbani na kusimamiwa kwa karibu ili kuhakikisha anaendelea kuwa na tabia njema nyumbani na nje ya nyumbani kwao kama shuleni na sehemu nyingine. Pia ieleweke kwamba shule nyingi hapa nchini zimejaa wanafunzi wengi, siyo rahisi walimu kujua tabia za kila mwanafunzi, hivyo wazazi na walezi wana sehemu kubwa katika maendeleo ya watoto wao, kwani siamini kama inawezekana walimu kajua kuwa mwanafunzi fulani yuko wapi na anafanya nini au anajihusisha na vitendo vibaya ili waweze kumpa taarifa mzazi wake.



# Kortini madai ya kutorosha madini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU watatu raia wa kigeni waliokamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kutorosha dhahabu wakishirikiana na maofisa usalama wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya, kwa kesi ya uhujumu uchumi.

Waliofikishwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Venance Mlingi ni Clive Rooney (62) raia wa Ireland, Ross Chertsey (34) na Robert Charles (58) wote raia wa Uingereza.

Watatu hao walikamatwa katika uwanja wa ndege wakitaka kusafirisha dhahabu kutoka Chunya kwenda jijini Dar es Salaam.

**Kama kweli mshtakiwa anaumwa anatakiwa akatibiwe na maofisa wa magereza badala ya kwenda kutibiwa uraiani.**

Wakili wa Serikali Jacquiline Nyantori alisema watuhumiwa hao walikamatwa Julai 3, mwaka huu, wakiwa wanatorosha dhahabu yenye uzito wa gramu 1043.33 yenye thamani ya Sh. milioni 98.5.

Alisema washtakiwa hao hawakuwa na kibali cha kusafirisha wala kumiliki madini hayo kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2002.

Alivitaja vifungu ambavyo washtakiwa wanadaiwa kukiuka cha 18 (1) na namba 4 (1) (a) cha mwaka 2010 kikisomwa pamoja na aya ya 27 ya jedwali namba moja na kifungu cha 57 (1) na 60 (2).

"Upelelezi wa shauri hili umekamilika, hivyo naiomba mahakama yako iendelee kusikiliza," alidai Nyantori.

Kaimu Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, Mulingi, alisema mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza shauri hilo, hivyo akaahirisha mpaka Julai 22, mwaka huu.

Aliamuru washtakiwa warejeshwe rumande mpaka siku iliyopangwa kusikilizwa tena ya Julai 22.

Hata hivyo, Wakili wa Kujitegemea anayewatetea washtakiwa, Bonface Mwabukusi, aliiomba mahakama hiyo kumruhusu mshtakiwa namba moja kwenye kesi hiyo, Rooney, aruhusiwe kwenda kutibiwa kwa madai kuwa anaumwa.

Akijibu ombi hilo, Nyantori alidai kuwa kama kweli mshtakiwa anaumwa anatakiwa akatibiwe na maofisa wa magereza badala ya kwenda kutibiwa uraiani.

## Ushirika wapewa neno kwa viwanda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imevitaka vyama vya ushirika kuwa chachu ya maendeleo ya viwanda kwa kuweka mifumo itakayowavutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata mazao.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alitoa rai hiyo jana alipokuwa anafunga maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. Maadhimisho hayo kitaifa yalifanyika katika viwanja vya CCM Ruanda, Nzovwe jijini hapa.

Alisema endapo vyama hivyo vitavutia wawekezaji wa viwanda nchini, vitakuwa vimesaidia kuongeza ajira kwa vijana wa Kitanzania watakaokuwa wanafanya kazi kwenye viwanda pamoja na kuwachochea wakulima kuzalisha zaidi.

Aidha, Mgumba alisema viwanda vya kuchakata mazao vitasaidia kuongeza thamani ya mazao ya wakulima wa Tanzania kwa madai kuwa wataondokana na tabia ya kuuza mazao ghafi ambayo bei yake inakuwa ya chini.

"Lazima tuweke mfumo ambao utawawezesha wawekezaji wa viwanda nchini kupata malighafi za kutosha ili kuwezesha ushindani katika soko la kimataifa. Tusipofanya hivyo hawa wanapeleka ujumbe mbaya kwenye soko la kimataifa kwamba wamewekeza lakini malighafi hakuna, hivyo hata wapya wanaotamani kuja watakata tamaa," alisema Mgumba.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC), Theresia Chitumbi, alisema ushirika ni njia mojawapo ya kuimarisha uchumi kwenye jamii ndiyo maana sekta hiyo imepanua wigo wake kutoka kwenye mazao ya biashara pekee na kuingia kwenye mazao mengine.

Pia alisema sekta hiyo imejitanua zaidi na kuingia kwenye sekta za kifedha ikiwamo vyama vya akiba na mikopo kwa wakulima na wanunuzi wa mazao pamoja na wadau wote wa sekta ya ushirika.

Naye Kaimu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Tito Haule, alisema pamoja na changamoto zilizopo, ushirika Tanzania umeanza kuimarika. Alisema vyama vya ushirika sasa vinafanya kazi kubwa ikiwamo huduma za kifedha kwa wanachama wake.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Isewe, wilayani Chunya, mkoa wa Mbeya, wakiwasaidia mafundi wa kijiji kuwasogezea mawe kwa ajili ya ujenzi wa choo cha Shule ya Msingi Isewe, juzi, kinachojengwa kwa ufadhili wa Shirika la Catholic Relief Service (CRS). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mkuu wa mkoa abaini madudu ujenzi kituo cha afya

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amebaini madudu katika ujenzi wa Kituo cha Afya cha Masukulu wilayani Rungwe ikiwamo ubadhirifu wa fedha na kujengwa chini ya kiwango kwa baadhi ya miundombinu.

Akizungumza baada ya kukagua kituo hicho, Chalamila alisema tayari Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) inaendelea na uchunguzi wa mradi huo na kwamba muda wowote atakabidhiwa ripoti ya uchunguzi huo.

Alisema baada ya kupokea ripoti hiyo hatua kali zitaanza kuchukuliwa kwa wote watakaobainika kuhusika na uchakachuaji wa mradi huo ambao unatekelezwa kwa fedha za serikali.

Chalamila alisema baadhi ya vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa na kutumika kwenye ujenzi wa baadhi ya majengo ni tofauti na vilivyoainishwa kutumika kwenye ujenzi wa majengo ya serikali zikiwamo nondo na vigae.

Alisema kituo hicho ni miongoni mwa mifano michache ya vituo vya afya ambavyo vimefanywa kuwa mashamba ya bibi kwa baadhi ya watumishi wa serikali wanaochakachua na kujinufaisha wao wenyewe tofauti na malengo ya serikali.

"Nilitaka nifanye maamuzi (uamuzi) hapa hapa lakini mpaka nikasome taarifa ya Takukuru. Nitarudi tena hapa kwenye kituo hiki baada ya siku nne na kwa hali hii lazima tuwawajibishe wahusika. Mhandisi wa halmashauri hajitambui na hata msimamizi wa mradi huu hajitambui," alisema Chalamila.

Katibu Tawala Wilaya ya Rungwe, Mnkondo Bendera, alisema kilichofanywa na wasimamizi wa ujenzi wa kituo hicho ni uhuni wa wazi na kwamba wahusika hawawezi kukwepa huku akimtuhumu mkurugenzi mtendaji wa halmashauri kuwa hawezi kukwepa kitanzi hicho.

Alisema endapo baadhi ya watendaji wanaokwamisha miradi hawatakuwa wanachukuliwa hatua kali, kuna uwezekano miradi mingi ya serikali kukwama au kutekelezwa chini ya kiwango kama ilivyotokea kwenye kituo hicho.

Naye Diwani wa Masukulu, Weston Mwansasu, alisema kilichosababisha kuchelewa kwa mradi huo ni mkurugenzi mtendaji wa halmashauri kutowajibika katika nafasi yake kwa madai kuwa alichelewesha kupeleka fedha.

Alisema tangu fedha za mradi huo zifike katika ofisi ya mkurugenzi mtendaji, ni miezi mitatu imepita lakini hakuna kazi iliyokuwa inafanyika mpaka taarifa zilipotolewa kuwa Mkuu wa Mkoa atafanya ziara ndipo ujenzi ukaanza kufanyika kwa kasi.

Aidha, Mwansansu alidai kuwa alikuwa hapewi nafasi ya kuhoji kama diwani kwa madai kuwa kila akitaka kufanya hivyo alikuwa anaambiwa kuwa ni maagizo ya Mkurugenzi na kwamba hata kwenye usafirishaji wa mchanga kulikuwa na uhuni uliokuwa unafanyika.

Alisema magari yalikuwa yanabeba mchanga yalikuwa yakibeba mara moja inahesabika kuwa ni safari tatu kitu ambacho alidai kuwa ulikuwa ni wizi wa wazi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Loema Peter, alisema walipokea Sh. bilioni moja kutoka serikali kuu kwa ajili ya vituo viwili yaani Sh. milioni 500 kwa ajili ya Kituo cha Ikuti na Sh. milioni 500 kwa ajili ya Masukulu.





# CCT yaitwa kuwekeza sekta ya elimu Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JUMUIYA ya Kikristo Tanzania (CCT), imetakiwa kuwekeza katika sekta ya elimu ikiwamo kuanzisha shule za kimataifa ambazo zitawasaidia kujiinua kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, wakati wa harambee ya kitaifa ya ujenzi wa jengo la kitega uchumi la CCT iliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini hapa.

Dk. Mahenge alisema Jiji la Dodoma kwa sasa lina maeneo mengi kwa ajili ya uwekezaji, hivyo jumuiya hiyo inapaswa kuomba eneo ili kujenga shule za kimataifa.

Alisema kutokana na hilo wanapaswa kuangalia uwekezaji katika maeneo mbalimbali ambayo yamebainishwa na Jiji la Dodoma kujenga vitega uchumi vyao ambavyo vitawasaidia kuwaingizia kipato.

**CCT itaendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha amani iliyopo inaendelea kudumu, tutazidi kuliombea taifa letu.**

Alisema wao kama mkoa wanawakaribisha kuwekeza katika maeneo ambayo yatawanufaisha wao na jamii kwa ujumla kutokana na kile ambacho watakuwa wamewekeza.

Alifafanua kuwa kuna maeneo mengi ya uwekezaji ambayo CCT wanaweza kuwekeza kwa hiyo kinachotakiwa wajipange kuomba maeneo hayo ambayo nayo yatawasaidia kujikwamua kiuchumi na kuepukana na fedha za msaada ambazo zinaendelea kupungua kila siku.

Naye Mwenyekiti wa CCT, Askofu Alimikisya Cheyo, alisema wanaishukuru serikali kwa kuwa pamoja na taasisi za kidini ikiwamo kushirikiana katika mambo mbalimbali ya ujenzi wa taifa.

Askofu Cheyo alisema CCT wanaipongeza serikali katika hatua za kimaendeleo inazofanya, ikiwamo kupambana na ujangili, kupiga vita dawa za kulevya na kusisitiza kilimo chenye tija kwa wananchi.

Alisema kanisa litaendelea kuhimiza kutafuta amani na uchambuzi kupitia mazungumzo na jamii, lengo ni kuona kila mwananchi anatambua nini maana ya amani.

"CCT itaendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha amani iliyopo inaendelea kudumu, tutazidi kuliombea taifa letu," alisema Cheyo.



Mkazi wa Jiji la Dodoma, akiwa ameisheheni baiskeli yake kuni kwa ajili ya nishati ya kupikia nyumbani katika Mtaa wa Uhindini jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TLP yaeleza mikakati yake uchaguzi ujao

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

UONGOZI wa Chama cha Tanzania Labour (TLP) Mkoa wa Dodoma, umesema wanajipanga kuweka wagombea kila ngazi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Mkoa wa TLP, Justous Silungwe, wakati wa kikao cha ndani kilichofanyika jana jijini hapa.

Silungwe alisema chama hicho kinakusudia kuweka wagombea kila ngazi katika uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa pamoja na Uchaguzi Mkuu 2020.

"Ni kweli tunapenda kukiri kuwa chama chetu kililegalega lakini sasa tumeanza mikakati ya kujkijenga kuanzia ngazi ya tawi hadi taifa," alisema.

Alisema wanakusudia kusimamisha wagombea wanaotokana na chama hicho kuanzia ngazi ya vitongoji hadi vijiji katika mkoa mzima.

Aliitaja mikakati waliojiwekea kwenye kikao chao kuwa ni kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uchaguzi na kutangaza sera za chama chao ili wananchi waweze kuwapa kura katika uchaguzi huo.

Silungwe alisema wananchi hawajapewa elimu kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo chama chao wameona wajipange mapema kutangaza na kuuza sera zao.

Aliongeza mikakati mingine ni kuimarisha matawi ya chama hicho pamoja na kuingiza wanachama wapya ili waweze kutoa elimu kwa wengine.

Kwa upande wake Katibu wa Mkoa wa chama hicho, Damari Richard, alisema kwa sasa chama hicho wanaofisi katika wilaya za Bahi, Kongwa, Mpwapwa na Dodoma mjini.

Richard alisema katika kujipanga upya kwa chama hicho kitaendelea kufungua matawi maeneo mbalimbali ikiwamo vijijini.

Alisema katika uchaguzi uliopita chama hicho kilifanikiwa kunyakua baadhi ya vjiji na vitongoji, lakini hapa katikati waliondolewa kutokana na kufanyiwa figisufigisu.

Hata hivyo, alisema pamoja na hivyo chama hakijakata tamaa ndio maana wameanza mikakati mapema ya kujipanga ili kupata ushindi katika maeneo mengi.

# Sido yahimiza wajasiriamali kuwa na nembo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Dodoma, limewataka wajasiriamali kuwa na nembo ya TFDA ili kupanua soko la nje na ndani kulingana na bidhaa wanazotengeneza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Sido Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, alisema nembo ya TFDA itawasaidia kupata masoko makubwa katika bidhaa wanazouza.

Alisema wajasiriamali wakifanikiwa kuwa na nembo hizo itawasaidia kujitanua kibiashara kwa kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya kimataifa ya biashara.

"Tunawaomba wajasiriamali wajitahidi kuwa na nembo ya TFDA kwa sababu ni muhimu na inasaidia kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya kimataifa," alisema Manongi.

Alisema serikali inasisitiza suala zima la viwanda, kwa hiyo ni vema wajasiriamali wakawa na nembo hiyo ili kujitanua kibiashara.

Manongi alisema lengo la kuhimiza wajasiriamali kuwa na nembo ni kutaka kuwasaidia kuendana na kasi ya serikali ya uchumi wa viwanda.

Aidha, alifafanua kuwa biashara ambayo ina viwango vyenye ubora ni rahisi kuuzika na kupata wateja wengi kulingana na ubora katika soko au maonyesho ambayo mjasiriamali atakuwa ameenda kushiriki.

Alisema lengo lao ni kuona wafanyabiashara wote wa Jiji la Dodoma na wengine wanatengeneza bidhaa zilizobora ambazo zinaleta ushindani katika maonyesho mbalimbali wanayoshiriki.

Naye mjasiriamali, Edna Ndejembi, aliishukuru SIDO kwa mafunzo wanayotoa kwa wajasiriamali kwa sababu yanawasaidia kupiga hatua katika biashara ambazo wanafanya.

Alisema wanaiomba jamii kujitokeza katika mafunzo mbalimbali yanayotolewa na shirika hilo kwa sababu yana manufaa makubwa kutokana na serikali ya awamu ya tano inasisitiza suala zima la viwanda ili kujiinua kiuchumi.

**Lengo lao ni kuona wafanyabiashara wote wa Jiji la Dodoma na wengine wanatengeneza bidhaa zilizobora ambazo zinaleta ushindani katika maonyesho mbalimbali wanayoshiriki.**



# Balozi Seif awafunda wawekezaji wa hoteli

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewashauri wawekezaji wa hoteli katika sekta ya utalii nchini kuzingatia umuhimu wa kutoa fursa za ajira kwa wazawa.

Lengo ni kudumisha mahusiano mema katika uendelezaji wa miradi yao.

Alisema hatua hiyo itakwenda sambamba na azma ya serikali katika kufungua milango ya uwekezaji itakayohamasisha fursa zaidi za ajira hasa kwa vijana itakayosaidia kupunguza msongamano wa makundi yasiyo na kazi mitaani.

Balozi Iddi aliyasema hayo wakati wa ziara yake ya kuangalia maendeleo ya ongezeko la ujenzi wa vyumba vya kulala wageni katika Hoteli ya RIU Palace Zanzibar iliyopo Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema ongezeko kubwa la vijana wanaomaliza masomo limekuwa kubwa na kuilazimika serikali kubuni mbinu za kupambana na changamoto hiyo.

**Ongezeko la ujenzi huo utafikia vyumba 100 vya kulala wageni vinavyojengwa katika mfumo wa vyumba 50 kwa kila awamu vitakavyoiwezesha hoteli hiyo kufikia vyumba 200.**

Makamu huyo aliupongeza uongozi mzima wa hoteli hiyo kwa uamuzi wake wa kutanua mradi wao, hivyo kuongeza mapato ya taifa na kukuza fursa ya ajira.

Balozi Seif aliutaka uongozi huo kuepuka uwezekaji wa makuti kwenye majengo yao ili kujikinga na janga lolote linaloweza kusababishwa na majanga ya moto hasa wakati wa kiangazi.

Alisema ipo miradi mingi ya mahoteli iliyowahi kutumia mfumo wa makuti kwa dhana ya kuridhisha wateja wao, lakini hatima yake imepunguza uzalishaji na mengine kufungwa kabisa baada ya kupata majanga ya moto.

Naye Meneja Mkuu wa Hoteli ya RUI Palace Zanzibar, Luis Sanchez Sarda, alisema uongozi wa hoteli hiyo umelazimika kuongeza idadi ya vyumba vya kulala wageni ili kukidhi mahitaji ya wateja wao wanaoongezeka kila uchao.

Alisema ongezeko la ujenzi huo utafikia vyumba 100 vya kulala wageni vinavyojengwa katika mfumo wa vyumba 50 kwa kila awamu vitakavyoiwezesha hoteli hiyo kufikia vyumba 200.

Kwa upande wake Mkurugenzi Uwezeshaji na Miradi ya Uwekezaji kutoka Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Shariff Ali Shariff, alisema mabadiliko ya sheria ya uwekezaji yaliyofanywa na serikali hivi karibuni inaelekeza mwekezaji yeyote analazimika kuwekeza mradi wake nchini usiopungua thamani ya Dola za Kimarekani milioni 100.

Shariff alisema uamuzi huo wa mabadiliko ya sheria ya uwekezaji umezingatia umuhimu wa kuimarisha miradi ya kudumu ya uwekezaji itakayoendelea kutoa ajira kubwa, kuongeza mapato na kuimarisha uchumi wa nchi.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, akipandisha bendera ya kampeni ya uhamasishaji wa ujenzi na matumizi ya vyoo nchini inayojulikana kama 'usichukulie poa, nyumba ni choo', jijini humo jana. Kushoto kwake ni balozi wa kampeni hiyo, msanii Mrisho Mpoto. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Salma Kikwete awapa mbinu wajasiriamali

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MKE wa Rais mstaafu wa Tanzania awamu ya nne, Mama Salma Kikwete amewataka wajasiriamali nchini kuzitumia fursa za mafunzo wanazozipata ili kubuni mbinu bora za kufanyia kazi.

Akifungua mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali wa mikoa mitatu ya Unguja yaliyoandaliwa na jumuiya rafiki wa wanawake na watoto Zanzibar (Rawaza), alisema mafunzo hayo waliopatiwa ni muhimu na yataweza kuwasaidia wajasiriamali hao kutengeneza bidhaa za kitaaalamu na zenye ubora kupata kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku.

Aidha, aliwataka wajasiriamali hao kubuni bidhaa zinazokwenda na wakati ili kuuzika katika masoko, jambo ambalo litaweza kuinua uchumi wao na taifa kwa ujumla.

"Muwe na mitindo mipya itakayowasaidia kukubalika katika soko na hatimaye kuinua uchumi wa wanawake," alisema.

Aidha, aliwataka kuhakikisha fedha wanayoipata kuitumia katika kuendeleza biashara zao ili kujikomboa kiuchumi na kuondokana na hali ya utegemezi.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Magharibi, Tauhida Cassian Galos, alisema lengo la kuanzisha jumuiya hiyo ni kuwasaidia wanawake kupigania haki zao katika ngazi za maamuzi.

Alisema pia jumuiya hiyo ina dhamira ya kuwasaidia wanawake kuepukana na changamoto mbalimbali zinazowakabili ukiwamo udhalilishaji wa kijinsia.

## Mfumo mpya kurahisisha usafirishaji

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amesema kukamilika kwa mfumo mpya wa kurahisisha utoaji wa huduma za usafiri salama na uhakika unaozingatia wakati (ZAN TAXI) kutawezesha kufuatwa kwa taratibu za utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji.

Alieleza hayo wakati wa hafla maalum ya uzinduzi wa mfumo huo wa utoaji huduma za usafiri wa taxi kwa kutumia simu za mikononi.

Alisema kuanzishwa kwa mfumo huo kutapelekea kupunguza matumizi mabaya za huduma za usafiri barabarani husuani taxi, hatua ambayo kila mtoa huduma hiyo atatakiwa kusajiliwa na kutambulika kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi na kupewa ruhusa za utoaji wa huduma hiyo.

"Sio kila gari zitakazokuja kwenu itakuwa inapaswa kupewa usajili kupitia Tantaxi ni gari maalum ambazo zimesajiliwa ndizo zitapewa ruhusa maalum ya kutoa huduma hii ya taxi hapo ndio mtaisajili," alisema Ayoub.

Aliutaka uongozi wa Tantaxi kutoa elimu kwa jamii juu ya mfumo huo mpya wa utoaji huduma za usafiri wa taxi, ili uweze katambulika kwa wananchi na kuweza kutoa huduma kwa ufanisi na wakati kama ulivyokusudiwa.

"Suala la utoaji wa huduma za usafiri wa barabarani hasa taxi kupitia mfumo huu ni mpya sasa hapa suala la elimu inahitajika kwa wananchi na inahitaji utaratibu maalum kulingana na umuhimu wa huduma hii hasa kiusalama," alisema Mkuu wa Mkoa.

Aliwapongeza vijana wazawa walioamua kubuni mfumo huo mpya wa kurahisisha huduma za usafiri kwani hatua hiyo itaendelea kuimarisha usalama wa nchi kwa kuwa kila mtoa huduma hiyo ataweza kutambulika pamoja na kusaidia kukua kwa ulipaji wa kodi na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Alisema Serikali ya Mkoa itaendelea kuunga mkono kwa nguvu zake zote katika kuhakikisha mfumo huo wa utoaji huduma za usafi wa gari za taxi kwa kutumia simu za mkononi uweze kufanya kazi kwa haraka na kuwa endelevu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mfumo mpya wa kurahisisha huduma za usafiri salama na uhakika unaozingatia wakati, salama, Othman Mgaza, alisema taasisi yao inakusudia kutanua huduma zao kwa mikoa ya Tanzania Bara ikiwamo Morogoro, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Tanga na Shinyanga.

"Tunakusudia kutanua mtandao wetu kupeleka huduma hii nje ya Zanzibar tutapeleka Tanzania Bara tumeazimia zaidi mikoa ya nje ya Dar es Salaam hivi karinuni tutapeleka huduma za Tan Taxi kwa baadhi ya mikoa ya bara," alisema.

Mhandisi Mkuu wa Mfumo huo, Haji Masoud Abas, alisema dereva ambaye atakuwa mwanachama wa mfumo huo atasajili bima na ruhusa ya matumizi ya barabara pamoja na leseni ya udereva ili awekwe katika mfumo maalum atakaokuwa akitumia katika kazi zake.

# Kaya 7,000 zakosa vyoo mkoa mmoja

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

KAYA 6,945 mkoani Mwanza hazina vyoo sawa na asilimia 2.38, huku kaya 113,280 zikiwa hazina vyoo bora.

Hali hii imesababisha mkoa huo kukumbwa na mlipuko wa magonjwa ya kuharisha ambapo mpaka kufikia Juni mwaka huu, watu 55,114 wameugua.

Kati ya wagonjwa hao asilimia 74.4 ni watoto wenye umri chini ya miaka mitano, ambapo kati yao 171 walipoteza maisha na kwa mwaka 2018 wagonjwa 121,226 waliugua magonjwa ya kuharisha na wengi wao wakiwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa asilimia 70.2 ambapo kati yao watoto 835 walipozeza maisha.

**Tufahamu kuwa matumizi ya vyoo bora huchangia kupunguza uwezekano wa kusambaa kwa maambukizi ya magonjwa yatokanayo na uchafu,**

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, wakati akizindua kampeni ya uhamasishaji wa ujenzi na matumizi ya vyoo ijulikanayo kama 'usichukulie poa, nyumba ni choo' kwa mkoa wa Mwanza.

Dk. Nyimbi alisema kampeni hii ya usafi wa mazingira inalenga kuimarisha kiwango cha usafi hususani ujenzi na matumizi ya vyoo bora na unawaji mikono kwa sabuni.

"Ndugu wananchi tufahamu kuwa matumizi ya vyoo bora huchangia kupunguza uwezekano wa kusambaa kwa maambukizi ya magonjwa yatokanayo na uchafu," alisema. Dk. Nyimbi.

"Tumeamua kushirikiana na Ofisi ya Rais (Tamisemi) na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kufanya uhamasishaji wa ujenzi na matumizi ya vyoo bora kupitia msanii mkongwe Mrisho Mpoto ili kuwa chachu ya wananchi wa Mwanza kubadili fikra na mitazamo katika suala la usafi."

Aidha, alitoa wito kwa viongozi kuweka kipaumbele suala la usafi hususan ujenzi na matumizi ya vyoo katika maeneo yao ili kuepuka kutumia gharama kubwa katika kutibu magonjwa yatokanayo na hali ya uchafu.

Naye Ofisa Afya Mkoa wa Mwanza, Fungo Masalu, alisema kupitia juhudi mbalimbali zinazofanywa na mkoa kiwango cha kaya zenye vyoo kimekuwa kikiongezeka kutoka asilimia 54.57 mwaka 2015 hadi asilimia 97.61 Machi 2019.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakipata maelezo kuhusu mitambo ya kutengenezea barabara kutoka kwa Ofisa Masoko wa Kampuni ya GF Trucks & Equipment, Lukolo Juma (kulia), walipotembelea Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rita yahakiki vyeti vya kuzaliwa 92,000

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), umefanikiwa kuhakiki vyeti vya kuzaliwa 92,324 kwa kipindi cha miezi mitatu tangu kufunguliwa kwa dirisha la uhakiki kwa ajili wanafunzi wanaotegemewa kuomba Mikopo ya Elimu ya Juu nchini.

Kwa mujibu wa Meneja Masoko na Mawasiliano wa RITA, Josephat Kimaro, kati ya vyeti vilivyohakikiwa, vyeti 84,166 vimekutwa havina upungufu, vyeti 2,203 vimebainika kuwa na upungufu mbalimbali.

Alisema wahusika wametaarifiwa kwa ajili ya kurekebisha au kutafuta nyaraka zilizo sahihi na kwamba bado kuna vyeti 5,955 viaendelea kuhakikiwa.

"Lengo ni kuhakiki wanafunzi 100,000 kwa ujumla, zoezi limefanikiwa sehemu kubwa ya wanafunzi wanaotarajiwa kuomba mikopo wameshatimiza moja ya kigezo cha msingi ambacho ni kuwa na cheti kilichohakikiwa," alisema.

"Zoezi la uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa ni muhimu ili kuhakikisha wanafunzi wanaopata mikopo ni wale wanaostahili na idadi ya maombi yaliyobainika kuwa na changamoto inawezekana ikaonekana kuwa ndogo ni kutokana na wahusika kujitahidi kuwa na nyaraka halali mara wanapojua zisizo halali zitabainika katika uhakiki," alisema Kimaro.

Aliwataka wanafunzi wote watume maombi ya uhakiki na kupokea majibu kwa njia ya Mtandao kupitia anuani ya http://uhakiki.rita.go.tz/uhakiki ambapo maombi yanaweza kutumwa kutokea sehemu yoyote hivyo kuwapunguzia waombaji gharama za nauli na muda waliokuwa wautumie kwenda katika Ofisi za Rita.

Alisema programu hyo ya uhahikiki ni moja ya mageuzi yanayofanyika ndani ya wakala kwa kuongeza ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa kutumia Tehama.

Alisema changamoto zinazojitokeza ni baadhi ya wanafunzi kutokumbuka nywila za akaunti zao ambazo walitumia kutuma maombi na watakiwa kuzitumia kupokea majibu baada ya kuhakiki.

"Wanafunzi hawa wamekuwa wakisaidiwa kwa kupewa suluhisho baada ya kupiga simu ambayo ni bure au kuma ujumbe katika mitandao ya kijamii," alisema.

Alisema pia wanafunzi wengine wamekuwa wakituma nakala za vyeti zisizosomeka vizuri na kupitia akaunti zao walitaarifiwa kutuma nakala nyingine.

Aidha, alisema wale waliokutwa na vyeti ambavyo sio halali walipewa taarifa na kutakiwa kufanya maombi ya cheti halali.

# DC Kawawa awapa neno kinamama

**Na Robert Temaliilwa,** BAGAMOYO

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Kawawa, amewataka wanawake wajasiriamali kuungana kwa lengo la kuinuana kiuchumi kupitia kwenye bidhaa zao.

Mkuu huyo wa wilaya alitoa wito huo juzi wakati akizindua soko la pamoja la wanawake wajasiriamali wilayani hapa, ambalo linalenga kuwakwamua katika shughuli zao za kiuchumi.

Soko hilo la pamoja linawaunganisha wajasiriamali wanawake kutoka kata mbalimbali za Dunda, Magomeni, Zinga, Kiromo na Nianjema wilayani hapa.

Katika uzinduzi huo wajasiriamali wanawake walifika kwenye soko hilo wakiwa na bidhaa mbalimbali za ubunifu na mazao ya kilimo zikiwa kama shughuli kuu za kujiingizia kipato.

Kawawa alisema ili lengo la soko hilo la pamoja la wajasiriamali wanawake liweze kuwa na mafanikio ni kwa wanawake wote kushirikiana na kuwa kitu kimoja.

"Siri ya mafanikio kwa jambo lolote la kimaendeleo ni kwa wahusika kuungana pamoja na kuwa kitu kimoja, hivyo ili soko lenu hili liweze kuwaletea mafanikio ni nyinyi wote kushirikiana kwa pamoja na kuwa kitu kimoja," alisema Kawawa.

Pia mkuu huyo wa wilaya aliwapongeza wanawake hao kwa hatua ya kuanzisha soko hilo kwa kutumia eneo lao binafsi badala ya kuisubiri serikali kuwatafutia eneo la kuweka soko hilo.

Kawawa alisema amefarijika na hatua hiyo ya wanawake hao na kuahidi kushirikiana nao bega kwa bega kuhakikisha wanapata eneo kubwa zaidi kwa ajili ya ujenzi wa soko la pamoja na wajasiriamali hao.

Aliwataka viongozi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wilayani hapa kushirikiana nae katika kupata eneo ambalo wanaona linawafaa kulingana na shughuli zao.

"Hatuwezi kuwa na bidhaa nzuri kama hizi halafu tukakosa soko la kuuzia bidhaa nzuri kama hizi ambazo ni alama ya Bagamoyo," alisema.

ITV

JARIDA LA WANAWAKE: SAA 1:00 USIKU

LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA NEEMA MTEI MJASIRIAMALI MKULIMA NA MSINDIKAJI WA UYOGA MBICHI AMBAYE PIA NI MWALIMU WA UKULIMA WA KISASA WA UYOGA TOKA MBEZI KUNGURU JIJINI D`SALAAM AKIONYESHA NA KUFUNDISHA UTAALAM HUO.

# Iran yatangaza kuvunja mkataba wa nyuklia

**TEHERAN,** Iran

IRAN imetangaza kuvunja mkataba kuhusu kiwango cha urutubishaji wa madini ya urani uliowekwa mwaka 2015.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Abbas Araqchi, amesema Iran bado inataka kutekeleza mkataba huo, lakini ameyashutumu mataifa ya Ulaya kwa kutotimiza wajibu wao.


Marekani ilijiondoa kwenye makubaliano hayo mwaka 2018, tangu wakati huo ikaweka tena vikwazo dhidi ya Iran. Mei mwaka huu Iran iliongeza urutubishaji wa urani, ambayo inaweza kutengeneza mafuta na silaha za nyuklia.

**Iran bado inataka kutekeleza mkataba huo, lakini ameyashutumu mataifa ya Ulaya kwa kutotimiza wajibu wao.**

Araqshi amesema Iran itaanza shughuli za kurutubisha madini ya urani zaidi ya asilimia 3.6 ndani ya saa chache, kwa ajili ya vinu vyake vya umeme vya Bushehr.

Araqchi amesema Iran itaendelea kupunguza utekelezaji wake kwa mkataba wa mwaka 2015 kila baada ya siku 60, mpaka pale mataifa yote yaliyosaini mkataba- China, Ufaransa, Ujerumani, Urusi na Uingereza watakapochukua hatua ya kuilinda Iran dhidi ya vikwazo kutoka Marekani.

Tangazo hilo limetolewa siku moja baada ya Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, kuzungumza na Rais wa Iran, Hassan Rouhani, akieleza shaka yake kubwa kuhusu kitakachotokea iwapo makubaliano



yatakiukwa.

Rouhani ametoa wito kwa mataifa ya Ulaya kuchukua hatua haraka kunusuru makubaliano hayo. Lakini alisisitiza kuwa wako tayari kwa mazungumzo ya kidiplomasia, kama vikwazo vitaondolewa. **BBC**



Mbabe wa zamani wa kivita na aliyekuwa kiongozi wa Kijeshi nchini DRC, Bosco Ntaganda, ambaye jana alipatikana na hatia ya makosa dhidi ya uhalifu wa kivita katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC). **PICHA: DW**

# ICC yamtia hatiani mbabe wa kivita

**THE HAGUE,** Uholanzi

MAHAKAMA ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita ya (ICC) ya The Hague, Uholanzi, imemtia hatiani mbabe wa zamani wa kivita wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Bosco Ntaganda, kwa uhalifu dhidi ya ubinadamu na uhalifu wa kivita.

Ntaganda, ambaye alishikiliwa hana hatia wakati wa kipindi cha miaka mitatu ya kusikilizwa kwa kesi dhidi yake, anakabiliwa na kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na hatia jana.

Ntaganda hakuonyesha hisia zozote wakati jaji aliyesimamia kesi hiyo, Robet Fremr, alipopitisha hukumu hiyo. Alitiwa hatiani mara ya kwanza mwaka 2006 na kuwa ishara ya kufanya uhalifu bila hofu ya kuchukuliwa hatua kisheria katika Bara la Afrika, akihudumu kama jenerali katika Jeshi la Congo kabla kujisalimisha mwaka 2013.

Ntaganda alishtakiwa kwa kusimamia mauaji ya raia na wanajeshi wake katika eneo linalokabiliwa na machafuko na lenye utajiri wa madini la Ituri Mashariki mwa DRC mwaka 2002 na 2003.

Waendesha mashtaka walitoa taarifa za kina za kutisha za waathirika wakiwamo baadhi waliopasuliwa matumbo na koo zao, kama sehemu ya ushahidi katika kipindi cha miaka mitatu ya kusikilizwa kwa kesi yake ICC.

Aliwaambia majaji wakati wa kesi yake kwamba alikuwa mwanajeshi na wala sio mhalifu, na kwamba jina la utani la "Terminator" halimhusu. Mzaliwa huyo wa Rwanda anakabiliwa na mashtaka 13 ya uhalifu wa kivita na mashtaka matano ya uhalifu dhidi ya ubinadamu kwa jukumu lake wakati wa machafuko ya kinyama yaliyotokea Kaskazini Mashariki mwa DRC.

Mashtaka hayo yanajumuisha mauaji, ubakaji, kuwasajili watoto kama wanajeshi na kuwanyanyasa kingono, uporaji na kuwalazimisha raia kuyakimbia makazi yao. Ntaganda ameyakanusha mashtaka yote dhidi yake katika kesi inayomkabili, ambayo ilianza kusikilizwa mnamo Septemba 2015 mjini The Hague.

Waendesha mashtaka wanasema uhalifu huo ulifanyika wakati Ntaganda alipoliongoza kundi la Patriotic Forces for the Liberation of Congo, FPLC, bawa la kijeshi la chama cha Union of Congolese Patriots, katika Jimbo la Ituri, Kaskazini Mashariki mwa Congo kati ya mwaka 2002 na 2003. **DW**

## Barua pepe kuhusu Trump zachunguzwa

**WASHINGTON,** Marekani

MAMLAKA nchini Marekani zimeanza kufanya uchunguzi kuhusu barua pepe zilizovuja zilizotoka kwa Balozi wa Uingereza mjini Washington ambayo imedai kuwa utawala wa Trump si "stadi".

Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Tom Tugendhat, amesema tukio la kuvuja kwa barua pepe hizo si jambo dogo, na yeyote aliyehusika lazima ashtakiwe.

"Wanadiplomasia lazima waweze kuwasiliana katika hali ya usiri," aliiambia BBC.

Ofisi ya Mambo ya Nje imesema kuvuja kwa barua pepe Jumapili ni jambo la "ufitini" lakini hakukana kuhusu ukweli wa barua pepe hizo.

Ikulu ya Marekani haijasema lolote kuhusu kilicho kwenye barua hizo, lakini barua hizo huenda zikaleta mushkeli kwenye mahusiano kati ya Marekani na Uingereza.

Katika ujumbe wa barua pepe, Balozi wa Uingereza, Kim Darroch, amesema Ikulu ya Marekani "haiwezi kufanya kazi ipasavyo" na "imegawanyika" chini ya utawala wa Trump.

Tugendhat ameiambia BBC kuwa kitendo cha kuvuja kwa barua pepe hizo kichunguzwe, lakini alimtetea Kim na kuhoji kama kuna siku Ikulu ya Marekani "itakuwa na uwezo".

Tofauti kati ya Marekani na Uingereza kuhusu mabadiliko ya tabianchi, uhuru wa vyombo vya habari, na hukumu ya kifo, ni vitu vitakavyojitokeza wakati nchi hizo zikitafuta kuimarisha mahusiano ya biashara baada ya Brexit, barua pepe hizo zimeeleza. **BBC.**

## Mhafidhina ashinda Ugiriki

**ATHENS,** Ugiriki

KIONGOZI wa upinzani wa chama cha kihafidhina nchini Ugiriki, Kyriakos Mitsotakis, ameshinda uchaguzi wa ubunge uliofanyika Jumapili ambao umetoa pigo kwa Waziri Mkuu, Alexis Tsipras, aliyeiongoza Ugiriki kwa miaka minne wakati wa mzozo mkubwa wa kifedha.

Chama cha New Democracy cha mwanasiasa Mitsotakis kimepata asilimia 39.8 ya kura ikilinganishwa na asilimia 31.5 za chama cha mrengo wa kushoto cha Syriza cha Waziri Mkuu, Tsipras. Mitsotakis, ambaye atakuwa waziri mkuu ajaye, ameahidi kupunguza kiwango cha kodi, kuvutia uwekezaji na kubuni nafasi zaidi za kazi.

Kwenye uchaguzi huo, chama cha mrengo mkali wa kulia cha Golden Dawn ambacho kiliundwa na wanazi mamboleo, kimeshindwa kurejea bungeni katika matokeo yanayoashiria kupotea uungwaji mkono wa chama hicho kilichokuwa cha tatu kwa ukubwa katika Bunge la Ugiriki.

Matokeo ya uchaguzi huo yameonyesha kuwa wapigakura wa Ugiriki wamekataa mwenendo wa raia barani Ulaya wa kuvichagua vyama vya siasa za mrengo mkali na zile zinazopinga Umoja wa Ulaya. **DW**

# Vyakula vyapaisha mfumuko wa bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUONGEZEKA kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula kwa kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2019, kumechangia kupanda kwa mfumuko wa bei wa taifa hadi asilimia 3.7.

Bidhaa zilizochangia ongezeko hilo ni pamoja na unga wa mahindi, ngano, mtama, samaki wabichi, dagaa, mafuta ya kupikia, maharage, mihogo, viazi mviringo, dizeli, petroli, gharama za nyumba za wageni na vitabu vya shule.

Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Daniel Masolwa, alisema mfumuko huo umeongezeka kutoka asilimia 3.5 kwa mwaka ulioishia Mei, 2019.

"Hii inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Juni, 2019 imeongezeka ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Mei, 2019," alisema.

Alifafanua kuwa kuongezeka kwa mfumuko huo kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula. Alizitaja bidhaa hizo na asilimia kwenye mabano kuwa ni unga wa mahindi (3.6), ngano (4.4), mtama (4.9), samaki wabichi (27.3), dagaa (16.50), mafuta ya kupikia (9.5), maharage (tatu), mihogo (16.6) na viazi mviringo asilimia 18.8.

Kwa upande wa bidhaa zisizo za vyakula ni dizeli (11.4), petroli (4.9), gharama za kulala kwenye nyumba za wageni (5.8) na vitabu vya shule asilimia 2.4.

"Mfumuko wa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Juni, 2019 umeongezeka hadi asilimia 2.3 kutoka asilimia 2.2 kwa mwaka ulioishia Mei, 2019," alisema.

Akizungumzia kuhusu fahirisi za bei, mkurugenzi huyo alisema fahirisi za bei kati ya mwezi Mei na Juni, mwaka 2019 zimepungua kwa asilimia 0.2 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 0.4 kati ya Aprili na Mei, mwaka huu.

"Fahirisi za bei zimepungua hadi 117.03 Juni kutoka 117.23 kwa mwezi Mei 2019," alisema.

Mshana alisema kupungua kwa fahirisi kumechangiwa na kushuka kwa bei ya bidhaa zisizo za vyakula ikiwamo gesi ya kupikia kwa asilimia 2.1, mkaa kwa asilimia 2.8, simu za viganjani kwa asilimia 3.7, mabegi ya mkononi ya wanawake kwa asilimia 0.5 na mavazi kwa asilimia 0.2.

Kadhalika, alisema mfumuko wa bei kwa nchi ya Uganda umeongezeka hadi asilimia 3.4 kutoka 3.3 kwa kipindi hicho, huku Kenya pia umeongezeka hadi asilimia 5.70 kutoka 5.49.




Ofisa Masoko na Mauzo Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania, Peter Mobe (kulia), akitoa maelezo kwa wananchi waliotembela kujua kazi ya bodi hiyo, katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ajali ilivyofupisha uhai watumishi Azam

INATOKA UK. 8

Naye Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, kupitia ukurasa wake wa twitter, aliandika: "Moyo wangu umeshuka na unatoa machozi ya damu kupata taarifa za kushtua na kusikitisha za ajali ya wafanyakazi Azam Media iliyotokea na kuchukua maisha ya watu saba kati ya 10 waliokuwapo."

Kwa upande wake, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, kupitia ukurasa wake wa Instagram alisema: "Nimepokea kwa huzuni vifo vya wafanyakazi watano wa Azam Media wakiwa miongoni mwa watu saba waliofariki katika ajali wakienda Geita kikazi. Serikali inatoa pole kwa Azam na ndugu wote. Tunawaombea nafuu ya haraka majeruhi na pumziko la amani na milele marehemu wote."

**TASNIA YA HABARI**

Nalo Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) lilituma salamu za rambirambi kwa uongozi wa Azam Media kwa kuondokewa na wafanyakazi wake watano.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa TEF, Nevile Meena, ilisema: "Tumehuzunishwa, kusikitishwa na kuumizwa na msiba huu kwani tasnia imepoteza wafanyakazi, wanataaluma mahiri kwa ajali. Imeacha simanzi kubwa kwa tasnia na wanahabari kwa ujumla."

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Rose Reuben, alisema wanasikitishwa na ajali hiyo iliyopoteza maisha ya watu saba.

"Msiba huu ni mkubwa kwa tasnia ya habari, Tanzania. Tamwa inaungana Watanzania kuwapa pole Azam Media Group. Vifo hivi vimeacha pengo kubwa kwa wanatasnia ya habari kwa sababu wamefariki dunia wakitimiza majukumu yao," alisema Mkurugenzi huyo katika taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Kwa upande wake, Baraza la Habari Tanzania (MCT) lilisema limepokea kwa mshtuko na simanzi kubwa taarifa ya vifo hivyo kutoa pole kwa uongozi wa Azam Media kwa kupoteza wafanyakazi wake watano.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania, Kajubi Mukajanga, alisema; "Tunachukua fursa hii kutoa pole za dhati na rambirambi zetu kwa kampuni, uongozi na wafanyakazi wote wa Azam kwa kufikwa na msiba huo mzito. Tunatoa pia pole na rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa za wafanyakazi waliofariki dunia. Tunawaombea Mungu awape wepesi katika kipindi hiki kigumu."

**VYAMA VYA SIASA**

Vyama vya siasa navyo vilituma salamu za rambirambi kutokana na msiba huo kikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho Katibu wa Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, kupitia ukurasa wake wa Twitter aliandika:

"Uongozi wa CCM umepokea kwa mshtuko na masikitiko taarifa za ajali iliyogharimu maisha ya watu saba wakiwamo wanahabari wa kituo cha Azam Media. Tunatoa pole kwa wafiwa na familia kwa ujumla. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina."

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari, kilielezea kushtushwa na tukio hilo na kutoa pole kwa tasnia ya habari nchini, familia, ndugu, jamaa na marafiki walioguswa na msiba huo.

"Wakati tunawaombea marehemu wapate pumziko la amani, tunawaombea na majeruhi uponyaji wa haraka warejee katika siha njema," alisema Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene.

# NEMC yafafanua kelele, mitetemo chafuzi

**Na Enock Charles**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetoa ufafanuzi kuhusu kelele na mitetemo chafuzi zinazotoka kwenye kumbi za starehe, baa na nyumba za ibada kwa mujibu wa kanuni na sheria ya mazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza halina mgogoro wowote na taasisi za kidini wala wamiliki wa kumbi za starehe na baa zaidi ya kutekelezaji wa sheria ya mazingira na kanuni zake.

"Kumekuwa na upotoshaji mkubwa wa taarifa ambayo ilitolewa awali na NEMC juu ya udhibiti kelele na mitetemo chafuzi kwa lengo la kulinda mazingira," alisema na kuongeza kuwa taarifa iliyotolewa na b baraza tofauti na ile iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamiii.

Kwa mujibu wa Dk. Gwamaka, taasisi za dini na wamiliki wa kumbi za starehe na baa ni wadau muhimu wa baraza na hivyo haina budi kukumbushana pale panakuwa na ukiukwaji wa kanuni na sheria.

"Tunafanya kazi kwa karibu sana na wadau mbalimbali wa mazingira zikiwamo taasisi za dini na wamiliki wa kumbi za starehe na baa, lakini mambo yanapokuwa kinyume na utaratibu basi ni jukumu letu kutoa ufafanuzi wa namna mambo yanavyotakiwa kwenda," alisema Dk. Gwamaka.

Dk. Gwamaka alitaja viwango vya sauti vinavyoruhusiwa kulingana na sheria na kanuni za baraza hilo kwa mtu au taasisi yoyote inayotaka kuanzisha huduma za baa, kumbi za starehe na shughuli za kidini katika maeneo ya watu.

"Sauti hupimwa kwa disibeli ambapo kwa nyakati za mchana kwa watoa huduma za dini haitakiwi kuzidi desibeli 60 na usiku desibeli 40, maeneo ya sokoni isizidi desibeli 75 na usiku desibeli 50 na viwandani ni desibeli 85 kwa mchana na 65 kwa usiku ili isiweza kuathiri wakazi wa eneo husika," alifafanua.

Aliwataka wananchi kuomba vibali kwa Mkurugenzi wa Baraza panapokuwa na kongamano au mikesha mbalimbali ambapo gharama zake ni shilingi milioni tano na baraza likijiridhisha litatoa kibali hicho.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALBERT FUNGAMTAMA SIYAME** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T. 508 BVD.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KW/RB/4432/2019.**

115312902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI


**EDWARD A.SYADALA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 173 CYU RANGI YA BLUE.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI **MBE/RB/111572/2019.**

115313802

## CHETI KIMEPOTEA




**TAIFA MWAISWELO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.219/124 kilichotolewa na SONGEA GIRLS SEKONDARI mwaka 1984.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: IGU/RB/1373/2016.**

115313602

## CHETI KIMEPOTEA




**LAURENT DAMAS MUMWI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.1141/0652** kilichotolewa na SWILLA SEKONDARI mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/KIG/RB/37670/2019.**

115313402

## VYETI VIMEPOTEA



**SUBIRA MASHAURI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0345-0256** kilichotolewa na **USAGARA SEKONDARI** mwaka 1995. Cheti cha kidato sita chenye **index namba S0345-0590** kilichotolewa na USAGARA SEKONDARI mwaka 1998. Cheti cha Chuo Kikuu kilichotolewa na CHUO KIKUU DAR ES SALAAM mwaka 2004.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: KJN/RB/8436/2018.**

115313602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 08/07/2019.


## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO **tarehe 10/07/2019** kampuni ya **TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka SAKINA kuelekea MURIET na kutoka MURIET kuelekea SAKINA gari hilo lenye namba za usajili: **T155BJM/ T916DCG.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu-mita 17.50**
   **Upana –mita 3.28**
   **Kimo – mita 4.60**
3. Njia itakayotumika **SAKINA** hadi **MURIET kupitia MBAUDA na kurudi SAKINA kupitia MBAUDA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115314302

## CHETI KIMEPOTEA




**ANANGE A. AME** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0194/0057** kilichotolewa na **FARAJA SEMINARY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/MBA/RB/113889/2019.

115314201

## CHETI KIMEPOTEA




**ANANGE A. AME** anatangaza kupotelewa na cheti cha JESHI kilichotolewa na 823 KJ MSANGE JKT mwaka 2014.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/MBA/RB/113902/2019.**

115314201

## CHETI KIMEPOTEA



**ANANGE A. AME** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuzaliwa kilichotolewa mwaka 1999.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/MBA/RB/I/3878/2019.**

115314201


KWA MATANGAZO MADOGO MADOGO TUPIGIE

***0767 223311***

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ALGERIA, MADAGASCAR ZATAKATA AFCON



**CAIRO,** Misri

TIMU ya Soka ya Taifa ya Algeria maarufu Les Fennecs imefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019) baada ya kuifunga Guinea's mabao 3-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa 30th June juzi usiku.

Kwa ushindi huo, Algeria sasa inasubiri kujua itakutana kati ya Ivory Coast au Mali, ambao walitarajiwa kucheza mechi ya hatua ya 16 bora jana usiku.

Youcef Bellaili alifunga bao la kwanza la timu hiyo kutoka Afrika Kaskazini na kwenda mapumziko wakiwa mbele kwa bao 1-0.

Kipindi cha pili kilianza kwa kazi na straika wa Algeria, Riyad Mahrez alifunga bao la pili pamoja na nyota Adam Ounas aliyeingia akitokea benchi alikamilisha idadi hiyo ya magoli.

Algeria itashuka tena dimbani kwa ajili ya mechi ya hatua ya robo fainali itakayochezwa keshokutwa mjini Suez.

Katika mechi ya mapema jana, Madagascar waliendelea kufanya vema katika mashindano hayo baada ya kuwaondoa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kwa penalti 4-2.

Timu hizo zilimaliza dakika 120 zikiwa sare ya mabao 2-2 na hivyo kulazimika kufika hatua hiyo ya matuta.

# Man City yajitoa mbio za kumsajili Maguire

**MANCHESTER,** England

MATUMAINI ya Manchester United kumsajili beki wa kimataifa wa England, Harry Maguire yameripotiwa kuimarika zaidi baada ya wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City kukataa kufikia beki wanayoitaka Leicester.

Maguire amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa mabeki bora wa kati kwenye Ligi Kuu England baada ya kuwa na misimu miwili bora zaidi pale katika dimba la King Power.

Kocha Pep Guardiola aliripotiwa kwamba alikuwa akimwania kwa udi na uvumba beki huyo mwenye umri wa miaka 26, lakini kwa mujibu wa gazeti la The Sun, City wamejiondoa kwenye mbio za kumwinda mchezaji huyo ambaye bei yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 85.

Sasa inasubiriwa kuona kama United watakuwa tayari kulipa kiasi hicho ambacho Leicester wanakitaka, kwani hata mpango wao wa kutaka kutoa pauni milioni 70 pomoja na kuwapa Marcos Rojo ulikataliwa wiki iliyopita.

Lakini Old Trafford kwa sasa ndio wanaonekana wenye nafasi kubwa zaidi ya kumpata Maguire kama akiamua kuondoka pale kabla ya kuanza kwa msimu mpya mwezi ujao.

Maguire yupo kwenye mkataba hadi mwaka 2023 na Leicester wanajulikana kwamba wapo vizuri mno kwenye msimamo wa bei ya kuuza wachezaji wao.




# Rooney amtaka Sancho asiondoke Dortmund




**LONDON,** England

WAYNE Rooney amemshauri, Jadon Sancho kubakia kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ili kuendelea kuimarika na Borussia Dortmund.

Sancho aling'ara msimu uliopita kwenye Ligi ya Ujerumani, na kutajwa kama mmoja wa vijana chipukuzi wenye kipaji cha hali ya juu watakaong'ara zaidi Ulaya siku za usoni.

Kiwango chake ndio kinachangia klabu ya Manchester United kutaka kumsajili ili kuimarisha kikosi chao.

Lakini gwiji wa United, Rooney ambaye ndiye mfungaji wa wakati wote wa mashetani wekundu amemshauri nyota huyo mwenye umri wa miaka 19, Sancho kubakia pale Dortmund, ambako ana uhakika atapata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

"Dortmund ni klabu kubwa na yenye mashabiki wazuri, na wanawaamini wachezaji wao vijana na hata ukiangalia Sancho amekuwa na wakati mzuri zaidi kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita," amesema Rooney akinukuliwa na gazeti la Bild.

"Kwa sasa Jadon anatakiwa kufikiria mwenyewe kama atapata nafasi ya kucheza mara nyingi zaidi kama anavyopata hivi sasa pale Dortmund.

"Kucheza ni muhimu zaidi kwa wachezaji vijana kama Jadon, hivyo wakipata nafasi nyingi zaidi ya kucheza mara kwa mara kama ilivyo pale Dortmund, basi anatakiwa kubakia kule kule."

Sancho alifunga mabao 13 na kutengeneza pasi za mwisho 19 kwenye mashindano yote kwa miamba hao wa Bundesliga ambao walishika nafasi ya pili msimu uliopita.

## HABARI MICHEZO

# Gerrard akataa kuinoa Newcastle

**LONDON,** England

STEVEN Gerrard amekataa ofa ya Mike Ashley kuchukua mikoba ya kuinoa klabu ya Newcastle.

Gerrard ambaye kwa sasa ni kocha wa Klabu ya Rangers ya nchini Scotland amekataa nafasi ya kutua pale katika dimba la St. James' Park kurithi mikoba ya Rafael Benitez.

Gerrard na Patrick Viera ndio yalikuwa majina makubwa yakitaja kupewa nafasi ya kuinoa Newcastle, lakini gwiji huyo wa Liverpool ameikataa nafasi hiyo kwa mujibu wa gazeti la Mirror.

Ashley alielewa kwamba, nafasi ya kumshawishi Gerrard kuchukua nafasi hiyo ilikuwa finyu, lakini aliamua kujaribu kutupa ndoano yake.

Gerrard mwenye umri wa miaka 39 anataka kwanza kujiimarisha na klabu yake ya Rangers na kuifanya irudi katika ubora wake baada ya sasa kupikuliwa na Celtic katika ufalme wa soka la Scotland.

Tayari amekuwa na kikosi hicho kinachojiandaa na maandalizi ya msimu mpya na wakijiandaa kucheza michuano ya Ligi ya Europa.

Inaonyesha pia Ashley hatakuwa na ushawishi mkubwa wa kumtaka Viera, ambaye kwa sasa anainoa klabu ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Nice.

Sheikh Khaled bin Zayed Al Nehayan ameripotiwa kwamba yupo kwenye mipango ya kuinunua Newcastle, lakini taarifa zake zimekuwa na sintofahamu nyingi.





# KOCHA WA BRAZIL AMPA SOMO MESSI

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

KOCHA wa Brazil, Tite, amemshutumu, Lionel Messi kwa kuwalalamikia waamuzi kwenye michuano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America.

Brazil iliifunga Argentina mabao 2-0 kwenye nusu fainali ya michuano hiyo na ilitwaa taji hilo juzi Jumapili kwa kuifunga Peru mabao 3-1, ikiwa ni mara ya kwanza kushinda Copa America tangu mwaka 2007.

"Anatakiwa kukubali na anahitaji kukubali matokeo wakati anapofungwa," amesema Tite, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Messi hakuhudhuria sherehe ya kuvalishwa medali baada ya Argentina kushika nafasi ya tatu kwa kuifunga Chile kwenye mchezo wao wa Jumamosi.

Messi alisema hakuhudhuria kwa sababu alikuwa akipinga rushwa kwa waamuzi kwenye Copa America.

Messi na Gary Medel wa Chile walitolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya kupigana vichwa katika kipindi cha kwanza cha mchezo wao.

Na mara baada ya mchezo huo, Messi alisema Argentina hawakutendewa haki na akadokeza walikuwa wamepanga kuinufaisha Brazil ibebe kombe hilo.

Aidha, Tite amesema kwamba, hafikirii kama Messi alitakiwa kutolewa nje kwenye mchezo dhidi ya Chile, na kwamba kadi ya njano tu ingetosha.

"Unatakiwa kuwa angalau na heshima kidogo na kuwa mwangalifu," alisema Tite. "Tulicheza vizuri dhidi ya Argentina. Messi hakupaswa kutolewa nje kwa kadi nyekundu dhidi ya Chile. Alitakiwa kupewa kadi ya njano. Lakini kuwa mwangalifu."

# Ndombele: Pochettino alinivutia kutua Spurs

**LONDON,** England

TANGUY Ndombele amebainisha kwamba, uwezo na ubora wa kocha, Mauricio Pochettino ndio ulimshawishi yeye kujiunga na Tottenham kwa ada iliyoweka rekodi.

Spurs walimsajili kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22 kwa ada ya pauni milioni 63 ambayo ni rekodi ya klabu hiyo. Nyota huyo wa zamani wa Lyon alikuwa akiwaniwa na klabu kubwa Ulaya zikiwamo Juventus na Paris Saint-Germain katika kipindi hiki cha majira ya joto.

Alisema: "Kilichonifanya niamue kuja kwenye Ligi Kuu England, ni kwa sababu ya kocha wao bora, ambaye naamini atanisaidia mimi kuimarika zaidi kiuchezaji.

"Tottenham wana mmoja wa makocha bora kabisa duniani. Ukweli ni kwamba akikutaka, inakufanya ujisikie kuwa na bahati kufanya nae kazi. Yeye ndiye aliyechangia mimi kuchukua uamuzi huu wa kuja hapa.

"Ni ngumu kuelezea, lakini anajua namna ya kuwa karibu na watu na nina amini hapa nitakuwa na wakati mzuri zaidi wa kuimarisha kipaji changu cha uchezaji. "Ni kocha ambaye anakuhamasisha kufanya nae kazi na kama nilivyosema yeye ndio amekuwa hamasa kubwa kwa mimi kujiunga na timu hii."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN UNITED YAJITOSA KWA MILINKOVIC-SAVIC

## Ni katika mchakato wa kuziba nafasi itakayoachwa na Pogba...

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa inataka kumsajili Sergej Milinkovic-Savic kama ndio mrithi wa kiungo anayetaka kuondoka, Paul Pogba (26).

**Majaliwa ya Pogba pale kwenye dimba la Old Trafford yapo shakani baada ya matamshi ya wakala wake, Mino Raiola, ambaye amebainisha wazi kuwa Mfaransa huyo anataka kuondoka klabuni hapo.**

United walikuwa hawana mpango wa kumuuza mchezaji wao huyo waliyemsajili kwa ada iliyoweka rekodi, lakini hali ilivyo kwa sasa, wanaonekana ni kama wamebadilisha uamuzi wao, kwa mujibu wa gazeti la Marca la Hispania.

Pogba alithibitishwa kuwa atakuwapo kwenye kikosi cha United kilichoondoka juzi Jumapili kwenda kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England nchini Australia, lakini wanaendelea kumtafuta mrithi wake.

Gazeti la Marca liliandika kuwa nyota huyo wa Lazio, Milinkovic-Savic ndio chaguo lao la kwanza la United kurithi mikoba ya Pogba ambaye pia anawaniwa na Juventus na Napoli.

Lakini klabu hiyo inaweza kukumbwa na kikwazo cha bei kutokana na ukweli kwamba miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, wameshabainisha kuwa wanataka wapewa euro milioni 120 ili kumwachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia.

Pogba ambaye alianza kuonyesha dalili za kuondoka United wakati timu hiyo ikiwa chini ya Jose Mourinho, ilionekana kama atabadili mawazo baada ya Mreno huyo kutimuliwa klabuni hapo tangu Desemba mwaka jana.

Mfaransa huyo alirejea katika kiwango chake chini ya Kocha Mholanzi Ole Gunnar Solskjaer, lakini baada ya United kukosa nafasi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, kiungo huyo pamoja na nyota wengine walionyesha dalili za kutotaka kubakia Old Trafford.

## ZISIKUPITE

### JUVE KUMNG'OA POGBA

JUVENTUS inajipanga kutoa kiasi cha pauni milioni 120 kwa Manchester United ili kuhakikisha inamsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Times - subscription required)***

### GERRARD ATAKIWA NEWCASTLE

MMILIKI wa Newcastle, Mike Ashley ameanza kumshawishi Kocha wa Rangers na kiungo wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard kuhusu kutua klabuni hapo ili kuwanoa wachezaji wa timu hiyo. ***(Mirror)***

### KLOPP AITAMANI UJERUMANI

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema siku moja anatamani kuifundisha Timu ya Taifa ya Ujerumani, taarifa kutoka kwa wakala wale imeeleza. ***(Welt - in German)***

### BARCA YAIPIKU PSG

BARCELONA imefanikiwa kuizidi kete Paris St-Germain kupata saini ya straika chipukizi raia wa England mwenye umri wa miaka 16, Louie Barry baada ya mkataba wake na West Brom kumalizika. ***(Sun)***

### SPURS, DAVIES SAFI

MABOSI wa Tottenham wako katika hatua za mwisho za mazungumzo ya kukamilisha kumpa mkataba mpya wa muda mrefu beki wa Timu ya Taifa ya Wales, Ben Davies (26). ***(Telegraph)***

### MAUPAY KUWEKA REKODI

MSHAMBULIAJI wa Brentford, Neal Maupay (22) anatarajia kutua Sheffield United na usajili wa Mfaransa huyo ambao umetajwa kuwa ni pauni milioni 22 utaweka rekodi mpya kwa timu hiyo iliyopanda daraja kucheza Ligi Kuu England msimu ujao. ***(Sun)***

### ARSENAL, NAPOLI VITANI

BEKI wa Celtic na Timu ya Taifa ya Scotland, Kieran Tierney, ametajwa kuwindwa na Arsenal pamoja na Napoli, huku klabu hiyo ya Italia ikiwa tayari kumuuza beki wake wa kushoto Mreno, Mario Rui ili kupata fedha za kumnunua nyota huyo wa Celtic. ***(Telegraph)***

### BURNLEY YAIMARISHA UKUTA

BURNLEY iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kumsajili beki wa Stoke City ambaye ni raia wa Uholanzi, Erik Pieters (30). ***(Mail)***

### JAMES KUTUA PALACE

CRYSTAL Palace imeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa Chelsea, Reece James (19), ili kuziba nafasi iliyoachwa na raia mwenzake wa England, Aaron Wan-Bissaka ambaye amejiunga na Manchester United. ***(Sun)***

### ROONEY AMSHAURI SANCHO

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (19), anatakiwa kusitisha mchakato wake wa kujiunga na Manchester United badala yake kubakia Borussia Dortmund, amesema straika wa zamani wa Old Trafford, Wayne Rooney. ***(Bild - in German)***

### MURIC KUONDOKA CITY

KLABU ya Nottingham Forest inatarajia kukamilisha mchakato wa kumsajili golikipa wa Manchester City ambaye ni raia wa Kosovo, Aro Muric (20), ndani ya siku chache. ***(Telegraph)***

## Watatu Makongo kuchuana Arusha

**Na Shufaa Lyimo**

WANARIADHA kutoka katika Shule ya Sekondari Makongo jijini Dar es Salaam wamechaguliwa kwenda kushiriki katika mashindano ya Shule za Sekondari Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika Agosti 10 mwaka huu huko Arusha.

Kocha Mkuu wa timu ya Makongo, Erick Magesa, alisema wachezaji hao wamepata nafasi hiyo baada ya kufanya vizuri katika mashindano ya Umiseta.

Magesa aliwataja wachezaji hao ambao watakwenda kuiwakilisha Makongo katika mashindano hayo kuwa ni pamoja na Ismail Tofil, Samuad Hamza pamoja na Veronica Paul. Kocha huyo alisema maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri na kudai kila mchezaji ana afya nzuri na anatarajia watarejea na medali.

"Maandalizi yetu yanaendelea vizuri, kila mchezaji ameahidi kwenda kuitangaza vema Makongo," alisema kocha huyo.

Aliwataka wadau wa mchezo huo kujitokeza kwa lengo la kuinua vipaji vya wachezaji chipukizi na kuwasaidia kupata viwanja vya kufanyia mazoezi, changamoto ambayo imekuwa ikiwasumbua wanamichezo mbalimbali.

## Yosso Mwanza waipania Ilala

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya Mkoa wa Mwanza, Abel Simba, amesema kuwa kikosi chake kimejipanga vizuri kuhakikisha kinapata matokeo mazuri katika mchezo wake dhidi ya yosso wenzao wa Ilala.

Timu hizo zinakutana katika mchezo wa hatua ya robo fainali ambao utachezwa leo kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Simba, alisema kuwa amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi zilizopita na anaamini wataendelea na kasi ile ile ili waweze kutimiza ndoto zao.

Simba alisema kuwa wamekuja jijini kwa lengo moja la kutwaa ubingwa wa mashindano hayo na wanaheshimu kila timu wanayokutana nayo.

"Kila mchezaji ameahidi kufanya vizuri katika mchezo wetu wa kesho (leo), malengo tuliyonayo ni kufika nusu fainali , fainali na hatimaye kubeba kikombe ili tuweze kuutangaza vema mkoa wetu," alisema Simba.

Kocha huyo amelishukuru Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kuandaa mashindano hayo ambayo yamewapa uzoefu wachezaji wengi ambao baadhi yao walikuwa hawajawahi kusafiri kwenda nje ya Mwanza kucheza mechi za kimashindano.

# KLABU Z'BAR ZATAKIWA KUREKEBISHA KATIBA ZAO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limevitaka vilabu vyote vya mchezo huo visiwani hapa kuhakikisha zinafanya marekebisho katika katiba zao, imefahamika.

**Kiongozi huyo alitoa maelekezo hayo katika uchaguzi mkuu wa klabu ya Kilimani City ambao ulifanyika juzi kwa Khamis Shaali Chum kufanikiwa kutetea nafasi yake ya uenyekiti kwa kipindi kingine.**

Akizungumza katika mkutano huo, Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu, alisema kwamba klabu zote zinatakiwa kuwa na katiba zinazoendana na shirikisho hilo ili kuruhusu kuanza kwa mchakato wa uchaguzi.

Pandu alisema chini ya utawala wake anahitaji kuona klabu zinafuata taratibu na kuacha tabia ya kuchagua viongozi bila ya kufuata maelekezo yaliyoko kwenye katiba ya klabu husika.

Alisema kuwa klabu kufanya uchaguzi ni jambo la lazima na si hiari, hivyo kila klabu ambayo inatambua inaongozwa na viongozi ambao hawakuchaguliwa kwa kufuata katiba, wahakikishe wanatekeleza jukumu hilo.

"Wakati naingia madarakani nilisema utawala wangu utakuwa ni wakufuata katiba na sheria, hivyo niwaombe vilabu mfanye uchaguzi ili mzidi kuviimarisha vilabu vyenu kuanzia ngazi za uongozi hadi timu zenyewe," alisema Pandu.

Aliwataka wanachama wa klabu zote zinazotambulika kisheria kufanya mikutano pamoja na kushiriki kuchagua viongozi kama katiba zao zinavyowaelekeza.

Katika uchaguzi wa klabu ya Kilimani City, Chum alishinda nafasi ya uenyekiti kwa kupata kura 36 dhidi ya 11 ambazo aliambulia mpinzani wake, Daruashi Khamis wakati Daud Mohamed aliyepata kura 36 aliibuka mshindi wa nafasi ya Makamu wa Rais dhidi ya Hassan Chau aliyepata kura 12.

Nafasi ya ya Katibu Mkuu ilichukuliwa na Abdulrahman Salum aliyepata kura zote 48, Fadhil Omar alichaguliwa kuwa Mweka Hazina baada ya kupata kura 46 baada ya kura mbili kuharibika na Aziz Idd akiibuka kuwa Mweka Hazina Msaidizi.




Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Marekani wakiwa na kikombe chao baada ya kutwaa Kombe la Dunia la Wanawake. Marekani ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Uholanzi katika mchezo wa fainali uliochezwa juzi. **PICHA: MTANDAO**

# *Azam FC, KCCA hapatoshi Kagame*

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi, Azam FC wanatarajia kukutana na KCCA kutoka Uganda katika mchezo wa Kundi B wa mashindano ya Kombe la Kagame utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Huye ulioko nje kidogo ya mji wa Kigali, Rwanda.

Azam FC ilianza mashindano hayo kwa kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mukura FC, wakati KCCA yenyewe ilitoka sare ya goli 1-1 na Bandari ya Kenya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Ettiene Ndayiragije, amesema kuwa, wamejiandaa kupambana katika mchezo huo baada ya kuwasoma wapinzani wao ambao wanacheza kwa soka la kasi.

Ndayiragije alisema ana imani na kikosi chake kuwa kitafanya vema kwenye michuano hiyo ambayo inashirikisha timu kutoka kwenye nchi za Afrika Mashariki na Kati, pamoja na nyingine tatu, za nje ya ukanda huo.

"Tutatumia nguvu nyingi kupata ushindi kwani kazi yetu ni kutetea ubingwa, bado wachezaji wana spidi ndogo nadhani ni ugeni ila hamna namna kwa kuwa tunatetea kombe ni lazima tupambane kufanya vizuri.

Kocha huyo wa zamani wa KMC FC aliwataka mashabiki wa Azam kuendelea kuwapa ushirikiano na kuwakumbusha kwamba hakuna mashindano mepesi.

"Mashabiki waendelee kutupa sapoti kwani michuano hii sio rahisi kama ambavyo wengi wanafikiria," alisema kocha huyo.

# Michezo

Jumanne Julai 9, 2019

Nipashe



Man Utd yajitosa kwa Milinkovic-Savic

UKURASA 30



Kikosi cha Timu ya Taifa ya Brazil kikiwa na kombe lao la ubingwa wa mashindano ya Copa America baada ya kuwafunga Peru mabao 3-1 katika mchezo wa fainali ya michuano hiyo, uliochezwa kwenye Uwanja wa Maracana juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

## Mrithi wa Amunike kutajwa Alhamisi

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), Alhamisi litamtangaza kocha mpya atakayechukua mikoba iliyoachwa na Mnigeria Emmanuel Ammunike, ya kuifundisha Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars).

Nipashe liliandika taarifa za Amunike kutimuliwa katika gazeti lake la jana, licha ya viongozi wa TFF kutopatikana kuthibitisha habari hiyo iliyokuwa imesambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii.

TFF ilitangaza rasmi jana kuachana na Amunike, nyota huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Nigeria (Super Eagles).

Taarifa ya TFF ilitolewa jana ilisema:- Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na Kocha wa Timu ya Taifa "Taifa Stars" Emmanuel Amunike, tumefikia makubaliano ya pamoja kusitisha mkataba baina yetu.

Shirikisho hilo lilisema kuwa litatangaza mapema kocha wa muda ambaye atakiongoza kikosi cha Stars ambacho kitaanza maandalizi ya mchezo wake wa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Katika mashindano hayo, Stars imepangwa kuanza na majirani zao Harambee Stars ya Kenya, ambayo walikuwa kundi moja katika Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019), lakini wote walitolewa katika hatua ya awali. Amunike alitua nchini mwaka jana na kuchukua mikoba iliyoachwa na Mzalendo, Salum Mayanga, ambaye naye alianza kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Lesotho wakati Stars ilipokuwa inasaka tiketi ya kushiriki fainali za Afcon ambazo zinaendelea nchini Misri.

Mnigeria huyo aliiongoza Stars katika mechi 10, ameshinda mbili, ametoka sare mbili na amepoteza michezo sita.

# Simba, Yanga dimbani Jan.4

**Na Shufaa Lyimo**

●●● Pazia la Ligi Kuu Bara 2019/20 linatarajiwa kufunguliwa rasmi Agosti 23...

WATANI wa jadi nchini, Simba na Yanga wanatarajia kukutana katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019/20 utakaochezwa Januari 4 mwakani kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, imefahamika.

**Hata hivyo, mechi ya marudiano kati ya timu hizo mbili ambazo zitashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika bado haijapangiwa tarehe.**

Akizungumza jana jijini, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura, alisema kuwa mchezo huo wa watani wa jadi utakuwa ni wa raundi ya 13, huku Simba ikishuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa bao 1-0 ambao waliupata katika mchezo wa mwisho wa msimu uliomalizika.

Wambura alisema kuwa msimu mpya wa Ligi Kuu utaanza ifikapo Agosti 23 mwaka huu na ratiba ambayo imetolewa imezingatia ushiriki wa klabu za Bara katika mashindano ya kimataifa, huku mchezo wa Ngao ya Jamii kati ya mabingwa watetezi, Simba dhidi ya Azam FC ambao ni washindi wa Kombe la FA utachezwa Agosti 17.

"Mchezo wa raundi ya 13 wa watani wa jadi, Simba na Yanga utachezwa Januari 4 mwakani, naamini ni mchezo ambao unasubiriwa na mashabiki wengi wa soka hapa nchini," alisema Wambura.

Alisema kuwa mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba wataanza msimu mpya kwa kutetea taji hilo kwa kukutana na "Maafande" wa JKT Tanzania wakati Yanga yenyewe itacheza dhidi ya Ruvu Shooting kutoka mkoani Pwani.

"Tumechelewa kutangaza ratiba ya Ligi Kuu msimu ujao, kwa sababu tumehakikisha tumeipanga kwa ubora zaidi ili kusiwapo na michezo mingi ya viporo kama iliyokuwa msimu uliopita, hatutaki mambo kama hayo yajirudie tena, tumezingatia kalenda ya mashindano ya kimataifa," alisema mkurugenzi huyo.

Kiongozi huyo pia alizitaka klabu zote zinazoshiriki ligi hiyo kuhakikisha zinasajili vikosi imara ili waweze kutoa ushindani katika michezo yote na kueleza kwamba hakutakuwa na mabadiliko ya ratiba ya mara kwa mara kama ilivyozoeleka.

Alisema pia Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) itakutana hivi karibuni kujadili mfumo na kanuni za uendeshaji wa ligi hiyo ikiwa pamoja na kujadili changamoto za viwanja ambayo msimu uliopita ilibainika kuwa na matatizo.

Wambura alisema katika kuhakikisha inazipunguzia klabu gharama za uendeshaji, timu zitakuwa zikicheza mechi zake zote katika kanda au mkoa mfululizo na si kwenda na kurudi.

Bila ya kutaja majina, alisema kuna baadhi ya viwanja tayari bodi imevikataa na kuzielekeza timu kuvifanyia marekebisho ili viweze kutumiwa katika ligi hiyo inayotarajiwa kumalizika ifikapo Mei 24 mwakani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >